ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.

11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.

22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani

35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni

57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tatu - Tarehe 24 Januari, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kuweka mezani hotuba ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya 2012/2013.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya 2012/2013.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani hotuba ya ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya 2012/2013.

Naomba kuweka mezani.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Zanzibar.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 7

Matumizi ya Fedha Zinazolipwa Katika Uhaulishaji wa Ardhi

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza**:-**

Miongoni mwa taratibu za kuhaulishaji wa ardhi ni pamoja na kulipa kiasi cha fedha kwa Shehia na Wilaya husika, ambapo mhaulishaji hutakiwa kulipa Tsh. 20,000/- kwa Sheha na Tsh. 30,000/- kwa Mkuu wa Wilaya. Je fedha hizi hutumika kwa utaratibu upi na kwa misingi ipi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli katika fomu za uhaulishaji wa ardhi kuna ada ya uhaulishaji ya Shs.20,000, katika ngazi ya Shehia na Shs. 30,000, katika ngazi ya Wilaya. Ada na viwango hivyo, vimo katika Tangazo la Serikali Namba 70 la mwaka 2011 ambalo limetoa ruhusa ya kukusanya kiwango hicho cha fedha katika ngazi za Shehia na Wilaya.

Mhe. Spika, fedha zinazokusanywa katika ngazi ya Shehia na Wilaya hutumika katika kugharamia vikao na shughuli nyengine zinazojadili maombi ya uhaulishaji na gharama nyengine zinazohusiana na uhaulishaji katika ngazi hizo.

Mhe. Spika: Kabla sijamuomba Mjumbe kuuliza swali la nyongeza, naomba nitoe taarifa kwamba mitambo yetu kuanzia *row* ya mbele hapa moja, mbili, tatu; yaani *row* ya Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa yote hii ninaambiwa haifanyi kazi, tatizo ni lile ambalo nimelisema *vibration* inakuwa kubwa inaleta *disconnection* ya vyombo vyetu. Kwa hivyo nimeambiwa kwamba akitokezea Mjumbe ana jambo katika eneo hilo itabidi a-*move* sehemu nyengine ili kutumia *microphone*.

Waheshimiwa Wajumbe ninaendelea kuhimiza tuweke nidhamu sana unapopiga mabao haya tuwe tunapiga mabao kwa utaratibu vyombo vyetu vinatetereka, lakini juu ya hivyo tunawaomba mafundi wanayarekebisha mambo haya mapema kabla ya kuingia katika shughuli zetu. Ndio taarifa nilizopewa hivi sasa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Napenda kumuuliza Mhe. Waziri fedha zote hizo zinazokusanywa na taasisi yoyote ya serikali hupelekwa katika mfuko wa serikali. Je, Masheha wanafanya hivyo.

(b) Je, fedha hizi zinakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

a) Ni kweli fedha nyingi zinazokusanywa kwa madhumuni ya mapato na matumizi ya serikali hutakiwa ziende katika mfuko mkuu wa Hazina, lakini kama nilivyosema kwamba ada inayokusanywa katika ngazi za Shehia na Wilaya imo katika tangazo la serikali Nam. 70 la 2011.

Na tangazo la serikali inakuwa ni *Legal Notice* ya kisheria ambayo imehalalisha jambo kuweza kufanyika. Sasa hizi zinazokusanywa zimeshatolewa utaratibu wake ni huu. Kwa hivyo hakuna kosa katika kutumika kwenye jambo ambalo limehalalishwa na tangazo rasmi la serikali. Maana yake kama limehalalishwa na tangazo rasmi la serikali, maana yake sheria nyengine zinazohusika au taasisi nyengine zinazohusika zitakuwa zimeridhia kufanyika kwa jambo hili.

b) Suala la ukaguzi fedha yoyote ya serikali Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa aifanyie ukaguzi. Kwa hivyo hakuna tatizo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenda kufanya ukaguzi katika mapato na matumizi ya fedha hizi.

Nam. 22

Kufunguliwa Kituo cha Afya cha Kijiji cha Kibokoni – Wawi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza**:-**

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali Nam. 22 la Mwakilishi machachari Mhe. Saleh Nassor Juma ninataka kutoa utangulizi mdogo, pamoja na serikali nia yake kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ni Hospitali ya Rufaa, lakini bado hali imekuwa ni tete katika hospitali hiyo ya rufaa inayotegemewa kuitwa ya Mnazi Mmoja kwa muda mrefu *CT Scan* haifanyi kazi na hadi hivi sasa *X-ray* haipatikanani.

Baada ya maelezo hayo pengine wahusika labda hawana taarifa naomba kuchangia suala hilo na naomba swali Nam. 22 lijibiwe.

Kwa kuwa wananchi wa kijiji cha Kibokoni katika Jimbo la Wawi wako mbali na Hospitali ya *Vitongoji Cottage*, na kwa kuwa katika miaka ya 1990 walihamasika kuanzisha jengo la kituo cha afya ambacho kiliwekewa jiwe la msingi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wakati ule, ambaye sasa ni Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein, na kwa kuwa kituo hicho tayari kimemalizika katika hatua zote za ujenzi pamoja na kuwekewa umeme.

Je, ni lini Wizara ya Afya itakifungua rasmi kituo hicho na kuanza kutoa huduma.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika Jimbo la Wawi lina wakaazi wapatao 15,517 na Shehia ya Kibokoni ina wakaazi wapatao 2612. Jimbo hilo lina hospitali kubwa ya Vitongoji (*Vitongoji Cottage Hospital)* ambayo imo katika mchakato kupandishwa daraja na kuwa ya Wilaya

Vituo vya Afya vipatavyo vitano (5) navyo ni kama ifuatavyo:-

1. Vitongoji Jeshini
2. Kituo cha Afya JKU
3. Kituo cha Afya Uwandani
4. Kituo cha Afya Mvumoni
5. Kituo kidogo cha huduma Fidel Casro

Mhe. Spika, Wizara ya Afya imefanya juhudi za makusudi za kuwapanga wafanyakazi katika Vituo hivyo kama ifuatavyo:-

Vitongoji Jeshini Wafanyakazi 5
Psy/N - 1, PHNB -2, MCH - 1 na L/Asst – 1.
Muuguzi wa afya ya akili, wauguzi wawili wa afya ya jamii, muuguzi wa afya ya uzazi na mtoto, mafundi sanifu msaidizi maabara.

Kituo cha Afya JKU
Kuna wafanyakazi wawili; muuguzi wa afya jamii, muuguzi wa afya ya wazazi.

Kituo cha Afya Jeshini
PHNB -1 na MCH -1

Kituo cha Afya Uwandani
PSY/N -1, PHNB -1, H/Asst -1, na H/*Oderly* -1
Kuna wafanyakazi wanne; muuguzi wa afya ya akili, muuguzi wa afya ya jamii, bwana afya msaidizi na mhudumu.

Kituo cha Afya Mvumoni
PSY/N -1, L/Asst -1, PHNB -1 na MCH-Aid 1
Kuna wafanyakazi wanne; muuguzi wa afya akili, fundi sanifu maabara, muuguzi wa afya jamii na muuguzi wa afya ya uzazi na watoto

Fidel Castro
SNMW -1
Kuna muuguzi mmoja ambaye ni mkunga muuguzi.

Pamoja na jitihada hizo pia Hospitali ya Vitongoji ina wafanyakazi 51. Pamoja na jitihada hizo za wizara bado tatizo la raslimali watu lipo sambamba na upungufu wa vifaa na madawa vinavyokabili vituo vyetu hivyo pamoja na hospitali.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya inafuata maelekezo ya Shirika la Afya (WHO) ambalo limeelekeza kwamba ili huduma za afya ziwe karibu na wananchi umbali wa kituo kimoja na chengine kisizidi kilomita tano.

Mhe. Spika, katika Jimbo la Wawi umbali kutoka kituo kimoja hadi chengine ni chini ya kilomita 3, na kutoka Kibokoni hadi Vitongoji *Cottage* chini ya kilomita 4. Kibokoni hadi hospitali au kituo cha afya Vitongoji jeshini barabara ni nzuri. Sambamba na hilo Timu ya Afya ya Wilaya ya Chake Chake ina utaratibu wa kutoa huduma mchanganyiko za mkoba katika eneo la Shehia ya Kibokoni mwezi mara moja zikiwemo za chanjo, uchunguzi wa afya na huduma za mama wajawazito.

Mhe. Spika, huko nyuma tulipojibu suala hili hili tulipendekeza kwamba kwa vile Hospitali ya Vitongoji inapandishwa daraja na kutakuwa na wafanyakazi wengi wanaohitaji makaazi, tulishauri jengo hilo lingekuwa nyumba ya kuja kuishi wafanyakazi ili tuweze kuboresha huduma katika Hospitali ya Vitongoji, lakini pia haitowazuia watu wa Kibokoni inapotokea dharura

kwenda kuwataka wafanyakazi hapo ili wawasaidie. Kwa hivyo bado wizara inawanasihi watu wa Wawi na hasa watu wa Kibokoni kukubaliana na ushauri wetu huo ambao utakuwa na manufaa zaidi kwa sote.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kwa heshima, taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana niulize swali dogo kama ifuatavyo.

Kwa kuwa wananchi wa Kibokoni wakati wanajenga kituo kile walijenga kwa dhamira ya kituo cha afya, na wakatoa taarifa serikalini na hatimaye Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kama nilivyosema awali kwa siku zile ndio Rais wa nchi hii, akaenda akaweka jiwe la msingi.

Na kwa kuwa wananchi wa pale hawakukusudia kwamba jengo lile liwe ni nyumba ya wafanyakazi, wao walitaka iwe ni kituo cha afya. Je, kulifanya jengo lile nyumba ya wafanyakazi wa hospitali badala ya hospitali si kwenda kinyume na matarajio waliotarajia wananchi wa Jimbo la Wawi hasa pale Kibokoni. Hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa hawa hawakutaka jengo lile liwe nyumba ya wafanyakazi na badala yake walitaka ni *dispensary*, kuachia nguvu zile zikapotea hivi hivi si kuwadhalilisha wananchi wa lile jimbo na hatimaye kuwavunja moyo katika kuleta maendeleo ya nchi hii,

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Nchi hii na serikali yake katika mawizara kuna taratibu. Huduma zinatakiwa zimfikie kila mwananchi katika nchi hii na ikiwezekana kwa usawa. Leo hii kuna baadhi ya sehemu ambapo huduma hii haijafika kwa ukosefu wa wafanyakazi na ukosefu wa vifaa vya afya, wanakwenda zaidi ya kilomita 10 kufuata huduma.

Sisi kama tuliopewa jukumu la kuhakikisha kwamba huduma inamfikia kila mtu, tuna taratibu ya kuangalia wapi kuna mahitaji ya zaidi tuanze na wao wasipate usumbufu kama ambao wananchi wa Jimbo wa Vitongoji hawapati.

Kama katika jimbo moja kuna vituo 5 na hospitali kubwa ya wilaya, wakati mwengine hata kituo cha afya hakipati, kweli tutachukua wafanyakazi tukawapeleke Kibokoni wakati wengine wanakwenda kilomita 10 kufuatilia hayo.

Sasa ushauri tulioutoa, tunajua kilichofanyika wala hatuna nia ya kudharau isipokuwa tunachotaka nchi hii watu wote wapate haki sawa kwa wote. Sasa kama haki sawa kwa wote basi wote wapate afya iliyo bora kwa kupelekewa wafanyakazi na kupelekewa vifaa na madawa. (*Makofi*).

Sasa sisi tunapogawa wafanyakazi kwa ajili ya kufungua vituo tunaangalia hilo, hatuangalii majengo mangapi yapo wapi, lakini bado tunawasihi wananchi wa Kibokoni kwamba ukiangalia uhalisia wa huduma ya afya wanazozipata, basi wanapata kuliko wengine wengi. Kwa hivyo itachukua muda sisi hata kama tunataka kufanya kituo afya, mpaka tutakapohakikisha na wengine wamepata na huduma nyengine hizo zinazostahiki, labda sina uhakika,lakini bado tunasema kwamba kile kituo kufunguliwa pale kwa kweli tunafanya jambo ambalo halitostahiki wakati huduma zipo hapa na pale. Kwa hivyo kwa sasa hivi mpango wa kufungua kituo kile hatuna, tutaendelea kufungua vituo vyengine ambavyo bado vina mahitaji makubwa ya masafa marefu kwenda kituo chengine au kina upungufu wa wafanyakazi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninashukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Vitongoji hasa Kibokoni walitoa ushauri na wakaelekezwa na serikali kama waendelee na jengo, na kwa kuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye kuwa ni Rais wa Zanzibar kwa sasa ndiye aliyekwenda akaweka jiwe la msingi wa lile jengo.

Je, Mhe. Naibu Waziri haoni kama wananchi wa Vitongoji wale walishauri vibaya kama walishauri na halafu hawataki kulifungua hili jengo likawa hospitali.

Pili je, kama jengo lile sasa hivi wizara inasema ni nyumba ya madaktari. Je, serikali itawalipa wananchi wa Kibokoni fedha wanazotaka kwa jengo kuwa ni nyumba ya daktari au je, madaktari watakaa tu kwa sababu ni jengo limejengwa na wananchi bure.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Maswali sikuyafahamu.

Mhe. Spika: Rudia maswali kwa utaratibu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri hao wananchi wa Kibokoni walipolijenga hili jengo. Je, hawakuomba ridhaa au ushauri kwa Wizara ya Afya, na kama waliomba wakashauri kama wajenge hawaoni kutolifungua jengo lile kuwa kituo cha afya watakuwa hawawatendei haki.

Na je, kwa kuwa wizara inataka lile jengo hivi sasa liwe ni nyumba ya madaktari, na wakati wananchi walijenga kama ni hospitali au kituo cha afya. Je, Wizara ya Afya italinunua jengo lile kwa fedha wanazotaka wananchi au

kuwapa madaktari wakakaa kwenye jengo, wakae bure tu kwa sababu wananchi wameshapoteza nguvu zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Sina uhakika kama kilipojengwa kituo cha Kibokoni waliomba ridhaa kwa sababu Wawakilishi wanatoa ahadi na wanajenga vituo bila ya wizara kuwa na taarifa. Na hilo ndilo lililopelekea wizara kwa amri ya serikali kusema kwamba yeyote anayetaka kujenga kituo aende Wizara ya Afya akapate ridhaa tuangalie kweli kuna uhalali wa hicho kinachoombwa kujengwa pale kulingana na hali halisi ya mahala pale na mahitaji yale na wingi wa watu waliopo sehemu ile.

Kwa hivyo kama kilipojengwa waliomba ridhaa, mimi hilo uhakika nalo sina lakini mgeni rasmi alialikwa kwenda kuweka jiwe la msingi, sidhani kama anajua kwamba kituo hicho kilikuwa na ridhaa au hakina, lakini jiwe la msingi limeekwa, hatukatai, lakini kweli Mhe. Spika, watu 2,616 hospitali sita wakati wenziwao elfu zaidi ya tano hawana kituo. Hivyo kweli kuna uhalali wa kufanya hilo.

La pili, wamelipa pesa kwa sababu kituo tumeangalia tumeona kwamba ulazima wa kituo kile kutokana na hali halisi haupo, na siku zote wakijenga vituo wakimaliza wanaikabidhi Wizara ya Afya. Kwa hivyo jengo la Kibokoni linakabidhiwa Wizara ya Afya, linakuwa tena si la wananchi, linakuwa ni jengo la serikali kwa sababu sisi ndio tunaolitunza, sisi ndio tunalipia umeme, maji, na sisi ndio tunaoweka vifaa na madaktari.

Kwa hivyo wao walijenga tunakubali, na wengi wanajenga lakini ikishakabidhiwa Wizara ya Afya linakuwa sio lao tena, linakuwa ni la serikali. Sasa kama ni jengo la serikali tena tunamlipa nani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwa vile wananchi wa Vitongoji Umangani, Kibokoni wanaishi Shehia ya Chake Chake na hospitali kuu ya Chake Chake hivi sasa haina daktari wa mifupa na hivi sasa tunajadili mswada wa karafuu.

Je, wizara ina mpango gani wa kupeleka daktari wa dharura kule kutibu mifupa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Daktari wa nini.

Mhe. Spika: Rudia swali Mheshimiwa. Ielekee hiyo *microphone* ili sauti itoke vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa vile wananchi wa Kibokoni, Wawi, Umangani wapo katika Shehia ya Chake Chake na hospitali kubwa ya Chake Chake kwa muda huu hauna daktari bingwa wa mifupa, wamekuwa wakipata shida na hivi sasa tunajadili mswada wa karafuu na wengi kule huanguka kwenye mikarafuu.

Serikali au wizara ina mpango gani wa dharura wa kupeleka daktari wa kutibu mifupa.

Mhe. Spika: Hili Mheshimiwa unakusudia kwamba maeneo hayo katika Shehia au Wilaya ya Chake Chake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Katika Wilaya ya Chake Chake.

Mhe. Spika: Eeh! sawa. Mhe. Naibu Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Hospitali ya Chake Chake kuna sajenti pale ambaye kasomea mambo ya upasuaji na mambo mengine yote hayo anayashughulikia. Yupo Daktari Shaaban.

Mhe. Spika: Inaelekea umemaliza Mheshimiwa. Tunashukuru tunaendelea.

Nam. 5

Vijana Kujiingiza katika Vitendo Viovu

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hutegemea sana wananchi wake, wakiwemo vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa letu, lakini hivi sasa imejitokeza tabia ya baadhi ya vijana wa kiume kujiingiza katika vitendo vichafu vya kufanya tendo la ndoa kinyume na maumbile. Vijana hao hivi sasa wanaiendeleza tabia hiyo kwa kuwaharibu wenzao ambao ni wadogo sana jambo ambalo ni la kusikitisha sana na la kupigwa vita. Je, Serikali imejipanga vipi katika kulichukulia hatua jambo hilo ambalo linaathiri sana jamii yetu na mustakbali wa taifa letu.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, pia nishukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uwezo wa kusimama mbele ya hadhara hii ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ninakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba serikali hutegemea sana wananchi wake wakiwemo vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa letu. Serikali inakerwa sana na tabia iliyojitokeza kwa baadhi ya vijana wa kiume kujiingiza katika vitendo vichafu ikiwemo kufanya tendo la ndoa kinyume na maumbile.

Ninapenda nimjuulishe Mhe. Mwakilishi kuwa jukumu la serikali katika suala hili ni kutoa elimu kwa vijana. Wizara yangu imekuwa ikitoa mafunzo kwa vijana ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazoathiri afya zao, ikiwemo vishawishi vinavyowapelekea kujihusisha na vitendo vichafu na matumizi ya madawa ya kulevya.

Hata hivyo ni vyema ikaeleweka kuwa serikali peke yake haiwezi kumaliza tatizo, wazazi kwa upande wao wana jukumu kubwa la kuwafunza vijana wao juu ya maadili mema, kufuatilia nyendo zao na kuwa karibu nao ili kutambua matatizo yao. Hivyo mashirikiano ya kila mmoja wetu yanahitajika katika kukabiliana na tatizo hili ambalo linaathiri jamii yetu na mustakbali wa taifa letu. Ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa sisi walezi na wazazi wengi huwaachia watoto wetu kulala nyumba za mageto, yaani kwa vijana wale wanaolala katika nyumba zile za mageto. Je, Mhe. Waziri unawaambiwa nini wazazi na walezi ambao watoto huwaachia kulala majumba hayo.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Ninawaambia wazazi na walezi wasiwaachie watoto wao kulala katika nyumba za mageto hiyo ni hatari kwa watoto na kwa sisi wazazi pia ni hatari.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, kabla sijauliza swali langu, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri afanye marekebisho katika jibu la msingi alilokuwa akijibu alipozungumzia kuhusu wale wanaofanya tendo la ndoa kinyume na maumbile. Kufanya tendo kinyume na maumbile sio tendo la ndoa ni tendo la ngono. Kwa hivyo, namuomba pale arekebishe ile lugha, kwa sababu ukisema tendo la ndoa ina maana kama tunahalalisha madukhuli

ya tendo lile kwa nyuma inakuwa kama ndoa. Kwa hivyo, naomba suala hili atakapokuwa ananijibu swali langu naomba arekebishe. Nawaomba na watendaji vile vile wanapotujibia maswali haya, basi waweze kutofautisha baina ya ngono na tendo la ndoa.

Mhe. Spika, baada ya marekebisho hayo, naomba Mhe. Waziri anijibu swali langu kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama swali la msingi la Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi linavyoeleza, kwamba kwa kweli sasa hivi Zanzibar matendo haya ya watu kufanya vitendo kinyume na maumbile vimekuwa ni vingi sana. Hata katika kikao kilichopita, Mhe. Mgeni Hassan Juma alileta hoja na hoja ile tulikuwa tunaizungumzia zaidi katika namna gani ya kuweza kudhibiti matendo haya.

Je, Mhe. Waziri uko tayari kuweka sheria ya kumfunga mtu kifungo cha maisha kwa yeyote atakayefanya au atakayegundulika amefanya tendo la ngono kinyume na maumbile? Ahsante Mhe. Spika.

.

Mhe. Spika: Ni kweli hata hilo swali lenyewe limetaja hiyo ndoa. Kwa hivyo, nadhani tunakubaliana kwamba kweli lilikuwa ni koseo kwa sababu ndoa ni kitu cha halali. Au sio?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndioo!

Mhe. Spika: Basi narekebisha swali lenyewe pamoja na yale majibu, kwamba sasa pale ambapo palikuwa pametajwa ndoa, basi itakuwa ni ngono. Haya Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hamza wa Jimbo la Kwamtipura swali lake kama hivi ifuatavyo. Lile swali la mwanzo alisema niseme tendo la ngono. Mimi nasema tendo la ndoa, kwa sababu ndivyo swali lilivyoulizwa, kwa hivyo nimeona nijibu hivyo. Sasa hayo mambo ya ngono tutakuja kujibu wakati mwengine tukijaaliwa. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, hebu kidogo. Spika, amesharekebisha hiyo kwamba ni kweli ndoa ni kitu cha halali, kwa hivyo ukitaja ndoa maana yake ndoa ya kinyume na maumbile mimi sijui. Haya tuendelee.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kama nilivyojibu majibu yangu mwanzo. Wazazi pamoja na serikali tutawaelimisha vijana wetu na wazazi wawe karibu na

watoto ili jambo hili tulishughulikie ipasavyo lisifanyike katika nchi yetu sio jambo zuri.

Kuhusu hayo mambo ya sheria baadae huko usoni labda mambo tukijaona yamezidi zaidi, ndio pengine tunaweza kuja kuunda sheria, lakini kwa sasa hivi bado kidogo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuingia hapa katika hali ya afya njema kwa mintarafu ya kujenga taifa letu.

Mhe. Spika, kwa kuwa tulipata semina mbali mbali katika mambo haya ya vijana wetu, na kwa kuwa Mhe. Mgeni Hassan Juma alileta hoja maalumu tukazungumzia mambo mengi sana. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba yale mambo ambayo yalizungumzwa kwenye semina na kutoa hoja kwa Mhe. Mgeni Hassan, yatafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili kulinda vijana wetu wanaopotoshwa kwa makusudi kwa lengo la kuwajenga vijana wetu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Asha Bakari Makame kwamba sasa hivi tumo tunashughulika katika mambo yote tuliyofanya kwenye semina na maelekezo yote yaliyofanywa kwenye semina yote tunayashughulikia. Kwa hivyo, baadae nadhani huenda tukakaa pamoja na kuyazungumza kwa pamoja ili angalau yaweze kutusaidia katika majanga haya yalioko mbele yetu. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 13

Ukosefu wa Huduma ya Maji na Umeme Baada ya Miaka 50

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Wakati Mapinduzi ya Zanzibar yametimia miaka 50 hivi karibuni na wananchi wanaendelea kusherehekea Mapinduzi hayo pamoja na matunda ya Mapinduzi.

Je, kusherehekea huko wakati wananchi hadi hii leo hawana maji wala umeme ama yote au moja kati ya hayo ni kuwatendea haki.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu :-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 13 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, miongoni mwa malengo ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ni kuwapatia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji katika kipindi cha miaka 50 ya Mapinduzi inaendelea na kuwapatia wananchi huduma hiyo ya maji safi na salama, kwa kupitia miradi mbali mbali inayohifadhiwa na serikali, nguvu za wananchi pamoja na washirika wa maendeleo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa sababu katika bajeti ya mwaka 2011/2012 na katika bajeti ya mwaka 2012/2013 wizara hii iliahidi kupeleka maji safi na salama katika Shehia ya Mtambwe Kaskazini. Hadi hii leo ukiachilia mbali zile sehemu ambazo tulipeleka kwa uwezo wetu. Kuna kijiji kama Chanjaani, Kidundo, Chekea mpaka leo hawajapata maji.

Vile vile tukitizama Shehia ya Mtambwe Kusini, kuanzia Makoongeni, Mitambuni mpaka Kinazini, ni sehemu kubwa sana hiyo hakuna maji, hakuna umeme na hakuna lolote. Kisiwani kuna Mleteni na Malindini hali ni hiyo hiyo.

Mhe. Spika, swali langu ni kwamba kwa sababu siku zote mimi huwa nazungumza sana tena kwa ukali, ili nione watu hawa wametendewa haki ya kupata maji safi na salama, kwa vile nawasikia Wajumbe wenzangu wanasema wana maji mpaka hawana vya kuyafanya.

Je, ni kwa sababu wananchi hawa wanakaa katika Jimbo la Mtambwe ndio mpaka leo wakaachiwa katika hali hii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati: Mhe. Spika, Mapinduzi matukufu ya miaka 50 yamefanya kazi kubwa sana katika Jimbo la Mtambwe. Kama mtu atakuja leo umshushe Bahanasa, umwambie nenda Mtambwe basi akifika Bwagamoyo atapotea hajui apite njia ipi. Kumeteremshwa barabara mpaka chini bondeni, kuna njia panda nyingi za barabara ambazo zinaendelea na kazi sasa hivi. Hapo Bahanasa kama atakuja leo mtu katika Jimbo la Mtambwe, basi hapo Bahanasa atakuta kuna tangi la maji jipya limejengwa na UNDP kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa eneo lile.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba ni wajibu wake kuwatumikia wananchi wa Chanjaani, Kilundo, Chekea, Makongeni, Kisiwani na kadhalika na ni wajibu wake kuuliza kila kitu ili ayaone mambo haya yanatekelezwa. Ninamuahidi tutaendelea kutekeleza kwa uwezo wa serikali na wote watapata maji tukiweza kukamilisha miradi yetu. Ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa mradi ule wa maji uliopo pale alipozungumza. Nilipozungumza mimi ni vijiji vile ambavyo nimevitaja, yaani Kinazini, Mitambuni, Makoongeni, Chanjaani, Kidundo, Chekea, Mleteni na Malindi vyote hivi havitofaidika na maji hayo aliyoyataja.

Kwa hivyo, nimezungumza hapa makusudi najua kuna mradi huo na ulikuwemo katika bajeti, lakini na huku vile vile ulikuwemo katika bajeti na hawakushughulikiwa, wala maji hayo hayafiki huko ni mbali sana na ni shehia tofauti.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, majibu umeshapata ukae kitako. Tunaendelea.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nataka kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya jitihada kubwa katika kuwaletea maendeleo wananchi wake na hususan katika suala la maji, lakini pamoja na jitihada za serikali kuna jitihada za Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi. Kwa bahati nzuri kuna mradi wa SEMUSO ambao ulilipiwa, lakini kulitokezea mgogoro baina ya wizara na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto palijengwa kisima pale Wazee, lakini tatizo lile limeshapatiwa ufumbuzi.

Nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwamba baada ya kupatiwa ufumbuzi kwa kuchimbwa kisima kile pale kwa Wazee. Je, ni nini kilichokwamisha hadi leo kisima kile kikawa hakijaanza kuchimbwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama alivyoelezea Mhe. Mwakilishi kuwa palikuwa na kasoro ndogo tu kati ya Mamlaka ya Maji na wenzetu wa upande wa pili, lakini pamoja na hayo kasoro zile tumeshaziweka sawa na wakati wowote tutakishughulikia kisima kile ili wananchi wa eneo lile wapate huduma hiyo ya maji safi na salama. Namuomba Mhe. Mwakilishi avute subra kidogo, wizara yangu inalisimamia suala hili kikamilifu na sio muda mrefu tutaliweka sawa.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jinsi inavyojitahidi kutekeleza wajibu wake kuhusu habari ya maji na umeme. Kwa kuwa hivi karibuni tulikuwa hatuna umeme wa uhakika na serikali ikahakikisha imeweka umeme wa uhakika. Kwa kuwa wananchi walikuwa wanalalamika Mhe. Spika, kuhusu maji, lakini kwa kweli kuna miradi mbali mbali ya maji.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri je atakubaliana na mimi kwamba pamoja na kutimiza miaka 50 tukiangalia maendeleo ya nchi hii ya maji na umeme, yameleta ufanisi kwa jumla katika nchi yetu hii?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuhusu suala hili.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu ya Mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika. Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa na kuvuta pumzi zake alizoniazima, huu sio ujanja wangu wala sio uwezo wangu, hii ni neema kubwa aliyonijaalia Mwenyezi Mungu, namshukuru.

Baada ya hapo Mhe. Spika, bila ya kupoteza muda nimshukuru Waziri wa mwanzo Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, nataka nimsifu akiwa hai na mimi hai. Wengi wetu tuna tabia baada ya kwisha kufa mtu ndio anaambiwa alikuwa mzuri yule, kwa jitihada anazochukua Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na ni Waziri wa mwanzo kupandisha bei ya karafuu.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa 19 naomba kuunukuu;

"mtu yeyote ambaye atakusudia kuhamisha karafuu kavu au mbichi au makonyo ya karafuu kutoka sehemu moja kwenda nyengine, basi atatakiwa kuomba kibali cha Sheha kitakachokuwa katika fomu maalum".

Mhe. Spika, huu utakuwa ni unyanyasaji, hiki kifungu Mhe. Spika, mimi ningeomba kifutwe. Haiwezekani mkulima leo anakaa Mkoani ana shamba lake Wete, atamtafuta Sheha na masheha ofisi hawana na huku karafuu

zinaharibika. Kifungu hiki mimi ningeomba kikaangaliwa kwa uangalifu kabisa, kitaweka urasimu mkubwa.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije katika kifungu cha 13(1), serikali lazima itoe elimu ya kutosha kwa sababu kifungu hiki kinamkataza mtu kukata mkarafuu kwa madhumuni ya kutengeneza makaa au kuchimba mawe karibu na mkarafuu au kuchimba udongo.

Mhe. Spika, wananchi wetu wengi uelewa wao ni mdogo na sio wengi wanaosikiliza Baraza la Wawakilishi hasa vijijini. Kifungu hiki ningeomba kikaangaliwa na adhabu iliyotumika ya Shs. 3,000,000 kwa wananchi wa Pemba ni adhabu kubwa sana, naomba kifungu hiki kifikiriwe na kiangaliwe.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije kwenye kifungu cha 18(1)(2) kuzungumza masharti anayotaka kuchuma karafuu na kuanika vifaa. Hapa wizara haikuweka wazi kuhusu karafuu, wengine wanaanika juu ya mapaa, wengine barabarani na wengine kwenye majamvi, ilikuwa iainishwe ni zana gani zinazotakiwa kutumika hapa.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nije na kilio kikubwa cha wachukuzi hasa kisiwani Pemba. Mimi ni Mjumbe wa kamati hii, tulikutana na wachukuzi kwa muda mrefu wana kilio cha bei ya kupandishiwa ubebaji wao wa magunia. Ukiwakuta watu wale kutokana na umri wao ni miaka 50 na 60 na kuendelea, wanalia kuhusu bei za ubebaji zimekuwa ni ndogo mno na wanafanya kazi katika mazingira ya kutatanisha, na ukizingatia bandarini kule kwa muda mrefu Pemba hakuna *crane* wanatumia vifua vyao tu, ni watu wanyonge sana wale.

Jengine ni suala la mageti Pemba. Suala hili limekuwa kero kubwa sana, mita kumi unakuta geti na mita kumi na tano geti, kweli karafuu zikapitishwe mchana mule, mimi sifikirii na suala hili la mageti linawasumbua sana wananchi wa kule Pemba.

Jengine Mhe. Spika, ni kuhusu usafiri kutoka vijijini hadi kuelekea kunakouzwa karafuu. Suala hili nalo liangaliwe kwa sababu wananchi wanapata shida kutoka vijijini kuhusu usafiri. Halafu tumeshuhudia mara nyingi katika ukamataji wa karafuu, zinakamatwa karafuu tu lakini wahusika hawapatikani mara nyingi sana, sijui tatizo liko wapi. Karafuu zinapatikana lakini mkamatwaji hapatikani, sijui tumejifunza nini kuhusu suala hili.

La mwisho Mhe. Spika, kuna mashamba walipewa watu wayaendeleze kule kwa muda mrefu. Nafikiri hivi sasa kuna sehemu vinauzwa viwanja, hayo mashamba yenyewe sijui kama yapo tena mpaka leo.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna sera hapa hasa wenzangu wa kambi ya upinzani walikuwa wakipigia kelele sana kuhusu kubinafsishwa hii sekta ya *ZSTC*. Je, wazo hili bado lipo au litaendelea vile vile. Kwa haya machache Mhe. Spika, mpaka nitakapopata maelezo ndio nitaunga mkono hoja hii.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa asubuhi hii ya leo na mimi kunipa fursa ya kuchangia hoja iliopo mbele yetu. Kwanza Mhe. Spika, napenda niishukuru serikali kwa kupitia Shirika la *ZSTC,* kama walivyozungumza wenzangu kwa kuongeza bei ya karafuu na wananchi wakajisikia kama kweli kumbe zao lao hili la karafuu lina thamani.

Mhe. Spika, kama walivyotangulia kuzungumza wenzangu, wamezungumza mengi na mimi sina budi niongeze mawili au matatu. Mhe. Spika, kama tunavyojua zao hili la karafuu kwa visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba ni zao muhimu sana na ni zao ambalo wananchi ukifika msimu wa karafuu, basi wananchi walikuwa wajua kwamba hiki ni kipindi changu cha kufanya shughuli zangu ambazo nitawezeshwa na Mwenyezi Mungu. Aliyekuwa na harusi ya mwanawe basi alikuwa anajiandaa kufanya harusi kwa zao la karafuu, aliyekuwa anataka kukopa shamba alikuwa anajiandaa kwa zao la karafuu, aliyekuwa na maulidi alikuwa anajiandaa kwa kujua kuwa kuna msimu wa karafuu, aliyekuwa na hitima ya wazee wake alikuwa anajiandaa kwa kujua kuwa kuna zao la karafuu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili zao la karafuu ni zao ambalo ni muhimu sana na watu walikuwa wanalitegemea na bahati nzuri zao hili la karafuu ukifika msimu wa karafuu basi aliyekuwa na mikarafuu, aliyekuwa hana mikarafuu basi ilikuwa neema hii inaenea kwa watu wote. Kwa sababu aliyekuwa hana shamba na mikarafuu, basi ni mchumaji wa karafuu, aliyekuwa sio mchumaji ni muanikaji wa karafuu, kwa hivyo neema hii ilikuwa imeenea kwa watu wote.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa siku zinapita na kuna mabadiliko ya tabia nchi kila leo kunakuja hali ya mabadiliko ya nchi, lakini Mhe. Spika, naiomba sana wizara hii kwa kupitia Shirika hili la *ZSTC*, ione kwamba kuna umuhimu wa kurudisha ile hadhi waliyokuwa nayo watu ya kuipa thamani zao hili la karafuu, kwa sababu ni uti wa mgongo wa uchumi wetu tukitaka tusitake. Kwa sababu utalii unasaidia katika nchi yetu, lakini ni kitu cha msimu ni cha kupita, sio kitu cha kutegemea sana tukawabwaga machoke mpaka tukamaliza.

Mimi napendelea tubwage sana machoke kwenye zao letu hili la karafuu, kwa sababu huu ni uti wa mgongo na ni hazina tumepewa na Mwenyezi Mungu ipo, lakini utalii Mhe. Spika, ni kitu cha mpito, naomba sana hili zao

la karafuu tulitilie nguvu sana na tuone kuwa ni zao ambalo linasaidia uchumi wa nchi yetu. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na jitihada waliyofanya serikali ya kuongeza bei na ikawa sasa hivi wananchi wanafaidika, basi irudishwe ile hadhi watu waweze tena kukopa na kukopeshwa kwa ajili ya zao hili la karafuu.

Mhe. Spika, nimeona katika hii sheria kwamba anatakiwa mchumaji wa karafuu, muanikaji na mzalishaji wa karafuu kabla ya kuchuma karafuu basi awe na vifaa hivi vinavyotakiwa na aoneshe kwa karani anayetakiwa, ili athibitishiwe kuwa ana majamvi, ana sehemu ya kuanikia. Jambo hili Mhe. Spika ni zuri sana, lakini mimi ningeomba kwamba asiombwe mwananchi kuwa athibitishe, bali serikali ihakikishe kama ni wakati wa kuzichuma karafuu hivi vifaa serikali ivitafute na ihakikishe kuwa inavyo ili kuwapatia wananchi kama kwa njia ya kuwakopesha, kama njia ya kuuziwa lakini serikali ivitafute hivi vifaa na wananchi wakavichukue vifaa hivi kwa serikali, sio kuwa mwananchi aoneshe yeye, yeye ataonesha wakati hali zetu kama tunavyozijua atavipata wapi, kama serikali haijawatafutia na ikawawekea wakaenda wananchi kukopa.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba serikali ina azma ya kukopesha pesa watu, basi hii ni azma nzuri sana, lakini serikali ijipange vizuri ikifika zao la karafuu, ili wale wazalishaji wa karafuu na wachumaji wa karafuu waweze kukopeshwa fedha kwa ajili ya kuihudumia hii karafuu.

Jambo jengine ambalo nataka kulizungumza Mhe. Spika, ni suala la bei ya karafuu. Mhe. Spika, magendo ya karafuu yalikuwa yanasababishwa na bei kuwa ndogo sana na kuwa wananchi wamekata tamaa ya zile karafuu kwa hali ya bei ambayo ilikuwa ni ndogo sana. Lakini sasa hivi wale wanaopeleka magendo ya karafuu, basi ni wale watu ambao mfano wameshapigwa muhuri tu wa laana, lakini kwa kweli karafuu sasa hivi wananchi wetu wameitikia wito wa kuuza karafuu kwa serikali yao, wanaziuza na wao wenyewe ni walinzi wa karafuu zao hizi ili zisiuzwe kwa magendo.

Kwa hivyo, ninachokiona hapa ni kwamba bei ikiwa nzuri basi mwananchi hauzi karafuu kwengine, pamoja na kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba kitaundwa kikosi kazi kwa ajili ya kulinda karafuu, lakini kikosi kazi kikubwa ni bei ya karafuu.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kama alivyosema huko nyuma, kwamba karafuu zikipanda bei duniani basi na wananchi watawapandishia bei ili wapate. Basi kama Mhe. Waziri atafanya hivyo, mimi

ninamuhakikishia kuwa huyo ndiye mlinzi mkuu wa karafuu zisiuzwe magendo.

Mhe. Spika, sisi sote ni mashahidi kama kipindi kilichopita karafuu serikali ilikuwa haizipati, karafuu zote zilikuwa zinakwenda Kenya, na watu wa Kenya walipewa zawadi duniani kwa kuuza karafuu, tizameni maajabu hayo. Watu wa Kenya walipewa zawadi kwa kuuza karafuu nyingi na bora zaidi duniani. Hivi Wakenya wana mikarafuu wameipata wapi, kwani hatujui karafuu zile na zawadi walizopata ni kwa karafuu zetu za hapa Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, baada ya kupandisha bei, sasa wapewa zawadi mwaka huu? Kwa sababu kama kuna watu wanaoziiba karafuu na kwenda huko basi ni chache mno, karafuu zote zimeuzwa serikalini. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakusihi sana kama hali ikiwa nzuri duniani basi wapandishie bei wananchi, na karafuu nakuhakikishia chembe moja haiendi Kenya na hawaipati tena zawadi ile waliyoipata kwa ajili ya karafuu zetu. Kwa sababu umejua kuzidhibiti karafuu, na ukidhibiti na ukizidhibiti kwa bei basi Mhe. Waziri karafuu zetu zote tutaziuza wenyewe.

Mhe. Spika, mfano mdogo tu, kipindi cha msimu huu tunaoingia tumeona kama karafuu hazipo ni ndogo ndogo, lakini karafuu zimejaliana kwa sababu hazipiti njia ya nyuma, ni chache mno wale waliokwishapigwa mihuri ndio wanaokwenda nazo Kenya kwa njia ya panya, tena hizo wananchi ni walinzi wote. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakusihi sana suala hilo ulione na *inshaallah* hali ikiwa nzuri basi na wananchi uwawekee vizuri.

Jengine Mhe. Spika, kuna huu mfuko. Na Mhe. Waziri umezungumza katika mfuko huu kwamba majukumu yake utawasimamia wananchi, na jengine nimeona kama watakuwa na Bima. Kwanza watafanyiwa usajili kutokana na hawa wachumaji wa karafuu na wakulima wa karafuu, halafu kutakuwa na mfuko maalumu ambao utaanzishwa na serikali, na mfuko huu jukumu lake moja nimeona amesema kuwa kutakuwa na bima, nafikiri bima hii ni kwa ajili ya watu wanaoanguka kwenye mikarafuu, aidha, wakaumia au wengine wakapoteza maisha yao ikiwa Mwenyezi Mungu keshataka muda wa kuwaita waja wake. Lakini sasa nauliza hii bima huyu atakaesimamia ni kwa yule mtu aliyeumia, maana saa nyengine inakuwa hasemi. Sasa huyo atakaekuwa msimamizi mkuu wa kusimamia akahakikisha kwamba bima yake imefunguliwa ni hawa watu wa mfuko au ni ndugu zake? Nilikuwa nataka ufafanuzi zaidi hapa Mhe. Waziri atakapokuja atufafanulie.

Je, kwa sababu watu wanapitana, kuna wengine wameumia viungo na kuna wengine wamepoteza maisha hizi bima zitakuwa za aina ngapi. Kwa hivyo hapa naomba ufafanuzi utakapokuja unifafanulie ili nipate nielewe.

Mhe. Spika, hii sheria ni nzuri kama walivyozungumza wenzangu lakini kuna mambo mengine ukiangalia inakuwa kama ni kikwazo kwa wananchi. Kwa mfano, hili suala la kuhamisha karafuu. Mimi jimbo langu la Micheweni hakuna mikarafuu kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor Juma. Jimbo langu ni Ukanda wa Mashariki ambao huwa ni ukanda kame. Kwa hivyo, karafuu nyingi nnvyokumbuka ilibidi kuanikwa Micheweni kwa sababu kule kunakuwa na jua saa 24. Kama walivyosema baadhi ya waheshimiwa kwamba karafuu zikipigwa na mvua zinafura na zinapoteza thamani yake. Kama ilikuwa upate *grade* ya kwanza basi unakuwa unapata mpeta tu. Sasa leo tunaambiwa hairuhusiwi kusafirisha karafuu kutoka sehemu moja kwenda kwengine. Kwa hivyo suala hili inabidi lizingatiwe upya.

Mhe. Spika, sisi nia yetu ni kupata karafuu zilizo na kiwango kizuri duniani ili tupate faida na tupate tujulikane kama karafuu zetu ni nzuri. Sio tupate karafuu zilizokuwa hazina kiwango kizuri.

Mhe. Spika, huu mswada kama nilivyozungumza ni nzuri na mimi nauunga mkono. Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na taadhima nataka nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia mswada huu. Kabla sijakwenda kwenye mswada wenyewe naomba ruhusa yako na naamini umeshanipa kwanza kabisa nitoe pole kwa chama cha CCM kwa kufiwa na Mbunge wa Jimbo la Chalinze. Tumuombee kwa Mwenyezi Mungu mwenzetu huyu alietangulia mbele ya haki amlaze mahali pema Peponi, amin.

Pia nitoe pole kwa Vijiji vya Shumbamjini na Maziwa Ng'ombe kwa maafa makubwa ya kuunguliwa na moto nyumba na mali zao. Ni mambo yanatokea lakini kibinaadamu ni watu wanaohitaji sana msaada. Naishauri serikali pamoja na juhudi zote ambazo wameanza kuzichukua wazidi kuwasaidia kwani wananchi hawa wamo katika madhila makubwa na ni masikini kama mnavyojua Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa Wilaya ya kwanza kwa umasikini. Kwa hivyo serikali itupie jicho wananchi hawa kwa sababu wengi wao hivi sasa wanahangaika kama ndege ambao hawana pa kutua.

Mhe. Spika, nasema haya kusisitiza serikali ifanye hivyo kwa sababu mwaka 2012 wananchi wa kijiji cha Kangagani walipatwa na maafa, ulitokea upepo mkali na dharuba kali, mapaa ya nyumba zaidi ya 20 yakachukuliwa yakatupwa zaidi ya maili moja kutoka yalipokuwa. Serikali ilienda kwa hamasa kubwa na wananchi walikuwa na imani kwamba watapata msaada, pamoja na ahadi zote zilizotolewa hadi hii leo hakuna aliyepita. Sasa haya ni

masikitiko na nashauri kabisa kwamba kwa vijiji vya Shumbamjini na Maziwang'ombe basi utaratibu uliotumika Kangagani usitumike huko. Vyenginevyo serikali itaonekana inakwenda mbio sana lakini wakishakutoa pole inakuwa basi. Hawa wanahitaji kusaidiwa.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye mswada wenyewe. Waziri wa wizara hii amesifiwa sana na kuna sababu za msingi za kusifiwa. Mtakumbuka kwamba zao la karafuu ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar, tangu enzi na jadi. Hivi karibuni utalii ulikuwa unasaidia. Lakini mtakumbuka kwamba kipindi cha kati pamoja na kwamba karafuu ni uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar, zao hili lilipewa mgongo, lilifumbiwa jicho na ikafika wakati mbungo ukawa ni bora kuliko mkarafuu. Baadhi ya wananchi wakaanza hata kuikata mikarafuu yenyewe kwa sababu haikuwa na thamani yoyote. Ni kipindi hiki cha serikali ya awamu ya saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa na chini ya Waziri wa Biashara, ndipo zao la karafuu lilipofumbua tena jicho.

Mhe. Spika, unaposema kwamba kuanzia sasa bei ya karafuu kwa mkulima itategemea bei ya soko la dunia ni mara ya kwanza kusikia sisi, kama vile soko la dunia limeanza juzi. Kumbe soko la dunia katika biashara mbali mbali na katika bidhaa mbali mbali liko miaka nenda miaka rudi. Kweli ahadi hii ikatekelezwa na karafuu ilipanda kutoka shilingi 3,500/- au 5,000/- mpaka shilingi 18,000/- na hapo tena kila mkulima akachacharika.

Mhe. Spika, suala la karafuu kwa kila aliye na karafuu ni sawa sawa na dhahabu. Zamani ilikuwa unaanika karafuu unakwenda zako shamba, unakwenda zako pwani huna habari ya karafuu, ikija mvua, likija jua, zikichukuliwa na upepo haya. Leo mtu anapoanika karafuu zake anakaa mwenyewe kwenye kiti analinda karafuu zile, akiondoka anamuweka mwanawe, kwa sababu ukiondoka kutokana na ile thamani ya karafuu mtu yeyote anaweza akakunja jamvi akatia guniani akenda zake akauza. Hii si neema ndogo na ndio maana tunatoa pongezi.

Si hilo tu karafuu sasa hivi kuna utaratibu mzuri wa kusarifiwa, ukipata ile *package* ndogo pale Air Port *departure*, huamini kwamba *package* ile ni karafuu za Zanzibar. *Grading* iliyofanywa na naamini kwamba wataalamu wa Wizara hii wanaendelea na juhudi za ubunifu kuhakikisha kwamba karafuu yetu inakuwa *number one* katika dunia.

Mhe. Spika, mswada huu ambao sasa hivi tunaujadili, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Tumejitahidi kuupitia mswada huu kama taarifa yetu ilivyosomwa na Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa

hivyo mimi naunga mkono mswada huu mia juu ya mia, lakini nina machache ya kuzungumza kama ifuatavyo;

Mhe. Spika, karafuu tangu asili na jadi ndio muokozi wa masikini ya Mungu. Ni kweli kabisa kwamba hapo zamani karafuu zikichumwa nyengine zikiuzwa na nyengine ilikuwa ni fimbo ya kipembe. Sasa kama nikiuza karafuu zangu zote leo, nikapata milioni 20, Mhe.Spika, fedha ukishakuwa nayo unaipangia matumizi tu. Sasa wazee wetu walipokuwa wakiuza karafuu na nyengine wanazibakisha ikawa ndio silaha yao ni kwamba zile karafuu kwanza huwezi kuzila. Kwa hivyo alikuwa mtu anauza pale ambapo ana haja ya kufanya hivyo.

Nakubali kabisa kwamba ni vizuri karafuu zote ziuzwe kwa serikali, lakini Mhe.Spika, hili limenung'unikiwa sana na wakulima na wachumaji wenyewe wa karafuu kwamba karafuu zako zote ukishazipata pale pale ukaziuze? Na wengine katika haya wamepewa shubiri wakachukua pima. Maana ukisema kwamba huruhusiwi kuhifadhi karafuu kavu ndani ya nyumba, maana yake ni kwamba hata zile za dawa ya tumbo ukikutwa nazo wewe ni kosa hilo.

Mimi nashauri kwamba pamoja na marekebisho yote yaliyofanywa basi uwepo utaratibu angalau mtu yeyote si lazima mmiliki au mchumaji kuwe na kiwango maalum akionekana nacho hicho asiwe na kosa. Kwa sababu mimi nikiwa na nusu kilo ya karafuu ukanambia kwamba wewe umehifadhi karafuu kavu ni mkosa na napaswa nikahukumiwe jela miaka mingapi au faini milioni tatu. Kwa kweli hili wakulima wetu hatutowatendea haki. Tusisahamu asili.

Si hilo tu Mheshimiwa karafuu ni dawa ya tumbo na pia ni chachandu, msio karafuu inasarifiwa *locally* na wenyewe wanasema kabisa wanachanganya na vitu vyao sijui vipi, Mhe. Bi Panya Abdalla anacheka. Masaji ya karafuu unaweza ukapata usingizi mpaka ukaamshwa, adhana inasomwa huna habari. Sasa hata hizo pia ukikutikana nazo waheshimiwa ni kosa? Kwa hivyo mimi nashauri katika hili kwamba ifike wakati kwamba angalau kiasi fulani kiruhusiwe kuwa nacho.

Jengine Mhe. Spika, kila msimu wa karafuu serikali inanunua karafuu, wauzaji wanapata pesa, lakini upande mwengine wa shilingi ni kwamba tunashuhudia vifo na vilema. Zanzibar si nchi pekee duniani wanaolima karafuu, kuna Brazil, Comoro, Indonesia na sasa hivi Kenya na sehemu nyenginezo. Mimi nilikuwa nampa changamoto tu Mhe. Waziri hivyo nchi nyengine ikifika wakati wa kuchuma zao la karafuu na wao wanakufa na kupata vilema kama sisi. Sasa kama si hivyo, basi waziri achukue

changamoto hii kwa kuwapeleka watu wake wakasome, ajue wao wana utaratibu gani ili angalau na sisi tupate afueni.

Mhe. Spika, jengine kuhusu karafuu,karafuu ina *grades.* Kule kwetu kuna *grades* kama mpeta kuna kamthiria, *grade two*, *grade one* na hizo zote zina bei zake. Wakati mmoja nilimsikia Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, akasema kwamba sasa hivi wanafanya utafiti ili wapate aina ya karafuu hizi tulizonazo ambayo kilo moja inaweza ikafika shilingi 50,000/-. Hii ni katika karafuu yenyewe, ichumwe vipi, ianikwe vipi, na ichumwe wakati gani. Naamini alikuwa hasemi vile kwa utashi tu. Kwa sababu kama kuna karafuu kamthiria hata mtu haitaki, kuna mpeta, hiyo ni *grade* ndogo na kuna mpaka *grade one*. Hapa si mwisho. Lazima usarifu mwengine na usanifu mwengine upo wa kupata zaidi ya *grade one* ya sasa ambayo kilo ni shilingi 12,000/- mpaka 14,000/-.

Ningemshauri Mhe. Waziri hili aliharakishe kwa sababu kama karafuu itafika mahali kilo ni shilingi 50,000/- mazanzibari aliye na mkarafuu na asiye na mkarafuu, maana neema ikiingia kama mvua haichagui, tutaneemeka sana.

Mhe. Spika, sheria hii inatungwa, lakini katika suala la karafuu na sio karafuu peke yake ni vizuri waungwana sisi tusitunge sheria ambayo sehemu nyengine inakirihisha. Kuna kifungu cha 13(1) naomba nikinukuu.

Kifungu cha 13(1) "Inakatazwa mtu yeyote kufanya jambo lolote kati yafuatavyo kwenye mashamba ya mikarafuu:-

(a) kuchoma au kutengeneza makaa,
(b) kuchimba mawe, udongo au mchanga,
(c) kuangusha, kung'oa, kukata, kuharibu, au kuathiri mkarafuu; na
(d) kufanya shughuli nyengine yoyote ambayo imekatazwa na iliyotungwa kwa mujibu wa sheria hiyo."

Mhe. Spika, hapa mimi nazungumzia kukata. Mheshimiwa mikarafuu ni miti sawa na minazi. Kwa sheria na kifungu hiki mikarafuu inang'oka kwa upepo tu na mikarafuu inakufa. Hapa ulikuja mradi wa utibabu wa mikarafuu *daybeath* na *suddandeath*, mkarafuu umeshakufa, umeshakauka, tuufanyeje? Huko ndio mpaka upate ruhusa ya Waziri. Sasa nazungumzia mkarafuu umenyauka kabisa kwa dharura, uko kwenye barabara gari hazipiti, bado ni mkarafuu. Ukichukua shoka ukiukata ili gari zipite kwa sheria hii ni kosa. Itafutwe lugha hapa ili kukata mkarafuu wa namna hiyo ninayoisema isiwe ni kosa.

Mkarafuu umeanguka juu ya nyumba ya mtu. Maana nyumba za wakulima wa mikarafuu nyingi zipo kwenye mikarafuu, itabidi ukate na ung'oe na hili ni kosa, au ukamtafute waziri, wakati huo watoto wamo ndani ya nyumba, hapo waziri utampata saa ngapi. Kwa ufupi nakusudia katika hili itafutwe lugha nzuri ili matendo kama haya isiwe ni kosa.

Mhe. Spika, kifungu cha 19(2) wenzangu wamesema sana katika kifungu hiki. Maana yake ni kwamba kifungu hiki kinahitaji kifanyiwe marekebisho.

"Kifungu cha 19(2) "Kifungu kidogo cha 1 cha kifungu hiki, hakitotumika kwa wachumaji wa karafuu ambao watakuwa katika majukumu yao ya kawaida, kurejea majumbani mwao kutoka katika sehemu za uchumaji wa karafuu."

Jana Mheshimiwa Mwakilishi wa jimbo la Konde alisema hapa kwamba kuna sheria, sasa sijui, maana jana nilikuwa naiangalia sheria tuliyoifuta. Mtu unapomuona na karafuu, Mhe. Spika, wewe Pemba umekaa na hukukaa siku tatu. Kipindi ulichokaa Pemba misimu ya kuchuma karafuu ulikumbana nayo, ingawa ulikuwa huchumi. Lakini kwa kwa kawaida yetu sisi kuna watu wanakodi mikarafuu, wanahama na watoto wao wanakwenda kuhamia kama mwezi, miezi miwili, mitatu. Mimi nakaa Kangagani lakini nina mkarafuu wangu mmoja tu Kirimdombo ni meli nne tu kutoka pale ninapokaa. Sasa mimi siwezi nikahama na wanangu kwenda kule Kirimdomo kuchuma ule mkarafuu mmoja, ninachofanya tunasema kuna karafuu za mbio, unatoka asubuhi unakwenda kuchuma, unapata kipeto chako kama pishi tano au sita unajitwika. Sasa Kangagani ni Shehia moja, napita shehia tatu ili nifike Kirimdombo. Nikishakuchuma karafuu zangu Kirimdombo nakuja zangu Kangagani, sheria inanambia hapana. Eti nikae pale, nichambue, nianike, zikauke, ingekuwa suala hilo ni kufumba na kufumbua sawa. Lakini kuchambua polo la karafuu kama ni peke yako ni masaa mawili, kuzianika ni masiku.

Kwa hivyo nasema wachumaji wa karafuu wanaotoka mahali pamoja kwenda pengine, karafuu za mbio kusiwe na vipingamizi vinavyokithiri na vikikithiri hizo karafuu nyengine hazitochumwa na kama hazichumwi atakaekosa karafuu ni wewe mwenye mkarafuu lakini na serikali vile vile itakosa. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba kifungu hiki kiongezwe, maneo wakiwa wamechukua karafuu au makonyo.

Kifungu cha 19(4) "Inakatazwa mtu yeyote, isipokuwa Shirika kuhifadhi karafuu kavu ndani ya nyumba, ghala au sehemu nyengine yoyote"

Hapa watu mtawamaliza kwa kuwafunga. Maswali yangu ni haya yafuatayo sisi hapa tuna taasisi, tuna NGO's na kuna jumuia za kukodi mikarafuu si shirika hilo kwa mujibu wa tafsiri ya sheria hii. Shirika ni ZSTC. Je, na hawa na wao kuhifadhi, maana kuhifadhi humu haukuwekwa muda wala kiwango. Lakini tafsiri ya kuhifadhi ni kuweka kitu katika hali ya usalama ili kisiharibike. Sasa ndio yale yale niliyoyasema mwanzo. Ukisema karafuu kavu, hata moja ni karafuu kavu, maana yake wingi wa karafuu ni karafuu, ikiwa moja ni karafuu, likiwa gunia ni karafuu.

Kwa hivyo hapa nashauri kabisa kwamba pafanywe marekebisho ya kifungu hiki ili tuwe na kiwango ambacho ukikutwa nacho iwe si kosa. Lakini vile vile na mda wenyewe wa kukutwa nacho. Karafuu zamani na mpaka leo tusione siku hizi inatokea barka lakini imeshatokea Pemba miaka mitatu karafuu haijaonekana mkarafuuni, kabisa. Tusione leo kwamba kila mwaka kuna mizao ya vuli na mwaka. Na kama imeshatokea maana yake inaweza ikatokea tena, haikuwa mwisho.

Kwa hivyo kifungu hiki nashauri kabisa kwamba isiwe shirika pekeyake itanuliwe zaidi ili ionekane kabisa kwamba hata kama kuna taasisi nyengine. Na kuna taasisi za serikali kabisa ambazo hizo huna shaka nazo kwamba zinakwenda kufanya magendo. Sasa sheria nafikiri ingefafanuliwa zaidi ili kuipa nafasi sheria hii isiwe kwamba ni kikwazo. Maana sisi hapa tuko kutunga sheria zinazotekelezeka. Sheria yoyote ambayo haitekelezeki hiyo sheria isitungwe.

Mhe. Spika, mimi kwa heshima na taadhima nifikie hapa na kama nilivyosema kwa niaba yangu na wananchi wa jimbo la Ole tena wote naunga mkono mswada huu.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kabla ya kuanza nianze kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia uhai tukakutana hapa asubuhi hii lakini pia nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe ambaye na mimi umenipatia nafasi hii niweze kutoa mchango wangu japo mdogo katika mswada huu. Lakini kabla sijaanza kuchangia napenda pia nitoe pongezi ya pekee kwako Mhe. Spika, kwa utaratibu mzuri ambao umetuonesha katika kipindi hiki cha huu mkutano wetu. Kwanza kufanya marekebisho ya saa na ukaleta saa nzuri zenye kiwango, lakini pili nimeona jambo jengine tumepata *diary* Wawakilishi wote. Ni kitu cha kushukuriwa na kupongezwa sana.

Mhe. pia nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu mzuri ambao una manufaa kwa wananchi wa Zanzibar na Taifa kwa jumla. Mhe. pia nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Mwenyekiti

wa Kamati hii kwa jitihada kubwa ya kuupitia mswada huu na akaufanyia marekebisho mengi yakapelekea kutoa mswada mwengine mpya ambao umewarahisishia wajumbe kuweza kuchangia vizuri. Mheshimiwa hilo naomba nitoe pongezi zangu.

Pongezi nyengine za dhati kabisa napenda nitoe kwa Rais Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein ambaye pia aliyeongeza bei ya karafuu na leo tukaweza kuwa na sababu ya kuleta miswada ambayo inaweza kuboresha zaidi maslahi ya wazanzibari. Mheshimiwa, mengi wameshayasema wenzangu lakini na mimi nikasema kwa uzuri wa huu mswada basi na mimi niseme angalau machache ili kutia barka katika mswada huu.

Mhe. Spika, nataka nianze mchango wangu katika kifungu cha 5 (j) ambacho kinaelezea kusaidia huduma za matibabu na huduma nyengine za Bima kwa wakulima na watu watakopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu. Mhe. Spika, hili napenda nilipongeze kwa dhati kwa sababu sote ni mashahidi tuliona uchumaji wa karafuu siku za nyuma ulivyokuwa jinsi ya watu walivyokuwa wakianguka na kupoteza maisha au kupata vilema. Lakini kupata msaada ilikuwa ni ngumu sana. Lakini leo mswada huu umeanza kutupa imani kwamba sasa kweli zao la karafuu tumeweza kulipa thamani kwa kuwajali kwanza wachumaji wenyewe.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika ukurasa 371 kwenye kifungu cha 11 ambacho kifungu kidogo cha (a) kinaeleza kuidhinisha aina tofauti za karafuu zitakazopandwa Zanzibar. Hili mimi kwanza nilikuwa nataka nijue tuna aina ngapi za karafuu hapa Zanzibar. Lakini pia kifungu cha (b) kinasema kuanzisha, kulinda na kuendeleza vitalu vya mikarafuu. Hili pia naomba nilisisitize kwa sababu kwa muda huu tuna uhaba wa vitalu vya mikarafuu hali ambayo inapelekea wananchi wenye mashamba wanapotaka kupanda mikarafuu wakati wa msimu wa mvua basi wengi wanakosa miche.

Jengine kifungu (c) kinasema kulinda mkulima na kutibu na kusafisha mashamba ya karafuu. Na hili nalo napenda nililisitize kwa sababu elimu hii bado inahitajika sana kwa wananchi wetu kwa sababu bado wapo ambao wanabeza kuyasafisha mashamba ya karafuu.

Niende katika ukurasa wa 372 katika kifungu cha 3(a) ambacho kinasema idadi ya wakulima walioomba na walio na sifa za kupewa vivutio kutoka kwenye mfuko. Mheshimiwa hapa mimi nilikuwa nataka kujua kwanza ni sifa gani labda mtu anatakiwa awe nazo ili aweze kupata hivyo vivutio. Baada ya kuzijua mimi pia nilitaka elimu hii iweze kutolewa kwa wananchi ili waweze sasa kujiandaa baada ya kujua kumbe unatakiwa uwe na sifa gani

na sifa gani ndipo uweze kupewa hivyo vivutio ili wananchi wetu waweze kujiandaa waje kufaidika na huo mfuko.

Mheshimiwa nikienda katika ukurasa wa 373 ambapo kifungu cha 13(1) hiki ambacho Mhe. Hamad hapa amekisema hivi punde. Mimi nilitaka tu kueleza pamoja na yale ambayo yeye ameyasema ni kweli mengine yataleta utata kama yakiwa hayajapatiwa ufumbuzi, lakini kwa yale ambayo yapo katika ufumbuzi mzuri, mkarafuu hauna tatizo haujapata athari yoyote, kuukata na kuuchoma tu makaa na kufanya vyenginevyo, hili mimi nataka litolewe elimu, tena iwe ya makemeo kwa sababu watu wanakuwa wanaihujumu tu mikarafuu ovyo ovyo na sasa tayari hili zao limekuwa la manufaa makubwa kwetu.

Mhe. Spika, nikenda katika ukurasa wa 374, kifungu cha 18(3) ambacho kinaeleza kila mkulima mmiliki au mkodishwaji wa mikarafuu ambaye atakusudia kuchuma na kuanika karafuu wakati wa msimu wa uchumaji karafuu anatakiwa awe na vifaa vifuatavyo vilivyothibitishwa na mamlaka husika.

Mheshimiwa kifungu hiki mimi hapa nilikuwa napendekeza pia ingeundwa kamati, kamati ambayo ingeweza kushughulikia zoezi zima hili la uchumaji na uanikaji wa karafuu. Pamoja na vifaa ambavyo tumevitaja lakini ukaidi wa binaadamu wetu tunauelewa. Tungekuwa na kamati ambayo itawapitia wachumaji wa karafuu; kwanza ingeweza kuwadhibiti pale wanapokuwa wanavunja vunja tu mikarafuu kiholela. Kwa sababu uchumaji wa karafuu pia nao una mbinu zake, vyenginevyo mkarafuu unachumwa unanyonyolewa wote matokeo yake hata msimu mwengine unashindwa kutoa mazao vizuri.

Kwa hivyo ingeundwa hii kamati ambapo ikawa inawapitia watu wakati wa uchumaji basi hata huo uanikaji wangeweza kuona tunakwenda sambamba hali ambayo vile vifaa vilitakiwa vitumike basi vingeweza kutumika ili tukaweza kupata kitu kilicho katika hali nzuri.

Mheshimiwa nikenda katika ukurasa wa 375 kwenye kifungu cha 20(2)(a) ambacho hapa ndio kutakuwa na kusimamia fedha zilizotengwa kwa ajili ya wakulima wa karafuu. Mheshimiwa hapa mimi nilikuwa nataka nisisitize, tukiwa na huo mfuko basi tuweze kuzitoa hivi fedha; tuwe na mfumo mzuri ambao utaweza kuondosha malalamiko kwa wakulima wetu.

Pia nisisitize katika kutolewa fedha hizi pia kunatakiwa marejesho, kwa hivyo kuwe na usimamizi mzuri wa ufuatiliaji ili fedha hizi ziweze kurejeshwa kwa wakati ili mfuko huu uweze kuendelea vizuri kwa kuwasaidia wakulima wetu wa karafuu.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa 376 hapa nilikuwa nina tatizo dogo na nadhani labda ni *typing error* katika kifungu cha 24(4) ambacho mstari wa mwisho wa chini kinasema, 'madhumuni ya urahisi wa kuratibu na kuiainisha, sasa hapa hili neno sijui kama limekosewa au ni mimi sijalifahamu maana yake, basi ningeomba labda kama limekosewa basi liwekwe vizuri na kama labda mimi tu sijalifahamu maana yake basi utakapokuja uweze kunifahamisha.

Mhe. Spika, kwa kweli wenzangu wamesema mengi na huu mswada kwa kweli tunaupongeza ni mzuri nami tu nilisema angalau niweze kusema maneno mawili ili kutia barka katika mswada huu ambao unaonekana utakuwa na manufaa makubwa kwetu na wananchi wetu na taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na nautakia kila la khheri ili tuweze kuendelea vizuri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi ninashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa sheria ya kufuta sheria ya karafuu nambari 11 ya mwaka 1985 na kuweka sheria mpya ya maendeleo ya karafuu na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza kabla kuanza kuchangia mswada huu naomba ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambahyo mimi mwenyewe sijayaelewa viziri kama ifuatavyo:-

Tukianzia na ukurasa 268 kifungu cha 2 kinachohusiana na matumizi ya sheria kinasomeka kama ifuatavyo; kwa ruhusa yako Mhe. Spika, 'sheria hii itatumika katika uzalishaji na maendeleo ya karafuu isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo. Sasa hii kama itaelezwa vyenginevyo ningeomba nipate maelezo, kwa nini kuwe na ziada ya maneno haya.

Ya pili katika tafsiri, kifungu cha 3 kuna neno limeandikwa 'karafuu' ambalo maana yake ni mauwa ya karafuu ikiwa yamekua au vyenginevyo yaani yakiwa mabichi. Matende ya karafuu au makonyo ya karafuu na mazao yaani bidhaa zinazohusiana nazo, zote hizo huwa ni karafuu. Lakini Mhe. Spika, ukiangalia katika vitabu kwenye mitandao vinavyotoa tafsiri ya karafuu zinasema kuwa karafuu maana yake nakuja kwa jina la kisayansi, kwanza inaitwa huu mkarafuu binafsi unaitwa *Syzygium aromaticum*, hilo ndio jina la kisayansi na halafu hili neno *clove* ni neno la kilatini ambalo maana yake ni *nail* na baadhi ya watu wanatumia karafuu kuwa ni msumari.

Sasa karafuu hii wanasema kuwa ni maua ambayo hayajafumbua yaliyoanikwa yaani wanasema *cloves is dried bud*, nimesahau Mheshimiwa

nitakumbuka baadae. Lakini ni ua ambalo halijachanua hii karafuu na iliyokuwa inaanikwa. Sasa tukisema matende, matende Mheshimiwa si karafuu kwa maana ya ma-*dictionary* yale ni matunda ya karafuu. Makonyo ni vijisehemu vinavyoota hizo karafuu zenyewe, kwa hivyo tujuwe karafuu kwa mujibu wa vitabu ni matunda ambayo hayajafumua, yanayoanikwa, yanayotokana na mkarafuu unaoitwa *Syzygium aromaticum tree.* Sasa ikiwa sivyo nilivyoeleza mimi naomba maelezo zaidi.

Halafu Mhe. Spika, mkarafuu kasema maana yake ni mti unaozaa karafuu unajumuisha majani, magogo, matawi na mizizi. Mheshimiwa, ukisema mti maana yake hayo majani, magogo, matawi yameshaingia ndio ukaitwa mti kwa nini hatusemi tu kama mkarafuu ni mti unaozalisha karafuu au unaozaa karafuu na hiyo naomba maelezo.

Mhe. Spika, tukiendelea ukurasa wa 370 kifungu cha 7(1) kinaeleza kitaanzishwa kikosi kazi chini ya Waziri chenye jukumu la kuzuia magendo ya karafuu na vitendo vyengine vinavyoathiri biashara ya karafuu. Sasa Mheshimiwa sisi tunacho Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, kinafanya kazi zake kwa ufanisi kina vyombo na kadhalika. Hivyo kutafuta Kikosi Maalum tukatumia pesa nyingi sana kwa watu ambao hawana utaalamu wa kuzuia magendo huko baharini si kupoteza pesa za serikali bure? Kwa nini Mhe. Waziri haoni kuwa iko haja ya kuimarisha hiki kikosi chetu cha KMKM kikafanya kazi kwa ufanisi ili karafuu zetu zisiuzwe kimagendo. Vile vile kwa nini haangalii kulikuwa na sababu gani ya karafuu zetu kusafirishwa magendo ili sababu hizo zikapigwa vita na magendo ya karafuu yasiendelee tena hasa kwa vile Mhe. Waziri kachukua kazi kubwa sana, nzuri na ya mfano hii ya kupandisha karafuu bei katika hali ambayo wananchi wote wameridhika.

Halafu tukienda katika kifungu cha 11 ukurasa wa 571 hiki kinahusiana na mfuko ambao mfuko huo unasema utasaidia mamlaka inayohusika kwa (a) kuidhinisha aina tofauti za karafuu zitakazopandwa, hapa naomba nipewe maelezo. Sisi tuna karafuu zetu, Mwenyezi Mungu kazijaalia karafuu hizi ni nzuri ninasikia katika ulimwengu mzima ni za aina yake, karafuu hizi haziharibiwi na wanyama, haziliwi na wadudu kama inatokezea hivyo ingelikuwa kazi kubwa ya kulinda, sasa tukisema tunataka kuleta aina tofauti, maana yake tofauti ya hizi tulizonazo aina hiyo ni ile inayotoka Madagascar, Indonesia, Malasia, Sirilanka au vipi naomba maelezo au ni kutokana na hizi *species* zetu tulizonazo tunatafuta mbegu bora zaidi iliyokuwa ina makonyo mafupi, karafuu nyingi na inazaa karafuu kwa wingi zaidi. Naomba hapa nipate maelezo.

Halafu kifungu cha (c) kimeeleza kulinda, kulima na kutibu au kusafisha mashamba ya karafuu na naongeza cha (d) kinasema kuwa kuchunguza sababu, tukio, kinga, kudhibiti, au kukodisha, au kuondosha maradhi yoyote ambayo yanaelekea kuhatarisha maslahi ya zao la karafuu na kuendelea.

Sasa Mhe. Spika, mikarafuu iko hapa miaka mingi sana ukweli tunaujua na karafuu zilikuwa ndio zao letu kubwa sana hapa linalokuza uchumi katika nchi hii. Na ilitokea awamu hapa mikarafuu ikatibiwa, lakini baada ya kutibiwa ikafa mingi sana. Mimi namuuliza Mhe. Waziri, hivyo mpaka leo hatujawa na wataalamu waliokuwa wanajua kuwa hii mikarafuu inapata maradhi vipi na iko haja ya kuwa tayari tuna matibabu yake hata akaandika kulinda, kutumia na kutibu na kusafisha mashamba ya karafuu na kadhalika, kuchunguza sababu yaani ndio tunaanza leo, hatujui kuwa ni viumbe hivi naomba maelezo.

Halafu tukija kifungu cha 13 ukurasa wa 573 kifungu kidogo cha pili kinasema hivi, 'ni marufuku kutumia mkarafuu kwa ujenzi wa aina yoyote, mbao, kuchonga vinyago au mapambo. Mhe. mikarafuu inazeeka na inakufa tujaalie mkarafuu unakufa wangu mwenyewe wa kurithi au wa kununua unakufa na hauzai tena na ninataka kuusarifu, hivyo nikiambiwa ni marufuku kutumia mkarafuu kwa ujenzi wa aina yoyote mbao, kuchonga vinyago na mapambo, mkarafuu unaokufa ulikusudiwa nini kwa Mhe. Waziri mpaka akauwekea vikwazo vyote hivyo.

Na halafu ukaendelea mtu yoyote ambaye anakusudia kukata mkarafuu kwa madhumuni ya shughuli za maendeleo atatakiwa kuomba kibali kwa Mhe. Waziri, Mhe. Waziri anakaa Unguja, mimi nina wananchi huku Unguja hawakujui wachilia kumjua Mhe. Waziri mwenyewe, mikarafuu iko mwituni huko imekufa na kadhalika hivyo mkulima huyu na mkarafuu ule ni wake afanye fanye vipi mpaka aonane na Mhe. Waziri huyo ambaye yuko Unguja huku. Naomba maelezo.

Halafu mtu yoyote ambaye atakwenda kinyume na kijifungu hiki atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atapaswa kulipa faini isiopungua shilingi za kitanzania milioni tatu. Wengine wanachuma karafuu mpaka wakimaliza wakishalipa vibarua hizo milioni hawajaziona. Je leo kwa kukata mkarafuu mkavu, naomba kifungu hiki kipitiwe na nipewe maelezo ambayo yataniridhisha Mheshimiwa.

Chengine ni ukurasa wa 374 na ni kifungu cha 18 (1) hapa kaeleza kutakuwa na msimu wa zao la mwaka na msimu wa zao la vuli la karafuu, kama ni misimu ya uchumaji wa karafuu ya kila mwaka. Mimi naona hata ingelikuwa hakuna hizi karafuu tunao msimu wa mwaka na tunao msimu wa vuli. Na

kwa sababu karafuu zinaingia katika misimu hii, hii misimu iko tokea zamani. Kwa hivyo tukisema kutakuwa maana yake ni kitu hakipo kwa hivyo naomba kama kutakuwa kuna uwezekano wa kubadilisha lugha ibadilishwe kwa sababu hii misimu ipo zamani.

Halafu kifungu cha 3 katika kifungu hicho cha 18 kinaeleza ambacho kimefanana na kifungu cha pili ambacho nimekifuta kimeeleza kuwa kila mkulima, mmiliki au mkodishwaji wa mikarafuu ambaye atakusudia kuchuma na kuanika karafuu wakati wa msimu wa uchumaji wa karafuu atatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo, yaani vilivyothibitishwa na mamlaka husika. Vifaa vyenyewe ni vifaa vya kuhifadhia karafuu, vifaa vya kuanikia karafuu, vifaa vya upimaji na mahitaji mengine yoyote ambayo mfuko itayaona inafaa kwa kuidhinishwa na mamlaka husika.

Mhe. Spika, uchumaji wa karafuu wengine maskini na ikitokea zao la karafuu ndio anapofaidika. Watu wanahifadhi karafuu zao katika vipolo wakati ZSTC ndio yenye magunia, watu hawana pesa za kununua majamvi ya kuanikia karfuu na karafuu tusipozianika kwenye majamvi hupati ile *grade one* hata jua likawa kali vipi. Vifaa vya upimaji hapa ni pishi pamoja na minzani si rahisi mkulima kuweza kumiliki vitu hivi, nauliza sheria hii iliwekwa kwa kukusudia nini, Wizara itahakikisha kuwa hao wachumaji wa karafuu itawasaidia kupatikana kwa vifaa hivyo. Naomba maelezo.

Halafu kifungu kidogo cha nne katika kifungu kile kile cha 16 kinasema kila mkulima, mmiliki au mkodishwaji wa karafuu atahakikisha kwamba karafuu zake ziko katika hali nzuri na hazijaharibika au kuchanganyika na vitu vyengine wakati wa uchumaji, uanikaji na uuzaji. Mimi kuchanganyika na vitu vyengine sina matatizo nayo kwa sababu kweli karafuu ni lazima ziwe nzuri, tunajua kuna watu wanazighushi karafuu sana kwa kuchanganya na makonyo mengi, hili si jambo zuri.

Lakini hivi kuwa katika hali nzuri na hazijahrika, tunajua Mhe. Spika, wachilia mbali sasa kwa sababu kuna tabia hii ya nchi, lakini karafuu zinazovunwa wakati wa vuli kunakuwa na mvua nyingi sana. Mtu anaweza akaanika karafuu zake katika hali nzuri asubuhi jua linatoka akenda kuchuma karafuu huko lakini huku ikanyesha mvua nyingi na karafuu zikiroa zinaharibika. Karafuu usipozianika kwa sababu ya mvua nyingi humo ndani unamoziweka vile vile zitapata joto na kuharibika ile *grade* inayotakiwa haitakuwa nzuri na karafuu hazitakuwa nzuri.

Sasa Mhe. Waziri akisema karafuu lazima ziwe katika hali nzuri na hazijaharibika kakusudia nini kwa hili au atakuwa na mpango wa kufanya viwanda maalum vya kukausha karafuu ili watu wapeleke huko. Naomba

maelezo. Hii kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine imeshazungumzwa.

Sasa Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati, naomba kumalizia kwa mambo yafuatayo:-

Mhe. Spika, tunapozungumza karafuu tujuwe hii ni raslimali aliyotujaalia Mwenyezi Mungu ambayo ina umuhimu sana kwetu na vile vile dunia nzima. Mhe. Spika, karafuu inatumika katika hali nyingi tofauti. Kwa mfano karafuu inatumika kwa kuondoa matatizo kwa watu wanaoumwa na meno, ukitia mafuta ya karafuu yale maumivu yanapungua au ukitafuna karafuu maumivu vile vile yanapungua.

Mhe. Spika, vile vile karafuu ikiwa ni unga au karafuu yenyewe inatumika katika mapishi ya aina kadhaa, wenzetu huko wanatumia japo kuwa sisi hatutumii. Karafuu vile vile inatumika katika mambo kadhaa mfano kuondoa maumivu ya sehemu kadhaa. Na kwa sababu hiyo hutokea kila baadhi ya kipindi watu wakasaidiana kwa sababu ya karafuu unakuwa madhubuti kabisa.

Mhe. karafuu inafanywa chai kwa wale wanaosafiri wanaojihisi kama unataka kutapika, wakinywa hali inarudi katika hali ya kawaida. Karafuu inasaidia vile vile tena sana tu wale watu waliokuwa wanasafiri kwenye anga huko.

Karafuu inatumika kwa kuua *intestinal parasite*, karafuu inatumika wa *uterine consumption* kwa hivyo ndio mama wajawazito wakaambiwa wasitumie sana karafuu. Kule Indonesia karafuu inatumika hata katika mambo ya kimila, wapo baadhi ya makabila mtu akizaa mtoto mwanamme siku ile ile anaotesha mkarafuu, na ana imani kadri mkarafuu unavyonawiri ndio na mtoto wake atakavyokua.

Karafuu imetumika China tokea miaka 2000 iliyopita kwa madawa kadhaa, Mwenyezi Mungu katujaalia tumepata karafuu katika nchi hii. Mimi ninaloomba Mhe. Waziri ni kufanya kila inavyowezekana mikarafuu ikaimarishwa, ikalimwa, ikaoteshwa katika sehemu tofauti za nchi yetu. Tumesema tuwe na wataalmu, waangalie *soil analysis* ilivyo kule mikarafuu inakoota na sehemu nyengine ienezwe isiachiwe sehemu zile zile tu ili pato la nchi liweze kuongezeka.

Na la mwisho ninalozungumza Mhe. Spika, ni kuwa mkulima anapochuma karafuu zake anakwenda kuziuza katika vituo vya ZSTC. Lakini zilioko minzani nyingi, zinazotumiwa hadi leo ni kongwe na kwa hivyo,

hawajazikagua watu wa *ZSTC,* lakini wakulima kwa bahati mbaya wanakoseshwa haki yao halisi.

Hata katika msimu uliopita kwenye jimbo langu kuna watu walikataa kuuza karafuu zao katika vituo fulani na wakazipeleka Wete, kule Wete kilo ziliongezeka na fedha ikaongezeka. Wito wangu kwa Mhe. Waziri, ni kuwa Mwenyezi Mungu anasema adhabu kubwa itawafikia wale wanaowapunja wenzao. Naomba minzani aitilie mkazo sana, aone kuwa watu wetu wanapopeleka karafuu zao kuuza kule *ZSTC,* basi wanapata haki kutokana na karafuu zao zilivyo.

La mwisho Mhe. Spika, karafuu ni uchumaji wa hatari tena hatari sana, kuna watu walikuwa wakianguka zamani na nashukuru walikuwa wakishughulikiwa na wakilipwa, lakini kuna kundi liliachwa njiani mpaka leo hawakupata haki yao na mikarafuu ya kwetu ni tofauti na nchi nyengine, ni mikarafuu mirefu sana. Namuomba Mhe. Waziri, ule mpango aurudishe ili ikitokea bahati mbaya mchumaji wa karafuu kupata ajali, basi ashughulikiwe angalau kupata fidia yoyote.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba kukaa kitako.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu muhimu. Kwa kweli mimi sitokuwa na mengi kwa sababu karibu vifungu vyote vishachangiwa, lakini kwa vile nilikuwa tayari nimeshaleta jina langu itabidi nichangie kidogo. Kwa hivyo, naomba uniruhusu nianze na madhumuni na sababu.

Katika ukurasa wa 378 chini kabisa Mhe. Spika, kuna kifungu ambacho kinasema kuwa rasimu ya mswada huu imezingatia mambo bora yanayofanywa duniani na imezingatia miswada ya sheria kukuza mazao katika nchi za Afrika Mashariki, kama uendelezaji wa mazao ya kahawa na mengine yametajwa hapa. Sasa ikiwa kweli madhumuni ya mswada huu ni kuliendeleza zao la karafuu kama vile wenzetu walivyoendeleza mazao yao, basi mimi mswada huu nauunga mkono mia juu ya mia, kwa kweli ni jambo zuri.

Lakini Mhe. Spika, naomba nimkumbushe Mhe. Waziri, kama uwasilishaji wa mswada na upitishaji wa sheria ni jambo moja na utekelezaji wa sheria ni jambo jengine. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, mara baada ya kupitishwa sheria hii utekelezaji wake ufanyike mara moja ili suala la kuendeleza zao la karafuu lianze hatua kwa hatua.

Mhe. Spika, hali ya mashamba ya mikarafuu ni mbaya sana, mashamba hayahudumiwi, mikarafuu haipaliliwi na hatimaye inakufa. Kwa kweli kufa kwa mikarafuu hii kumesababisha zao la karafuu kupungua kuliko siku za nyuma. Mhe. Spika, mimi binafsi nilikuwa najiuliza je, sababu zilizosababisha mashamba ya mikarafuu yasiendelezwe na hivyo mikarafuu mingi kukauka zimerekebishwa vipi kwenye mswada huu?

Katika ukurasa wa 369 kifungu cha 4, kinaeleza kuanzisha Mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Maendeleo na Mfuko huu utasimamiwa na Mfuko wa Shirika la *ZSTC*. Sasa Mhe. Spika, sheria ya kuanzisha *ZSTC* tulipitisha hapa Barazani mwaka juzi tu, sheria hii ni mpya. Suala langu ikiwa tunaanzisha Mfuko utakaosimamiwa na *ZSTC,* kwa nini mswada huu usiwe ni sehemu ya sheria iliyoanzisha Shirika la *ZSTC*. Hapa Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, anipe ufafanuzi.

Pili, Mhe. Spika, nimefurahi sana na kazi za Mfuko wa Maendeleo na kazi moja iliyopangwa ni ile ya kifungu cha 5(j) ukurasa wa 370, kinachozungumzia kuhusu kusaidia huduma za matibabu na huduma nyengine za bima kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu.

Mhe. Spika, hilo ni jambo zuri na ni muhimu sana. Kwa sababu hivi sasa wananchi wanaopata ajali ya kuanguka mikarafuu hawapati huduma vizuri, wala yale malipo waliyokuwa wakipewa zamani hawapewi. Mhe. Spika, katika kila kijiji cha Pemba si rahisi kukaa usimkute mlemavu aliyesababishwa na ajali ya kuanguka mkarafuu. Baya zaidi hakuna anayewajali wala kuwasaidia. Ushauri wangu Mhe. Spika, mswada huu utafute suluhu ya tatizo hili na liondoke ukishapita mswada huu.

Vile vile, katika ukurasa huo huo wa 370 kifungu cha 5(i) na (j), namuomba Mhe. Waziri, anifahamishe kidogo kwa sababu naona sijafahamu. Kifungu cha 5(i) kuwepo daftari la usajili wa wakulima, wamiliki, wakodishwaji na wadau wengine wanaojishughulisha na shughuli za uzalishaji karafuu kwa madhumuni ya kurahisisha shughuli za ulimaji wa karafuu, huduma za kifedha, bima na shughuli nyenginezo zinazohusiana na karafuu. Lakini hiki kifungu kinachofuata kimesema;

> “kusaidia huduma za matibabu na huduma nyengine za bima kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu”

Mhe. Spika, mimi sijafahamu jambo moja hapa, kwa sababu najua hupewi bima kama hujajiunga na bima, kuna bima ya afya, bima ya magari, kuna

bima ya mambo chungunzima. Lakini sasa hapa hawa wakulima na mashamba yao watajulikana na watasajiliwa, wakodishwaji wale wanaokodi yale mashamba pengine mara hii wamekodi, mara nyengine hawakukodi. Halafu kuna wale wachumaji ambao kwa kwetu tunawaita vibarua, wale pengine leo kachuma kisha hachumi tena mpaka mwaka ujao anakuja kuchuma siku moja. Sasa sijui huu usajili utafanywa vipi. Kwa sababu ikiwa mfano mtu kenda kuchuma leo na ile ile leo aliyochuma imetokea bahati mbaya kaanguka sasa mtu huyu kasajiliwa saa ngapi? Au hii bima ataipata vipi?

Hapa kidogo nimuombe Mhe. Waziri, anifahamishe ili na mimi nikifahamu kifungu hiki. Kwa sababu mimi naelewa kuwa hata upatwe na tatizo gani ikiwa hujajiunga na bima huwezi ukapewa bima. Sasa hapa kuna mtu aliyekwenda kuchuma karafuu leo na hiki kifungu kimeweka kwamba mtu yeyote yule atakayepata athari ya kuanguka atapata huduma hii, sasa itakuwaje kuwaje. Hebu Mhe. Waziri, akija anifahamishe.

Mhe. Spika, vile vile, katika ukurasa wa 373 kifungu cha 13(3) ambacho kinasema;

> "Mtu yeyote ambaye anakusudia kukata mkarafuu kwa madhumuni ya shughuli za maendeleo atatakiwa kuomba kibali kwa Mhe. Waziri"

Mhe. Spika, hiki kifungu ni kizuri sana na nakiunga mkono. Kwa sababu siku hizi ukataji wa mikarafuu umekuwa mkubwa. Mikarafuu sasa hivi inakatwa bila ya kisisi, nadhani jambo hili ni zuri na Mhe. Waziri, asiwe rahisi kutoa kibali.

Nataka nitoe mfano Mhe. Spika, kwa mradi wa maji mijini unaofadhiliwa na *ADB* kule Pemba ambao hivi sasa unaendelea. Mradi ule Mhe. Spika, umekata mikarafuu mingi kwa sababu ya kutengeneza njia ya kupitisha vifaa vyao vya kuchimbia visima vya maji.

Mhe. Spika, nadhani walifanya hayo kwa sababu kulikuwa hakuna udhibiti. Kwa hivyo, wakati sasa hivi tunapitisha sheria hii na kutakuwa na udhibiti namuomba sana Mhe. Waziri, asiwe rahisi kutoa vibali kwa kukatwa mikarafuu. Kwa sababu maeneo mengine iliyokatwa ile mikarafuu unajua kama hapa njia ingeliweza kupita, lakini waliamua kukata mikarafuu. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri, awe makini.

Mhe. Spika, nimalizie kusema kwamba Mfuko huu utakuwa na maana kutegemea na namna fedha za Mfuko zitakavyotumiwa. Ikiwa fedha

zitalengwa kwa wakulima hasa wa mikarafuu, basi nadhani lengo letu litafikia, lakini ukitumika vyenginevyo, basi ile dhamira ya kupitisha mswada huu haitakuwepo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, na hapa awe makini.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na naunga mkono mswada huu.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru *Allah* kutujaalia Ijumaa hii ya leo mchana huu kuweza kupata nafasi hii adhimu na mimi kutoa mawazo yangu juu ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya mwaka 1985 na kuweka sheria hii mpya.

Mhe. Spika, kwa kweli hii sheria ni kitu muhimu kuwa nayo ili kuweza kukijali kwanza hiki kilimo cha mikarafuu na kuwajali wakulima, wakodishwaji na wachumaji wa zao hili la karafuu. Hili zao ni zao moja kongwe sana hapa nchini, iliundwa sheria hapa mwaka 1985, lakini inaelekea kwamba haikujitosheleza.

Lakini ukiangalia pia mwaka huo hadi leo ni muda mrefu mno ambao serikali mfano wake kama ilijisahau kiasi fulani. Hata Waswahili waliwaambia wakulima wa mpunga kwamba, "Umeacha wakati wa kusia wajasia makobe yashalia". Maana yake ule wakati wa kusia hukusia mvua zinakaribia kuanza ndio mkulima anatakiwa afanye matayarisho ya kusia mpunga wake, ili hata makobe yakija yakilia maji yashasambaa katika mashamba awe tayari anajiandaa kwa upalizi na mambo mengine.

Sasa na sisi kipindi chote cha kuutunza mkarafuu hatukushughulika mpaka Mhe. Spika, tunakujashughulika mkarafuu haupo tena duniani, umebakia mchache mno. Mhe. Spika, utakaposafiri hebu jaribu kuiangalia mikarafuu iko hali gani, karibu asilimia 90 ya mikarafuu tayari imeshaota mvi na mvi ni dalili ya ufu. Kwa hivyo, hivi sasa ni kutafutana muhali, hicho ndicho kilichobakia, sasa sio mbaya sheria kuwepo, lakini pia tulijisahau kuushughulikia mti huu wa mkarafuu mpaka tumekuja dakika za mwisho.

Mhe. Spika, kwanza niunge mkono kwa wale wachangiaji waliopita jana na hawa wanaoendelea leo, kwamba vifungu vyote vile vilivyochangiwa, basi mawazo yao ni miongoni mwa mawazo yangu. Kwa kuwa kutokana na muda kuwa ni mdogo sitaweza kurejea rejea katika vifungu vile, lakini niseme navi-*support* vifungu vile.

Na kwa vile ambavyo vinahitaji kufanyiwa marekebisho, basi vifanyiwe marekebisho hasa ile sehemu ambayo imeambiwa hata ule mkarafuu mkavu

uliokwishakufa, basi ni vigumu kwa mkulima kuweza kuutumia. Hapa ni lazima mkarafuu ambao ushakufa wizara au shirika watakuwa hawana uwezo wowote wa kuweza kuurejeshea uhai, lakini pale mkulima wa ule mkarafuu atapata faida, (a) ataweza kupata kuni, kupata miti mingine ile kuweza kuuza ili kuweza kupata pato katika ule mti wake ambao umekufa.

Kwa hivyo, sehemu kama hii ya mikarafuu ambayo hatuna uwezo nayo tena kuirejesha katika hali ya uzima, basi wenye mashamba haya iwe ni ruhusa kwao kuweza kufaidika kwa rasilimali yake ile aliyonayo.

Mhe. Spika, nianze katika ukurasa wa 370 kuanzishwa kwa kikosi kazi, kifungu cha 7(1). Mheshimiwa silikatai hili kuanzisha kikosi kazi, hivi sasa kama walivyosema wenzangu hapa kwamba kuna vikosi kazi katika kila barabara na kila madiko kuzuwia hali hii ya magendo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad, amesema hapa tusiangalie tu magendo, tuangalie kwa nini watu wakafanya magendo ndio la msingi, si hasha hata tukianzisha hivi vikosi kazi vikawa vimefurutu kila kichochoro, lakini kama kikosi hicho hakikutunzwa, basi bado magendo yataendelea na yatakuwepo.

Mhe. Spika, katika vikosi kazi hivi sasa tulivyonavyo tayari kuna malalamiko wanalalamika, kwamba kuna baadhi wanapewa posho katika kulinda kwao, lakini posho hili halienei kwa askari wengine. Hili lalamiko lipo, sasa kama wengine wanajaliwa, wengine hawajaliwi katika maposho au kama yanatoka, lakini wale walioko katika ulinzi posho lile haliwafikii, mimi imani yangu ni kwamba hapo magendo yatakuwepo.

Kwa sababu binadamu ni binadamu kila mmoja anahitaji kutunzwa na kuishi, kama hivi vikosi wengine wanafaidika na wengine hawafaidiki na yeye atatafuta njia yoyote ile anufaike, mzigo unaweza ukapitishwa pale wakapata chochote na wao wakaweza kuishi. Kwa hivyo, ningeliomba sana hapa Mhe. Waziri, wanapotoa maposho kwa hivi vikosi kazi, basi wawe na uhakika kwamba vikosi kazi hivi kila mmoja amefaidika na posho lile. Kinyume na hivyo, bado magendo yataendelea kwa sababu nchi imejaa rushwa.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu cha 11(c) kinasema kwamba kulinda, kulima na kutibu au kusafisha mashamba ya karafuu. Mheshimiwa suala la kutibu tunakumbuka miaka ya 1980 mpango wa kutibu mikarafuu tulikuwa nao tukiita *dieback*. Faida ile haikuonekana, mikarafuu ilikuwa inatibiwa ndani ya miaka mitano utaukuta mkarafuu ni mzuri na mzima kuliko, lakini haimalizi miaka mitano mingine mkarafuu ule unakufilia mbali. Hapa pia nilikuwa nataka nipate maelezo kwa Mhe. Waziri, huu utibabu

anaokusudiwa hapa ni upi, ni kuja kufanya kama awamu zilizopita na kuja kuimaliza mikarafuu au amegundua utibabu mwengine. Kama ni hivyo basi, tupate maelezo huu utibabu utakuwaje.

Mhe. Spika, nikirudi nyuma kidogo katika kifungu cha 5(j) kinasema kwamba, kusaidia huduma za matibabu na huduma nyengine za bima kwa wakulima na watu waliopata madhara. Mheshimiwa jambo hili naiomba sana serikali ilipe kipaumbele, katika kazi moja ya utumwa ni uchumaji wa karafuu.

Mhe. Spika, ile ni kazi moja ngumu, karafuu ina utumwa bwana, karafuu kwa kule kwetu Pemba sana iko katika maeneo ya milima, pengine unapanda milima mitatu minne ndio utafika kwenye kambi unayokusudia kuchambua karafuu. Kibarua azitoe chini huko mpaka azifikishe kwenye kambi ya karafuu, akizifikisha pale kazi yake haijamaliza zinahitaji kuchambuliwa na likitokea la kutokea akapata ajali mchumaji huyu kwa kweli ni dhiki moja kubwa sana.

Kwa hivyo, kuwajali hawa watu wanaopata matatizo kama hayo ya kuanguka, basi serikali hili walipe kipaumbele na huduma zao ziwe nzuri, isiwe mtu keshapata ulemavu kazi yake ilikuwa kuchuma karafuu pengine na minazi, lakini sasa hiyo kazi ikamshinda na ikawa maisha sasa imekuwa ni dhiki kwake. Kwa hivyo, hii huduma iwe endelevu na tena iwe na tija na huruma kwa hawa watu wetu ambao watapata ajali kama hizo.

Mhe. Spika, niende katika kifungu cha 18 katika mabadiliko kifungu cha 3 pale, kinasema kwamba “kila mkulima mmiliki au mkodishwaji wa mikarafuu atahakikisha kwamba karafuu zake ziko katika hali nzuri na hazijaharibika au kuchanganyika na vitu vingine wakati wa uchumaji”. Nataka nifike hapo wakati wa uchumaji.

Mhe. Spika, mchumaji wa karafuu ni mtu anayehitaji kupata pishi nyingi na wakati ule wa kuchuma inawezekana wengine wanalikata lile shada na majani yake, hapunguzi hata yale majani anayatia katika chombo chake cha kuhifadhia. Lakini na mkarafuu ni mti ambao unaacha matawi makavu, katika kuchuma kule matawi yale mengine yanadondoka, yanakatika na kuingia katika kile chombo anachochumia mchumaji wa karafuu. Kwa hivyo, kama tutambana huyu mchumaji wa karafuu akilikata lile shada apukuchue majani na majani yale ahakikishe kayatupa kando halafu aje arudi huku achume ili karafuu zake ziwe safi, kwa kweli hapa tutakuwa hatujawatendea haki wachumaji wa karafuu.

Ni lazima sheria ya sehemu hii mchumaji wa karafuu apewe uhuru jinsi alivyokuwa na taaluma yake ya kuchuma karafuu, kama anachuma karafuu na majani anatia humo humo, kama wakati wa kuchuma kuna majani mengine yanaanguka katika pakacha au katika kapu la kuchumia karafuu. Ninachokiomba hapa Mhe. Spika, wakati wa kuzichambua karafuu hapa ni pahala pamoja pakuangaliwa usafi wa karafuu, wakati wa kuzichambua ni sehemu ambayo inatakiwa huyu mchumaji kwa sababu ndiye anayechambua karafuu zake ahakikishe zile takataka zimetolewa.

Katika kifungu hiki uchambuzi wa karafuu sioni wapi kimeelekeza, hamna. Kwa hivyo, naomba wakati wa uchambuzi wa karafuu zihakikishwe karafuu ziko safi. Hapa tutasaidia upunguzaji ule wa takataka na wakati wa kuzisafisha kwa kwenda kuuza, pia zionekane kuwa zile karafuu ziko safi. Lakini kama tutambana mchumaji wa karafuu iwe hamna jani wala nini, kwa kweli tutamfanya kama alikuwa anachuma pishi 30, awe anapata kama pishi tano au kumi. Kwa hivyo, tutamnyima ile mori yake ya uchumaji wa karafuu.Hivyo, naomba hapa tupafanyie marekebisho Mhe. Spika.

Pia, niseme kwamba katika kifungu cha 18(5) kinasema kwamba “kila mkulima, mmiliki au mkodishwaji wa mikarafuu atazianika karafuu kwa kutumia jua tu na vifaa vilivyothibitishwa kwa kuanikia”. Wenzangu wamesema hapa, kwamba wakati wa uchumaji wa karafuu wanaomiliki karafuu huwa ni watu wengi, karafuu ni msimu wa watu wazima mpaka watoto wadogo. Kwa hivyo, karafuu kuna baadhi ya hawa vijana wetu wadogo wadogo huwa wanakwenda wakiokota mpeta. Mpeta tunahesabu ni ile karafuu ambayo imedondoka kwenye mkarafuu wake ikaja ardhini, ile unaokota moja moja.

Wakati wa msimu mkarafuu hupunguzwa matawi wengine huomba vishada waangushiwe na wale wanaochuma karafuu na mara nyingi wenye mashamba yale wanaridhika na hili.

Kwa hivyo, kwa hali yoyote karafuu kila mmoja atakuwa anayo, lakini haiwezekani mtoto kwenda kuokota kikopo cha karafuu ukamwambia awe na chombo kinachothibitishwa, hii itakuwa ni ngumu Mhe. Spika, tuone tu kwamba wale ambao umiliki wao wa karafuu ni mwingi, basi waweze kwenda na vyombo hivi ambavyo vimethibitishwa na wale ambao wanaokota kikombe cha karafuu, basi wawe na utaratibu ambao karafuu ile itakauka na iwe katika hali nzuri. Lakini tukiweka kwamba tutumie vyombo hivi tu vilivyotajwa viwili, basi karafuu baada ya kuzipata nyingi itakuwa hazipatikani tena, watu watasamehe.

Kwa sababu sheria iliopo ukikamatwa ni shilingi 3,000,000; leo watoto wamekwenda kuokota tu, lakini wameanika katika maeneo dhaifu wamekamatwa, kukamatwa wameshtakiwa, wamepandishwa Mahakamani wamehukumiwa, wamefungwa au wametoleshwa faini shilingi milioni tatu kaokota kikombe kimoja, hizo karafuu hazitaokotwa tena na kama hazikuokotwa serikali pia itapata hasara. Serikali ikipata hasara na hawa wananchi pia watapata hasara kwamba watakuwa hawawezi tena kujivisha. Kwa hivyo, ni lazima hii sheria iwekwe wazi ili wananchi wetu waweze kupata mafaniko katika mzao huu wa karafuu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo ni mengi niliyonayo ya kusema, lakini muda wako hautoshi. Kwa hivyo, niseme kwamba baada ya mabadiliko hayo tuliyoyataja pamoja na wenzangu hapa yatakapofanywa, basi nitaunga mkono hoja. Asante sana.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) aliyenijaalia katika safari ndefu niliyokuwanayo na nikaweza kurudi nyumbani salama na kujumuika na wenzangu.

Halafu vile vile, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na vile vile, nitoe mkono wa pole kwa wenzangu waliofiliwa. Nakuja hapa nasikia wenzangu wengine wamefiliwa na mama zao, dada zao, hata wewe Mhe. Spika. Kwa hivyo, natoa mkono wa pole kwa ujumla sote tuliopo hapa.

Vile vile, nawatakia dua wenzetu wanaoumwa Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma. Mwenyezi Mungu awajaalie awape nafuu ili tuweze kushirikiana katika kazi zetu hizi za Baraza.

Pia, nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuweza kuzipa kipaumbele karafuu. Mheshimiwa, karafuu ni uti wa mgongo, kwa kule kwetu ukiingia msimu huu ndio msimu wa neema na mavuno. Mimi sitakuwa na mengi kwa sababu mswada huu tumeupitia kifungu kwa kifungu, isipokuwa katika Sehemu ya Nne ukurasa wa 371 kifungu cha 10(1) kinachoeleza kuwa; “kutakuwa na daftari la usajili la wakulima” inaendelea kifungu cha 10(2) na 10(3); “kutakuwa na usajili wa mashamba”.

Mimi nasema hii inawezekana Mhe. Waziri, kwa sababu waliopewa eka wote walisajiliwa na ukienda kule kunakohusika utawakuta watu wale waliopewa eka tatu tatu, wote wapo wamesajiliwa. Sasa wenye mashamba ya karafuu naomba katika hili daftari la kuwasajili wenyewe waweze kusajiliwa majina yao, shamba ilipo, idadi ya mikarafuu yake pamoja na picha ya

passport size. Nasema hivyo Mhe. Spika, kwa maana yangu, kunatokea ubadhirifu watu kuweza kughilibu watu kuuza mashamba si yao na kesi zimeshatokea nyingi tu.

Hata hivi juzi juzi kesi hizo tumezipata, watu wanauza mashamba ya karafuu, wanatapeli mtu, anaoneshwa shamba na watu wanapata nyaraka za kufoji ambazo hazijulikani nyaraka zile zinapatikana wapi na hata saini za sheha zinatiwa. Mtu anaambiwa shilingi milioni 40 anatoa shamba si lake, watu wakienda pale anatafutwa muuzaji haonekani na shamba unaambiwa si lake.

Kwa hivyo, mimi naomba waziri aweze kuyafanyia usajili mashamba haya na kwa kila mmoja ajulikane shamba lake liko wapi, miti mingapi, jina lake na picha awe nayo, yule atakayetokea kwenda kufanya ubadhirifu akifika pale likitizamwa shamba hili aambiwe shamba hili ni la Mhe. Pangu Ameir Kificho, sio lako, arudi nyumbani. Kwa sababu tushapata matatizo haya ya kufanyiwa ubadhirifu.

Halafu niseme tu kuhusu aina za karafuu. Mhe. Spika, waziri ajitahidi sana katika upandaji wa mikarafuu tusije tukapanda karafuu kama nilizozikuta nilikokwenda. Mheshimiwa, kuna karafuu zinapandwa huko zinatiwa mbolea hiki kidole kidogo, wiki tatu karafuu haijakauka. Kwa hivyo, mimi naomba karafuu kama zile huku sisi tusiwenazo tuwe na karafuu zetu za asili, watu wasije kukubaliwa kupanda mikarafuu wakatia mbolea za kukuza karafuu zile mpaka ikanenepa ikaondoa hadhi yake.

Halafu hizi karafuu ziko za aina tatu, watu walizozisema hapa. Kwa sababu hapo zamani tulipokuwa watoto sisi tulikuwa tukiokota karafuu za mpeta na karafuu zile utazikuta zimo aina nyingi, nyengine nyeusi, nyengine hazina vichwa, nyengine hazina ubora, lakini zilikuwa zinanunuliwa karafuu zile na watoto wakapata kutumia. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, namuomba katika sheria hii hawa wasibanwe. Kwa sababu kule kwetu neema hii ikiingia kwa kila mmoja anaona ndio mavuno na watoto wote wanajibwaga hata ukimwambia vipi hasikii anakwenda kwenye mkarafuu kuweza kufanya kazi hii.

Mhe. Spika, tukienda kwenye kilimo, miche ya mikarafuu iko kule kilimo, halafu kuna mikarafuu ambayo watu wanapanda ile ya asili maboi, iliyomo mle mle shamba, watu wanachimba halafu wakapanda. Wengine ikiwa yameota vizuri yako mbali mbali wanayalimia wanaondoa kile kiyale ili ijibwagebwage vile vile inatumika kuwa ni mikarafuu. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, hapa napo vile vile tunataka tupate mahitaji mazuri kuweza kuboresha mambo haya ili karafuu ziwe za kudumu.

Pia, niseme katika hii nguvu kazi wengine wanaitafsiri kuwa kutakuwa na majeshi mengi au kutakuwa na Mgambo wengi. Nguvu kazi zamani kulikuwa na wale waliokuwa wakifanya kazi ya *dieback* kupitia kwenye mashamba, kuna mashamba mengi yaliyopandwa minazi na *dieback.* Mashamba yale hatujui kama walikuwa wakilipa wenyewe shirika au serikali. Haya yanaweza kuwa mashamba yale ambayo mfano mimi nina shamba na nishalisafisha, lakini siwezi kupanda au sina taaluma, ikawa iko nguvu kazi ile ya kutolewa kama ilivyokuwa hao *dieback* zamani, kuweza kupanda mikarafuu ile na kuishughulikia ikahuwika na ikaja juu katika shamba lile. Sijajua mwenye shamba watapigwa faini kiasi gani katika kuwapa wale, litalipa shirika au serikali? Lakini vile vile, tungelirudisha kufanya hivyo katika hicho kikosi kazi. Kwa sababu kikosi kazi unaweza kukitafsiri kwa mambo mengi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nauunga mkono mswada huu kwa sababu mswada ni mzuri na una lengo zuri. Mimi nimeupitia mswada huu chini ya Mwenyekiti wangu Mhe. Salmin Awadh Salmin. Hivyo, nilikuwa nataka nizungumze tu kidogo kama kuwaamkia wenzangu katika Baraza. Kwa hivyo, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kuwashukuru kwa kushirikiana katika shughuli zetu na nafikiri dalili inaonesha kwamba tumeshafikia pahala pazuri kwa mchango wa mswada huu. Na makusudio ni kwamba wakati wa jioni Mungu akipenda, basi tuwaombe wahusika, Mhe. Naibu Waziri na Waziri ili kuweza kufanya majumuisho. Kwa hivyo, niwaombe basi kwa kuwa tumeshafikia pahala pazuri tusitishe shughuli zetu kuanzia sasa ili tuwape muda Mhe. Waziri na naibu wake kwenda kujitayarisha kwa kufanya majumuisho hapo jioni.

Baada ya hayo, basi Waheshimiwa Wajumbe niakhirishe kikao hiki hadi saa kumi na moja jioni leo hii.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nadhani kipindi cha asubuhi tulimaliza michango kwa Wajumbe. Sasa ni nafasi ya Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na baadae tutamwita Mhe. Waziri, amalize majumuisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi jioni hii ya leo kunipatia nafasi ili niweze kuchangia mchango huu wa Sheria ya Kufuta, Sheria ya Karafuu nambari 11 ya mwaka 1985 na kuanzisha Sheria ya Maendeleo ya Karafuu ya mwaka 2013 na Mambo mengine yanayohusina na hayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia na kusema machache.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bishara, Fedha na Kilimo, pamoja na Wajumbe kwa kazi kubwa walioifanya kwa kutusaidia katika kuupitia mswada huu na kufanya marekebisho ili kuimairika mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, miongozo yao imekuwa ni mizuri na imetupa maelekezo kama ambavyo ameyasoma Mhe. Hija Hassan Hija, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Mhe. Naibu Spika, tunaahidi kuwa tutayafanyia kazi yote yale yalioelekezwa na kupendekezwa ili kuweka utaratibu wa kuendeleza taratibu zao za karafuu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu umechangiwa na Waheshimiwa wa kusema jumla 11 akiwemo Mhe. Hija Hassan Hija, kwa niaba ya Mwenyekiti. Waliochangia kwa maandishi Mhe. Naibu Spika, ni Waheshimiwa 6. Mengi tumeelekezwa na kushauriwa na tunasema kwamba tunayachukuwa na tutayafanyia kazi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, niseme moja moja tu na kwa kina atakuja kueleza hapa Mhe. Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko, atakapokuja kufanya majumuisho.

Limezungumzwa suala la kubadilisha jina zima la Mswada Mhe. Naibu Spika, tunalichukuwa hilo na tunalifanyia kazi tayari na ndio maana mswada huu sasa unasomeka kwamba ni Sheria ya Karafuu nambari 11 ya mwaka 1985 na kuanzishwa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu na mambo yanayohusiana na hayo, ndivyo unavyosomeka sasa.

Lakini Mhe. Nabu Spika, tafsiri ya neno Shirika nayo tumekubaliana nayo kama walivyopendekeza kwamba lisomeke Shirika la Biashara ya Taifa Zanzibar ambalo limeanzishwa kwa sheria namba 11 ya mwaka 2011.
Mhe. Naibu Spika, tumekubaliana pia na Mhe. Mwenyekiti na kamati yake kwamba Mkurugenzi Muendeshaji wa Shirika yeye ndio awe mtendaji mkuu wa mfuko huo. Kwa hivyo, tumelichukuwa hilo. Lakini pia, tumekubaliana

nao Mhe. Naibu Spika, kwamba tuingize fedha ambazo zile zitakusanywa katika faini katika mfuko huu wa Maendeleo ya Kafaruu. Tumesema kwamba hatuna pingamizi nalo.

Kwa hiyo, pesa hizi zote zitakazokusanywa katika fani hiyo Mhe. Naibu Spika, zitaingizwa katika mfuko huu wa Maendeleo ya Karafuu na pia suala zima la vibali, sasa wahusishwe Masheha kikamilifu nalo tumekubaliana nalo. Pamoja na mawazo mengi yaliyojitokeza hapa. Lakini bado ukweli unabakia pale pale kwamba Masheha Mhe. Naibu Spika, ndio serikali katika ngazi za mitaa.

Mhe. Naibu Spika, takriban Wajumbe wote wamezungumza umuhimu wa kuwaelimisha wakulima na zaidi wa karafuu kuhusiana na sheria hii hasa vipengele vile vinavyozungumzia adhabu. Kwa sababu tumepewa indhari na tumeizingatia, tusije kujikuta wakulima wanaishia kufungwa. Kwa sababu wasiwasi walionesha Waheshimiwa ni kwamba huenda wakashindwa kulipa ile faini ya milioni tatu. Kwa hivyo, tuwaelimishe sana na hilo tunalichukuwa kwa kulifanyia kazi. Tutatoa elimu kadri tutakavyoweza sisi kama wizara, lakini zaidi kupitia katika shirika letu la *ZSTC*.

Mhe. Naibu Spika, suala zima la kutoa zawadi kwa wakulima wanaofanya vizuri. Suala hili tumekuwa tumelianza toka mwaka ule wa 2011, kama mlifuatilia Waheshimiwa Wajumbe siku ya kufungua msimu ule wa karafuu. Mhe. Rais, alikuja Pemba tulikuwa na wiki nzima ya kushughulika na masuala ya karafuu na hatimae wale wakulima bora wa zao la karafuu waliouza karafuu nyingi kwa shirika letu wote walipewa zawadi bila ya kukosekana.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, tunasema hili tunalichukuwa na tutazidi kulizingatia na kulifanya liwe bora zaidi kadiri miaka inavyokwenda kama ambavyo Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu wametushauri.

Mhe. Naibu Spika, suala la kutumia mbinu za kisasa katika kuchuma karafuu. Suala hili nalo tumesema ni vyema kulizingatia kwa kina. Mhe. Naibu Spika, tunasema tunalichukuwa na wataalamu wetu ndani ya wizara watalifanyia kazi kwa kuangalia jinsi gani, basi wenzetu wenye zao hili la karafuu kama kuna mbinu za ziada wanazozitumia zaidi kupanda juu ya mikarafuu kwa kamba na mwisho wake baadhi yao huanguka na kuumia.

Basi tutalifanyia kazi kwa sababu sote kwa umoja wetu hatufurahi na hatupendi hata kidogo matatizo yanayowakuta wakulima wa karafuu pale wanapoanguka kwa sababu ni nguvu kazi ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, suala zima la kurahisisha upatikanaji wa vifaa wakati wa kuvuna karafuu. Suala hili nalo ni zuri, ni vyema tukalichukuwa na tukalifanyika kazi kwa uangalifu mkubwa sana ili kupunguza urasimu kwa wakulima wetu waweze kupatiwa zana kama majamvi na vyengivyo bila ya urasimu wowote, ili waweze kuuza karafuu katika shirika letu bila ya matatizo.

Mhe. Naibu Spika, usarifu wa karafuu nalo limezungumzwa takriban na Waheshimiwa wengi ndani ya Baraza hili tukufu. Tunasema kwamba mpango huu Mhe. Spika, tutauingiza katika mpango mzima wa maendeleo ya karafuu. Tumeanza na kama kuna Waheshimiwa wameweza kufatilia katika Sherehe zetu za Mapinduzi miaka 50, basi Mhe. Waziri, alizindua vifungashio vya kisasa kabisa vya karafuu katika ujazo tofauti, huu ni mwanzo. Lakini tutaendelea zaidi katika kuziongezea ubora ili tuweze kuongeza thamani hatimae karafuu zetu ziweze kuuzika bei nzuri na kubwa zaidi katika soko la dunia.

Kwa hivyo, hoja hii nayo Mhe. Naibu Spika, tunasema kwamba tumeichukuwa pamoja na kwamba tumeshaanza kuifanyia kazi. Lakini tutaongeza *speed* ya kuifanyia kazi ili matokeo yake yaonekane katika muda sio mrefu.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya sheria hii mpya kuna kipengele namba 5 kinazungumzia utaratibu mzima wa fedha zile za mfuko wa karafuu zitakazotumika. Kwa maana hiyo, basi tunachukuwa wazo lile ambalo limetokana na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwamba lile neno la kumuidhinisha au kuidhinisha bodi kutumia fedha kama ambavyo wataona wao inafaa, basi linafutwa katika sheria hiyo na tubaki tu. Yale yaliyoelezwa katika ile sheria, kwamba mfumo ule unajikita katika maeneo yale peke yake na sio kuidhinisha bodi kutumia fedha hizo vyenginevyo.

Kwa hivyo, maneno ambayo wanayoidhinishia kama itakavyoidhinishwa na bodi yanafutwa kabisa katika sheria hiyo ili kubakie matumizi yaendelee kuwa ni yale yalioainishwa katika kipengele namba 5 cha sheria hii mpya ya karafuu. Mhe. Naibu Spika, nimalize nimpishe Mhe. Waziri, kwa kuzungumzia suala zima la vituo vya ununuzi wa karafuu.

Nataka nichukuwe nafasi hii Mhe. Naibu Spika, kupitia Baraza hili kumpongeza sana Mhe. Rais ambaye amekuwa akitupa maelekezo ya hekima na busara kubwa ya jinsi ambavyo tutaweza kuwavutia wakulima wetu wa karafuu waje wauze karafuu zao *ZSTC*.

Mhe. Naibu Spika, tumefata ushauri ule na kwa kufanya hivyo toka msimu ule wa karafuu wa mwaka 2011/2012, tumekuwa tukijenga vituo vipya vya karafuu na tumekuwa tukivitengeneza vile ambavyo vipo ili navyo viwe katika ubora kama vile vipya ambavyo tunajenga. Mpaka sasa Mhe. Naibu Spika, tayari vituo 8 vimeshajengwa vipya kabisa na *ZSTC* katika kipindi hiki. Lakini na vyengine 6 vimetengenezwa viko katika ubora wa hali ya juu. Kwa hivyo, tumeweza kujenga pamoja na kutengeneza vilivyopo na vituo vyote ni 14.

Lakini tutaongeza kasi ya kuwasogezea wakulima wa karafuu vituo karibu zaidi ili kuwapunguzia masafa wasitembee na karafuu masafa marefu. Kwa hivyo, hilo tunalichukuwa Mhe. Naibu Spika, kwa kulifanyia kazi na kama kuna Waheshimiwa tulishiriki pamoja ziara ile ya Mhe. Rais, kuna vituo ambavyo vilifunguliwa na pia Mhe. Waziri, alifungua kituo kingine katika sherehe zetu za miaka 50 ya Mapinduzi.

Sio tu vituo Mhe. Naibu Spika, lakini pia tumesogeza maji katika vituo hivyo na tumejenga vyoo katika vituo hivyo. Lakini pia tumewaekea maeneo ya kukaa wakulima wetu wakati wanasubiri kuhudumiwa na watendaji wa *ZSTC* katika vituo hivyo. Huduma nyengine Mhe. Naibu Spika, kama kahawa na tende zinapatikana katika vituo hivyo ili kuwavutia wakulima wetu waweze kuongeza imani kama ambavyo tayari wameonesha imani kwa serikali yao ya kuuza karafuu zao zote *ZSTC*. Na kwa taarifa ya Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika, mpaka sasa lengo tulilojiwekea ndani ya wizara ni manunuzi ya karafuu kutoka kwa wakulima tayari tumeshavuka lile lengo na tunakwenda vizuri sana na bado tunategemea karafuu zitakuwa nyingi sana.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba na mimi naunga mkono sheria hii nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuunge mkono sheria hii sote kwa pamoja ili tuweze kuwatendea vizuri zaidi wakulima wetu wa zao hili la karafuu. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho ya Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Karafuu namba 11 ya Mwaka 1985 na kuanzisha sheria mpya ya maendeleo ya karafuu ya mwaka 2013 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mktukufu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako Mhe. Naibu Spika, kwa nafasi hii ya kufanya majumuisho ya mapendekezo ya Mswada wa Sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati wa Biashara, Fedha na Kilimo Mhe. Salmin Awadh Salmin pamoja na Wajumbe wa kamati yake kwa kazi kubwa waliofanya. Kuupitia mswaada huu na kufanya marekebisho ili kuimarisha mswada huu na miongozo mizuri na maelekezo ya kutosha waliyotupa na subira kubwa waliokuwa nayo na wakatoa hotuba nzuri iliyosomwa na Mhe. Hija Hassan Hija, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Tunaahidi kuwa tutayafanyia kazi vizuri kabisa kama ilivyopendekezwa ili kuweka utaratibu wa kuendeleza zao la karafuu hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwataje Wajumbe wote ambao wamechangia katika mswada huu tangu jana:
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Ismail Jussa Ladhu
Mhe. Asha Bakari Makame
Mhe. Salum Nassor Juma
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Marina Joel Thomas
Mhe. Abdalla Mohd Ali
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
Mhe. Mohammed Haji Khalid
Mhe. Suleiman Hemed Khamis
Mhe. Jaku Hashim Ayoub
Mhe. Subeit Khamis Faki
Mhe. Rufai Said Rufai
Mhe. Hamad Masoud Hamad
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Salim Abdalla Hamad
Mhe. Raya Suleiman Hamad
Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Naibu Spika, hawa ndio wachangiaji 21 waliochangia waraka huu kwa maneno.

Wengine ambao wamechangia waraka huu kwa maandishi ni :-

Mhe. Bikame Yussuf Hamad
Mhe. Farida Amour Mohammed
Mhe. Salma Mussa Bilal
Mhe. Asha Abdu Haji

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa

Vile vile, kachangia tena Mhe. Suleiman Hemed Khamis.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako waliochangia mswada huu kwa maneno na kwa maandishi. Wajumbe wote wamechangia kwa uwazi na kwa ufasaha na umahairi mkubwa. Michango yao na mapendekezo yao kwa ujumla imesaidia sana kufanya marekebisho ya msingi kwa baadhi ya msingi na baadhi ya vifungu vya mswada huu.

Napenda kukuhakikishieni kwamba kwa michango, maelekezo na ushauri tumeyapokea kwa mikono miwili na tutayafanyia kazi ipasavyo kwa ajili ya utelekezaji mzuri wa sheria hii katika kutekeleza na kulinda zao la karafuu. Aidha nashukuru pia kwa mchango na ufafanuzi wa kina uliotolewa na Mhe. Naibu Waziri, wangu wa Biashara, Viwanda na Masoko katika kufanya majumuisho haya ya mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali katika Baraza lako yanahusu mambo ya jumla na mambo mahasusi yanayotakana na maudhui kwa mujibu wa vifungu vilivyomo katika mswada huu wa sheria ya maendeleo ya karafuu ya mwaka 2013.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu hoja jumla zilizojitokeza naomba kutoa ufafanuzi wa hoja hizo kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza nawashukuru Wajumbe wote ambao wametoa pongezi nyingi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Wakatoa pongezi nyengine kwangu mimi binafsi na Mhe. Naibu Waziri wangu, Katibu Mkuu wangu, Naibu Katibu wangu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Tunafurahi sana kwa kupata pongezi hizi na tunawahakikishiwa Wajumbe wetu kwamba hatutogeuka Mgema, tutafanya kazi nzuri zaidi baada ya kupata pongezi hizi kwani zimetupa moyo na tunajua kwamba mko pamoja na sisi na naamini kwamba mtazidi kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, jina la Mswada lilipendekezwa kwamba lisomeke Sheria ya Kufuta Sheria ya karafuu ya namba 11 ya mwaka 1985 na kuanzisha sheria ya Maendeleo ya Karafuu na mambo yanayohusiana na hayo. Wizara inakubaliana na pendekezo hilo wala hatuna pingamizi yoyote.

Tafsiri ya Vyama vya Ushirika imependekezwa kuongezwa kwa neno Ushirika ambalo ni Shirika la Taifa Zanzibar liloanzishwa kwa Sheria namba 11. Wizara inakubaliana na pendelezo hili bila ya tatizo lolote. Mtendaji Mkuu wa mfuko amependezwa katika kifungu cha 6, isomeke kwamba Mkurugenzi wa Vyama vya Ushirika ndie atakaekuwa mtendaji Mkuu wa Mfuko. Wizara inakubaliana na pendekezo hilo bila ya tatizo lolote.

Kufutwa kwa kifungu namba 18(2) Mhe. Naibu Spika, imependekezwa kwamba kifutwe na baadae kisome kifungu cha 18. Wizara imekubaliana na mapendekezo hayo bila ya matatizo yoyote. Kuingizwa katika mfuko wa fedha zinazotokana na faini. Mhe. Naibu Spika, imependekezwa zile fedha zinazopatikana ziingizwe kwenye mfuko. Hoja hiyo imekubalika na itasomwa kama kifungu cha 26(2) wala hakuna tatizo lolote.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kupatiwa kibali kwa Masheha. Suala hili la kupatiwa Masheha fomu kwa kutoa vibali vya kuhamisha karafuu kutoka sehemu moja kwenda nyengine. Limekubalika na litafanyiwa kazi bila ya matatizo lolote.

Utayarishaji wa kanuni za sheria. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba katika sheria hii kuna haja ya kuwa na kanuni mapema iwezekanavyo. Hivyo, wizara inaahidi kutayarisha kanuni hizo ili ziwe sambamba na mswada huu hasa ukizingatia kwamba mswada huu unaaza kutoka mara moja Mhe. Rais atakapoweka saini yake.

Utoaji wa elimu kwa wakulima na wananchi Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kutoa elimu ya masharti, sheria hasa katika maeneo yanayohusiana na adhabu, vifaa vya kuanika karafuu ni muhimu sana. Wizara inaahidi katika Baraza lako tukufu kutekeleza kuhusu suala hili kwa umuhimu wake na kwa wakati ili wananchi wasije kusumbuka na sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, vigezo na upatikanaji wa fedha za mfuko imependekezwa kwamba ziwe wazi na visitumike kwa upendeleo wa aina yoyoye. Wizara inakubaliana na pendekezo hilo na itakuwa makini katika vigezo hivi na suala zima ili wananchi wasipate usumbufu na suala hili.

Kukosekama kwa adhabu katika kifungu cha 27-28 Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wameona kwamba katika vifungu hivyo haikuwekwa wazi adhabu inayopaswa kutolewa. Ufafanuzi wake kwamba vifungu hivi vinazungumzia makosa yatakayofanywa na shirika au wakala wa shirika. Makosa hayo yatajumuisha makosa yaliyoelezwa katika sheria hii na muhusika ataadhibiwa ipasavyo kulingana na kosa alilofanya.

Kikosi Kazi, Mhe. Naibu Spika, kimeulizwa kwamba kuna vikosi kazi vingapi vinahusika na magendo ya karafuu? Jawabu Mhe. Naibu Spika, kikosi kazi ni kimoja tu ambacho kinaongozwa na Mwenyekiti wake ni Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko ambacho kimeteuliwa na kinajumuisha wajumbe kutoka katika taasisi mbali mbali za serikali. Vizuizi vilivyoweka barabarani ni sehemu ya utekelezaji wa kazi za kikosi kazi.

Aidha, Wajumbe wamehoji kwamba matumizi ya Kikosi kazi ni makubwa. Mhe. Naibu Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi kwamba kazi za kikosi kazi ni kubwa na matumizi sio makubwa kama hivyo yanavyofikiriwa, kwa mfano mwaka 2011 tumeweza kuhifadhi karafuu karibu tani 2600 ambazo zilikuwa kila mwaka zinavushwa na kupelekwa Kenya. Katika mwaka 2012 tumeweza kuhifadhi tani 2600 na gharama zilizotumika kwa kikosi kazi ni tani 40 tu. Kwa hivyo, utaona namna gani kikosi kazi kinatumia rasilimali kidogo. Lakini inafanyakazi kubwa ya kuhifadhi magendo ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, matumizi ya kikosi kazi yanaendana na majukumu yake ya kuondosha magendo na masuala mengine yanayoharibu biashara ya karafuu. Kuhusu motisha kwa kikosi kazi wizara italifatilia suala hili ili manung'uniko yalivyo hivi sasa yasije yakaendelea. Kwa hivyo, kikosi kazi kinafanyakazi nzuri ya kuzuia magendo na tutahakikisha ili wahusika wasiwe na na malalamiko ya aina yoyote.

Kumependekezwa hapa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, tuweke siku maalum ya upandaji wa mikarafuu. Mhe. Naibu Spika, hili wazo zuri na wizara yangu italichukuwa wazo na tutafanya kila mwaka siku moja ya kupanda mikarafuu na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, tutamualika rasmi awe mgeni rasmi katika upandaji wa mikarafuu hiyo.

Kutoa zawadi kwa wakulima vile vile, ni wazo zuri sana na ndio maana tukafanya *registration* ya wakulima wote wanaokodi na wadau wote ili tuwe na vigezo vya kuona nani kafanya kazi nzuri zaidi. Kwa hivyo, mapendekezo ya kutoa vyeti au aina nyengine ya motisha kwa wakulima wa karafuu wanaofanya viziri, wizara imeshaacha utaratibu huu mwaka 2012 na itaendelea katika misimu ijayo. Huu ni ushauri mzuri na tutalifanyia kazi.Ahsante Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Usajili wa mashamba uko, lakini sisi tuna-*register* mkulima wa karafuu na kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 10(4) kwamba utaratibu wa usajili ya makundi hayo utaelezwa kwanini. Katika kanuni ambazo Mhe. Waziri, atazitunga kutakuwa na utaratibu mzima, nani anasajiliwa katika buku gani na kwa kazi gani na kwa namba namna gani. Kusitolewe kibadili cha kukata

mkarafuu Mhe. Naibu Spika, imependekezwa kwamba vibali vya kukata mkarafuu visitolewa kabisa.

Pendekezo hilo limezingatiwa katika kifungu 13(2) ambacho kimepiga marufuku kukata mikarafuu kwa ajili ya matumizi ya ujenzi. Hata hivyo, vibali vitatolewa kwa shughuli za maendeleo pekee baada ya kulipa fidia inayostahiki.

Mhe. Naibu Spika, hapa ni suala muhimu sana tuelewe kwamba sheria hii imekuja kuipa hadhi mkarafuu. Leo Mhe. Naibu Spika, Singapore kukata mti tu, si mkarafuu, mti njiani ukiukata utakoma maisha yako. Sasa sisi tumeweka sheria hii ili kuipa hadhi mikarafuu.

Mhe. Naibu Spika, kuna familia moja pale Wete imekata mikarafuu 100 kwa ajili ya kutengenezwa barabara. Mwenye mikarafuu ile baba mtu kafariki dunia kwa kupata kihoro kwa mikarafuu iliyokatwa. Hawajakaa vizuri familia ile ile, panataka kupitishwa umeme ikatwe mingine 50, mama mtu anasema kwamba mimi mume wangu ameshafariki mikarafuu 100 imekwenda msiba si mdogo. Sasa hivi mnataka kukata mingine 50 na mimi nina watoto 9 yatima wananitegemea.

Laiti huyu mikarafuu yake 100 iliyokatwa, angelipwa fidia nzuri inayofidia mikarafuu, kweli asingekufa kihoro. Angepata fidia nzuri na angejiimarisha akazidi kutafuta mashamba mengine akapanda mikarafuu. Lakini fidia aliyopewa ni ndogo sana mpaka kafa kihoro. Kwa hivyo, sheria hii imekuja kumkomboa mkulima wa karafuu ili aweze kilipwa fidia ambayo inastahiki. Mkarafuu mmoja kila msimu unampa mtu laki mbili au tatu, leo unampa elfu ishirini hawezi kupata hata msimu mmoja wa karafuu.

Kwa hivyo, Waziri wa Biashara atatangaza bei ya mikarafuu kila baada ya muda ili mkulima wa karafuu apate fidia inayolipia hadhi ya mkarafuu wake. Kwa hivyo, sheria hii imekuja kukukomboa mkulima wa karafuu na imekuja kuupa hadhi hasa mkarafuu wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, imependekezwa kutumiwe kwa mbinu za kisasa katika uchumaji wa karafuu. Wizara imeona kwamba kuna haja ya kufanya utafiti juu ya pendelezo la suala hili. Kwa sababu mpaka sasa hivi dunia nzima hakuna njia ya kuchuma karafuu isipokuwa watu wanapanda juu ya mikarafuu. Kuna nchi nyengine kwenye ile mikarafuu mikubwa, yanajifunga kamba nyuma huku kama wanapanda miti ile katika maguzo ya taa.

Kwa hivyo, hiyo ni njia moja ambayo mtu akijifunga *belt* nyuma pale akachuma karafuu akianguka atakuwa ananing'inia hafiki chini. Lakini tunataka kufanya uchunguzi wa kina namna gani utafiti ufanywe ili tupunguze ajali katika mikarafuu.

Vile vile, kuna utafiti sasa unafanywa utafiti huo wa moshi unafukizwa katika mkarafuu, karafuu zote zinapukutika chini zimeshachambuliwa. Lakini makonyo utayakosa na vile vile, mkarafuu kwa sababu vile vikonyo havikukatwa mpaka kupukutika unachelewa kuzalisha karafuu.

Kwa hivyo, kuna changamoto nyingi katika utafiti huu, tupeni muda utafiti utafanywa kuonekana namna gani ya kuweza kupunguza vifo au kuumia kwa wananchi wanaopanda katika mikarafuu.

Mhe. Naibu Spika, kuna upatikanaji wa vifaa, imeelezwa kwamba sheria iweke mazingira kwa mamlaka ya upatikanaji wa vifaa husika vya kuanikia karafuu, vya kupimia karafuu na mambo mengine. Wizara imekubaliana na pendekezo hilo na inapendekeza kuwepo kifungu kidogo cha 13 (3) ambacho kitaitaka mamlaka husika kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo.

Mhe. Naibu Spika, imependekezwa kwamba suala la uhifadhi wa karafuu liwekewe muda maalumu kwa kuwa kutakuwa na wakulima wanaoendelea kuchuma karafuu. Suala hili litafafanuliwa katika kanuni zetu. Katika kifungu cha 19 (5) kimeeleza kwamba Waziri atatengeneza kanuni. Kwa hivyo katika kanuni itafafanua wazi ni muda gani ambapo mkulima ataweza kuhifadhi karafuu zake katika nyumba yake. Na ni kiasi gani, kilo ngapi mkulima ataziweka katika nyumba yake.

Lakini sisi *ZSTC* tumetoa nafasi wazi kabisa mtu yeyote ambaye ana karafuu zake na hataki kuziuza, basi azipeleke *ZSTC* atahifadhiwa kule, atawekewa kule karafuu zake hazitoharibika, na siku yoyote atakayotaka kuuza atauza kwa bei iliyopo bila ya kuingiliwa. Sasa nasema kwamba suala hili sio geni, suala hili ukiangalia katika ripoti hii hapa ya *CGA* ya mwaka 1955 inasema hivi: "Wakulima wa karafuu wamehifadhi karafuu zao katika mwaka 1953 na 1954, na wameweza kuweka katika maghala karafuu zinafika farasia 300,000, ili mwenyewe anapotaka kwenda kutoa pesa anakwenda kutoa wakati wowote. Na pesa iliyopo wakati ule ratili mia shilingi mia mbili. Hii ni ripoti ya *CGA* ya mwaka 1955. Kwa hivyo suala la kwamba una karafuu zako unataka kuzihifadhi, kazihifadhi *ZSTC* watakuhifadhia na watakulipa wakati wowote unaotaka pesa zako kwa bei ambayo mmeafikiana, lakini kuweka karafuu katika majumba si jambo la busara.

Kweli ni mila zetu ndio, miaka 50 nyuma ilikuwa hakuna wizi wa silaha hapa, miaka hamsini, mia hakuna aliyekuwa akitia *grill* katika nyumba yake. Hata hivi juzi kila mtu hatii kufuli katika nyumba yake. Leo kumeingia wizi wa nguvu wa kutumia silaha za moto, na karafuu ni mali unaiweka ndani ya nyumba yako unahatarisha maisha yako na familia yako, na unawapa kazi polisi zaidi na zaidi. Njia nyepesi hutaki kuuza karafuu zako ziweke *ZSTC* wakati wowote unataka kuuza kilo 5, kilo 10 kachukue fedha zako utumie. Kwa nini ujitafutie mauti. Isitoshe karafuu zile katika nyumba nyingi zinaharibika kwa sababu haziwekwi katika makaazi mazuri, zipo pale zinavujiwa, zinapata unyevu. Na karafuu zile vile vile kuna *shrinkage*, suala la *shrinkage* ni muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, karafuu unapoiweka ina-*shrink*, ukiweka *ZSTC* karafuu imeshapimwa iki-*shrink* wewe hupati hasara. Karafuu mwezi mmoja ina-*shrink* 0.1, karafuu miezi miwili ina-*shrink* 0.5, mpaka ikifika miezi mitatu karafu imesha-*shrink* 1%. Kwa hivyo wewe karafuu yako ukiiweka *ZSTC* utakuwa hupati hasara ya *shrinkage*. Kwa hivyo tunawashawishi wananchi wote karafuu zenu msiweke nyumbani ni hatari kwa maisha yenu na kwa taifa. Kwa hivyo karafuu zako zipeleke *ZSTC* ziweke pesa zako zipo hazipotei.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 19 (1) kinaeleza kuhamisha karafuu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine. Utaratibu wake ulioelezwa katika kanuni kwa mujibu wa kifungu cha 19 (5) uhamishaji wa karafuu kutoka sehemu moja kwenda nyengine itatungwa kanuni ambayo itaeleza wazi ni masafa gani, na ni wapi na wapi, na ni nani ataruhusiwa kuhamisha karafuu. Watu wote wenye karafuu watakuwa *registered*. Kwa hivyo mtu yeyote atakayehamisha karafuu kutoka hapa na hapa atakuwa na namba yake ya *registration*, atakuwa na kibali chake na hakutakuwa na mizozo ya aina yoyote. Kwa hivyo hili lisiwashtue, sheria hii imekuja kuweka wazi, ile ya mwanzo iliyopita tunaifuta ilikuwa ina matatizo. Na kabla ya kutunga sheria hii mimi mwenyewe binafsi nimekaa na wakulima Wete, pamoja na wakulima wote wa Kaskazini walikuja tukazungumza pale siku nzima kwenye semina wakaleta mawazo yao tukabadilishana mawazo. Siku ya pili nilikwenda Chake Chake wakaja wa Mkoani na Chake Chake tukakaa tukazungumza. Kwa hivyo masuala haya wakulima wote wameyaridhia, tumezungumza, tumeyazingatia na tumewafahamisha wameelewa.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wengi wametofautiana kuhusiana na suala la adhabu; wengine wanasema kuwa adhabu hii ni kubwa, na wengine wanasema adhabu hii ni ndogo. Adhabu iliyomo katika kifungu cha 26 ni kwa ajili ya makosa madogo madogo ya kiutendaji kama ilivyowekwa katika kifungu hicho. Na adhabu nyengine iliyowekwa katika kifungu cha 13 (5) ni

kwa ajili ya ulinzi wa mikarafuu. Kwa hivyo naomba Waheshimiwa tukubaliane kwamba adhabu hii ni ya kiasi, hata sisi tumeweka adhabu kubwa zaidi ya hii lakini Kamati ilipunguza. Sasa tukipunguza na hili ile thamani ya mikarafuu na ile hadhi ya karafuu itashuka zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ajali ya kuanguka mkarafuu. Mhe. Naibu Spika, imeelezwa kwamba sheria haikuweka wazi utaratibu utakaotumika katika kumhudumia mtu aliyeanguka mkarafuu. Utaratibu huo utazingatiwa katika kanuni zitakazotungwa kwa mujibu wa kifungu cha 30. Itazingatia utoaji wa kipaumbele kwa walioanguka mkarafuu, kuondoa urasimu na kuhakikisha utolewaji wa huduma kwa wahanga wa zao hili. Aidha, kwa niaba ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko natoa pole kwa familia ya wale wote ambao walichuma karafuu, walifariki au wengine wamepata majeraha au kupata ulemavu. Poleni sana lakini sheria hii itakuwa ni mkombozi kwa wale wote watakaoathirika katika uchumaji wa zao la karafuu.

Tafsiri ya Ofisa wa Umma. Mhe. Naibu Spika, imeelezwa kwamba katika tafsiri ya neno Ofisa wa Umma iondolewe maneno ya Sheha na Diwani. Wizara inakubaliana na pendekezo la kumuondoa Diwani na Sheha, ila Sheha abakie kwa umuhimu wake wa kuwa na ngazi ya mwanzo ya utawala wa Serikali. Na kwa vyovyote vile wakati wa kupata *search warrant* Sheha lazima awepo katika ku-*search.*

Namba 23 uwiano wa kifungu cha 5 (1) (i), 12 (3) (a), 10 (1) na 10 (3). Mhe. Naibu Spika, imeelezwa kwamba kuna haja ya kuwa na uwiano katika vifungu hivyo. Wizara inakubaliana na hoja hizo na marekebisho hayo.

Mhe. Naibu Spika, imeelezwa kwamba tuongeze usarifu wa karafuu katika mpango wa maendeleo ya karafuu. Wizara inakubaliana na hoja hiyo moja kwa moja.

Taasisi ya Ardhi. Mhe. Naibu Spika, imeelezwa kwamba katika mswada huu tafsiri ya Taasisi ya Ardhi imekosekana. Wizara inapendekeza kutumika neno Waziri anayehusikana na Ardhi badala ya neno Taasisi ya Ardhi. Kwa sababu kuna taasisi mbali mbali zinazohusiana na mashamba ya mikarafuu. Kwa hivyo Waziri wa Biashara atashauriana na Waziri anayehusika na Ardhi ili kutangaza eneo la shamba la mikarafuu.

Ufafanuzi wa sheria zinazomueleza Mkaguzi. Mhe. Naibu Spika, imeelezwa kwamba maneno sheria zilizopo hayapo wazi. Ufafanuzi ni kwamba Wakaguzi hawa wanatarajiwa kutoka katika taasisi tofauti ambao tumewachagua kwa mujibu wa sheria zao. Kwa mfano kuna Ofisa wa Misitu amechaguliwa kutokana na Sheria ya Misitu. Kuna Ofisa wa Kilimo

amechaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kilimo. Kwa hivyo sheria hii inawakubali wale maofisa ambao wamechaguliwa kutoka katika wizara zao au taasisi zao kwa mujibu wa sheria zao.

Wakaguzi kuwa na uwezo wa kuchukua nyaraka. Mhe. Naibu Spika, imeelezwa kwamba uchukuaji wa nyaraka katika kifungu cha 17 (c) unaweza kutumika vibaya. Hivyo basi, ni kweli tumeona jambo hilo litaathiri. Kwa hivyo tunasema Wizara inapendekeza kifungu hicho kisomeke kuchukua nakala ya nyaraka na si nyaraka yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, imependekezwa kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar itajwe katika sheria hii. Wizara inaona si busara kutajwa benki hiyo katika sheria kwa vile tupo katika ushindani wa kibiashara. Na hii Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Wizara hii inashajihisha kuwepo na biashara ya ushindani, pia inajishajihisha kuwepo na *fair trade competition.* Hatuwezi kuitia *PBZ* kuwa iwe peke yake, itakuwa Wizara hii inakwenda kinyume na maadili ya kibiashara, tutakuwa tunafanya *unfair trade competition.* Kwa hivyo Wizara ya Biashara inashauri kwamba bado katika Zanzibar kuna benki 12, benki ambayo kama itaingia katika ushindani itashinda itapewa nafasi ya kufanya kazi hii. Kwa hivyo tunapendekeza bado tupate fursa bodi ichague benki itakayokuwa muafaka kwa kazi hii.

Bodi kuendesha matumizi ya mfuko. Mhe. Naibu Spika, imeeleza kwamba kazi za mfuko zimekwishaelezwa wazi katika sheria hii, hivyo hakuna haja kwa bodi kupewa jukumu la kuendesha matumizi. Imependekeza kwamba maneno kama itakavyoidhinishwa na bodi yaondolewe. Basi Wizara inakubaliana na pendekezo hili la kuondoa maneno haya kama itakavyoidhinishwa na bodi.

Masharti ya ukopaji na vivutio. Mhe. Naibu Spika, wajibu wa masharti ya ukopaji na vivutio yawepo wazi katika sheria. Kifungu cha 21 na 30 (2) (ii) vinatoa uwezo wa kuweka vigezo na taratibu za ukopaji na utoaji wa vivutio. Vigezo vya masharti hayo yatazingatia uwazi katika utekekezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, katika ukaguzi wa hesabu za mfuko. Imependekezwa kwamba hesabu za mfuko zikaguliwe na mkaguzi wa nje. Wizara haina pingamizi na suala hili, lakini kwa mujibu wa sheria mkaguzi wa nje hawezi kukagua hesabu za Serikali bila ya idhini ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo sisi hatuna pingamizi *provided* Mkaguzi Mkuu wa Serikali atatoa kibali hicho.

Bodi itakayosimamia mfuko. Mhe. Naibu Spika, imeulizwa kuhusiana na kuwepo kwa Mjumbe wa Kilimo katika Bodi inayosimamia Mfuko.

Namhakikishia dada yangu Mhe. Asha Bakari Makame kwamba katika Bodi inayosimamia Mfuko inajumuisha Mjumbe mmoja kutoka Wizara ya Kilimo. Huyu hatoki yupo *constant* kabisa.

Ukiangalia katika bodi ya zamani ya *CGA* kulikuwa na *Director of Agriculture*. Kwa hivyo na sisi bahati nzuri tumempata Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo yumo katika Bodi ya *ZSTC.*

Mpango wa Maendeleo ya Karafuu. Mhe. Naibu Spika, imetakiwa kutoa ufafanuzi wa kazi zilizopo katika kifungu cha 12 kuwa zinahusiana na kilimo. Huo ni mpango ambao umetayarishwa na bodi na utekelezaji wake utajumuisha wadau wengi wakiwemo Wizara ya Kilimo.

Kumetokea wasiwasi hapa baadhi ya Wajumbe wameona mbona Wizara ya Biashara imeanza kupora kazi za Wizara ya Kilimo? Hapana. Ukiangalia katika ripoti ya *CGA* ya mwaka 1955 hii hapa, *CGA* ilikuwa ikisaidia, kwa mfano katika mwaka 1954 imetoa shilingi laki mbili ili kutengeneza njia zinazokwenda katika mashamba ya mikarafuu. *CGA* imetoa pesa katika bajeti yake ya mwaka 1954/55 164,000/= katika kuvisha vitalu vya mikarafuu na kusambaza miche ya mikarafuu. Kwa hivyo tangu *CGA* ilikuwa ikishirikiana na taasisi mbali mbali kusaidiana ili kuweza kuboresha zao la karafuu. Zao la karafuu kwa muda mrefu halina mwenyewe. Nasikia siku moja *AG* alisema zao la karafuu limekuwa kama mtoto wa mwanaharamu, kumradhi. Siku ya ndoa anakuja Kadhi kuja kumuozesha, Kadhi yule hajui kamlea nani mtoto yule, kalelewa wapi, kwa kiasi gani, kwa kipindi gani, lakini yeye siku hiyo anakuwa kinara kumuozesha mtoto yule.

Sasa karafuu huko inalimwa, inachumwa, lakini *ZSTC* yeye anakuwa Kadhi, siku ya kuja kununua karafuu ananunua tu hajui inakotoka, wala hajui ilivyoendelezwa. Karafuu ni zao la biashara, kwa hivyo ni lazima lifanyiwe kila hila. Na limetangazwa rasmi kuwa ni zao la biashara, kwa hivyo Wizara ya Biashara kupitia *ZSTC* na mfuko huu lazima itunze zao hili kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kwa hivyo sisi Wizara ya Kilimo hatukuipora, sisi tukasaidiana na Wizara ya Kilimo kuona kwamba zao hili linaimarika zaidi na zaidi. Kwa hivyo mfuko huu kazi yake ni kusaidia tu Wizara ya Kilimo. Wizara ya Kilimo majukumu yake yapo pale pale hayajaondoshwa, ishughulikie masuala mazima ya kilimo cha mikarafuu. Na sisi kama mfano tulivyosema mwaka jana Wizara ya Kilimo imenunua miche ya mikarafuu kutoka kwa watu binafsi wenye vitalu, *ZSTC* imelipia karibu shilingi milioni 75 kwa wale wenye vitalu na itaendelea kusaidia kulipia vitalu. *ZSTC* imesaidia zaidi ya vitalu 30, wamepata ma-*sim tank*, ma-*wheel barrow*, mifuko ya *plastic*, mapauro na mipira ya maji. Tutaendelea kuwasaidia vitalu vya watu binafsi waweze kuimarisha upandaji wa mikarafuu. Kwa hivyo sisi

hatuna nia ya kupora mamlaka au kazi za Wizara ya Kilimo, lakini tutasaidia Wizara ya Kilimo ili kuona kwamba upandaji wa mikarafuu unaimarika zaidi na zaidi. Na lengo letu la muda wa miaka 10 ni kuona kwamba karafuu zinarudi hadhi yake.

Ukiangalia katika ripoti hii hapa ya *CGA* karafuu katika mwaka 1953/54 ilifika tani 20,000 na *graph* hili hapa. Kwa hivyo sisi sasa hivi tunatoa tani 4,000 au 5,000 kutoka tani 20,000 ya mwaka 1951/52, 1953/54. Kwa hivyo ipo haja ya kuona kwamba tunaongeza angalau tutafika tani 10,000 *by* miaka 10 kuanzia hivi sasa.

Ugonjwa wa mikarafuu. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe walieleza kuhusiana na kuwepo kwa ugonjwa wa mikarafuu wa *sudden death* na *die back.* Maradhi hayo yamedhibitiwa kwa kiasi kikubwa na tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie yasitokezee maradhi kama hayo au maradhi mengine ya mikarafuu. Hata hivyo, tafiti kuhusu maradhi ya mikarafuu na njia ya kukabiliana nazo na hata mabadiliko ya tabia nchi zitaendelea kufanywa kama ilivyobainishwa katika waraka huu.

Vituo vya karafuu. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri ameeleza vizuri sana habari ya vituo vya karafuu vilivyojengwa na vilivyokarabatiwa.

Mbegu mpya za mikarafuu. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wamependekeza kupatikana kwa mbegu mpya zinazoendana na mabadiliko ya tabia nchi, Serikali italifanyia kazi suala hili. Kuna wengine wameuliza hivi hapa kuna karafuu mbegu ngapi? Karafuu ni mbegu moja tu iliyopo sasa hivi, lakini tunachelea baadae wavumbuzi wanaweza wakavumbua mbegu nyengine na nyengine, ndio maana tukatia katika sheria hii kwamba hata mvumbuzi kama kishavumbua mbegu yake lazima kwanza ifanyiwe utafiti na ipatiwe kibali ndio itumike isije ikaharibu mazingira au ikaharibu mazao yenyewe yakawa mazao ya karafuu mbadala.

Njia mbadala ya uanikaji wa karafuu. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wamependekeza kuangalia uwezekano wa kukausha karafuu kwa kutumia mbinu mbadala hasa wakati wa mvua. Suala hili linahitaji utafiti mkubwa ili tusije kuiondoshea hadhi karafuu yetu. Hadi sasa njia bora inayokubalika na kutumiwa na nchi zote zinazolima karafuu ni uanikaji wa karafuu kwa njia ya jua na kwa kutumia majamvi.

Mhe. Naibu Spika, bado tafiti nyingi zitafanywa. Katika ripoti hii ya *CGA* mwaka 1953/54 mpaka 55 Kizimbani kulijengwa majokofu ya kukaushia karafuu ambayo hayakufanikisha suala hili. Kwa hivyo utakuta mambo haya ya utafiti wa kukausha karafuu hayakuanza leo, tangu miaka ya 50

imeshafanywa na *CGA.* Na *CGA* katika bajeti yao inaonesha walitumia pesa nyingi sana katika utafiti wa kukausha karafuu kwa kutumia majokofu hayo lakini kwa bahati mbaya hawakubahatika.

Katika *new policy* hizo ambayo ilifanywa Kizimbani. *Experimental extension as known to the hot air dryer for drying cloves artificially* na kwa kutumia betri hawakufanikiwa. Na Indonesia huko vile vile walifanya utafiti karafuu zikatoka nyeusi, hakuna mnunuzi wa karafuu nyeusi, kwa sababu karafuu za Zanzibar zina rangi ya dhahabu, ndio maana zikaitwa karafuu za dhahabu. Unapozitia katika jokofu zikawa karafuu nyeusi zitapoteza hadhi yake ya kuwa karafuu dhahabu. Njia mbadala ya kuanika karafuu mpaka sasa hivi hakuna lakini utafiti utafanywa. Mpaka sasa hivi tuanikeni karafuu kwa kutumia majamvi na sio mabati wala barabara za lami wala njia nyengine yoyote. Njia nzuri karafuu zianikwe kwa majamvi ili zisije zikaharibika.

Naona wengi hapa walikuwa wanasema karafuu zitaharibikaje? Karafuu zitaharibika, karafuu zikinyeshewa na mvua zitakosa *grade* tu, baada ya kuuza *first grade,* utauza *second grade, third grade* au mpeta, lakini bado haijaharibika. *ZSTC* inanunua *first grade, second grade, third grade,* inanunua mpaka mpeta. Karafuu inaharibika pindipo watu wanazikaanga kwa mafuta halafu asubuhi anazifuta mafuta anakuja kuziuza, zile zimeshaharibika. Karafuu anazichukua anakwenda kuzitia katika bahari ya maji chumvi mpaka zinaroana. Umeshazitia chumvi zimeshaharibika hizo. Karafuu hizi hizi sisi tunazichukua hapa tunazi-*pack* tunawapelekea wenzetu wanakula, wanafanya *tea masala,* wanafanya *curry powder,* wanafanya sigireti. Ukishazitia uchafu karafuu wa aina hiyo au makemikali hazifai tena kwa kazi hizo. Kwa hivyo lazima karafuu zitunzwe zisiharibiwe. Karafuu wanazitia vinyesi unadhani hazijaharibika mimi sikubali hivyo. Karafuu inaharibiwa inatiwa vinyesi haifai, inatiwa kemikali haifai, inakaangwa haifai. Karafuu ikipata mvua itashuka *grade* kutoka *grade 1,* kuja *grade 2,* kuja *grade 3,* lakini bado haijaharibika. Karafuu kuharibika inaghushiwa, inachakachuliwa hapo imeshaharibika na haifai katika soko wala haifai kutumika katika matumizi ya binadamu.

Usimamizi wa mfuko. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wanataka kujua Mkurugenzi Mtendaji atasimamia vipi mfuko. Bodi itaanzisha Idara Maalumu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mfuko kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 9 cha sheria hii.

Jengine *ZSTC* kutumia sheria za mfuko. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wamehoji matumizi ya kifungu cha 5 kuhusiana na usaidizi wa shirika wakati bei ya karafuu itakaposhuka katika soko la dunia. Usaidizi huu kwa shirika utasaidia pia kutupunguzia bei wakati bei yenyewe itakapoanguka.

Hii Mhe. Naibu Spika, haiji kusaidia shirika, inakuja kuwasaidia wakulima wa karafuu. Pindipo bei ya karafuu itakapotangazwa, bei imeshatangazwa kwa kipindi hichi cha vuli au cha mwaka, bei ya karafuu itakuwa kilo moja *first grade* 14,000/=. Kwa bahati mbaya bei ile imeshuka lazima mfuko usaidie mkulima asije akapata hasara. Kwa sababu mkulima au mtu amekodi karafuu kwa bei ile, anajitayarisha gharama kwa bei ile, halafu mkishusha bei atakufa mtu kihoro. Kwa hivyo lazima kwa kipindi kile tuweze kumhifadhi ili bei ya karafuu isishuke, lakini mfuko ndio utakaoweza kuchukua suala hilo.

Mamlaka ya Sheha kutoa vibali. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe walihoji sababu ya Sheha kupewa mamlaka ya kutoa vibali peke yake bila ya kuingiza maofisa wengine wa umma kwa mujibu wa sheria hii. Utaratibu wa kutoa vibali umewekwa kwa Sheha kwa sababu ndio ngazi ya mwanzo ya Serikali ambapo wakulima na wananchi wengine wanaeleweka katika Shehia na Sheha ndio kiongozi wa Serikali katika ngazi hiyo. Vile vile tutataka tumpate mtu mmoja tu ambaye atawajibika kufanya kazi hii na atalaumika kufanya kazi hii. Wakiwa watu wengi ndio wanaotoa vibali basi hapa hapana wa kumuwajibisha, hapana wa kumlaumu, kila mtu atatoa kibali na hatimaye tutaona mambo yanaharibika. Kwa hivyo tunamwachia Sheha wa Shehia atakuwa *responsible* wa suala hili na akiharibu tutamdhibiti Sheha na si watu wote.

Uchimbaji wa mawe. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wametaka uchimbaji wa mawe uruhusiwe katika mashamba ya mikarafuu. Suala la uchimbaji wa mawe Mhe. Naibu Spika, katika Sheria ya Misitu limekatazwa kabisa, hakuna kuchimba mawe katika mashamba. Kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 32 cha sheria namba 10 ya mwaka 1996 ambayo inahusiana na uhifadhi wa misitu, Baraza hili tukufu iliipitisha hairuhusiwi mtu kwenda kuchimba mawe. Sisi tumesema katika mashamba ya mikarafuu, hata katika mashamba mengine hairuhusiwi kuchimba mawe, ukichimba mawe mikarafuu itaanguka, ikianguka umeshafanya uhalifu mkubwa. Hatuwezi kuruhusu watu kwenda kuchimba mchanga, mawe katika mashamba ya mikarafuu, mikarafuu itang'oka, upepo ukija haina kizuizi itaanguka, na kwa hivyo itakuwa hatukuhifadhi mikarafuu kama tulivyoahidi.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe walihoji matumizi ya vifaa vinavyothibitishwa. Hivyo Wizara imependekeza kutumika vifaa vilivyokubalika. Hii *stage* ya kuweka vifaa vilivyothibitishwa tunafuta sasa tunaweka vifaa vilivyokubalika ili mtu asisumbuke. Tumesema tunataka jamvi, tunataka pishi, tunataka gunia, kwa hivyo atajua kama gunia hili na jamvi hili na pishi hii ndio inakubalika.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe walitaka kujua karafuu kuna aina gani. Nimeshajibu kuna aina moja tu.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe walitaka kujua utaratibu utakaotumika katika mkarafuu mkavu. Mtu atakayekata mkarafuu mkavu atatakiwa kuomba kibali kwa Waziri, na utaratibu wake utafanyiwa katika kanuni za sheria hii itakapotungwa. Kutokana na kanuni jamani, tusione tabu kuja kuomba kibali kwa Waziri. Tumetaka kuupa hadhi mkarafuu, tumetaka mkarafuu uwe na hadhi kubwa, mkarafuu mtu atakayeukata atalipa fedha za kutosha. Sasa unaposema kama mkarafuu huu kila mtu akate tu haiwezekani, mkarafuu ukitaka kuukata ukiwa umekauka lazima Waziri ahakikishe mkarafuu umekauka na kwa nini ukakauka. Pengine mkarafuu huu umeukausha wewe haujakauka, lazima tuthibitishe kwanza huu mkarafuu umekaukaje, umeukausha kwa kupiga tewe, umeutia mafuta ya taa, vipi mkarafuu umekauka. Mkarafuu lazima upewe hadhi, sio karafuu tu. Kwa hivyo mambo ya kukatakata mikarafuu matawi, kukatakata vigogo, kukatakata miche hakuna ruhusa, omba ruhusa kwa Waziri.

Ubinafsishwaji wa karafuu. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wametaka kujua kwa nini Serikali inaendelea kudhibiti biashara ya karafuu. Hili ni zao la taifa jamani, na huko nyuma Serikali imewahi kubinafsisha mazao mengi ambayo hatimaye yamepotea. Tulikuwa na pilipili hoho, mwani, mbata na vyenginevyo vyote vimebinafsishwa, viko wapi, vimekufa. Kwa hivyo kwa kauli ya mwenyewe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba karafuu haitobinafsishwa na karafuu zitakuwa ni zao la biashara la taifa. Kama zile nchi nyengine zenye mafuta hawasemi mafuta sasa hivi tunabinafsisha kwa sababu gani, mafuta ndio zao lao la taifa hapana kubinafsisha. Kwa hivyo ubinafsishwaji wa karafuu hakuna suala hili bado. Serikali itaimarisha zao hili la taifa, serikali itadhibiti zao hili la taifa kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar, si kwa ajili ya mtu mwengine yeyote. Hili ni zao la taifa, si zao lako.

Miundombinu katika sehemu za mikarafuu. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wamependekeza kwenye miundombinu hasa katika barabara zinazoelekea kwenye maeneo ya karafuu. Kifungu cha 5 (d) cha mswada huu kinatoa maelekezo ya kutosha kuhusu suala hili, lakini vile vile nataka kumtoa wasiwasi Mwakilishi ambaye ametetea sana Ngomeni.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais alifanya ziara Pemba katika mwezi wa Novemba. Na katika ziara ile Naibu Waziri wangu alikuwa naye Mhe. Rais. Mimi nilikuwa nje ya nchi, lakini kufika tu Mhe. Rais akasema namtaka Waziri wa Biashara aje Pemba, na mimi nikaruka nikaenda Pemba jioni. Usiku saa mbili tuko kwa Mhe. Rais.

Mhe. Rais akaniuliza, anasema karafuu zipo nyingi huku barabara mbovu mutafanya nini? Mimi Waziri wa Biashara, Naibu Waziri yupo na watendaji wangu na huku kuna Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na watu wake; Rais anataka kujua barabara ya Kipapo Mgelema, Kiuyu Ngomeni, Mgagadu Msengele, karafuu ni nyingi barabara ni mbovu.

Ndio tukasema lazima barabara hizi zitengenezwe na sisi *ZSTC* itachangia kwa mujibu wa uwezo wake barabara zitengenezwe. Kwa hivyo ninakuhakikishia Mhe. Mwakilishi Ngomeni ni amri ya Rais. Kwa hivyo kila penye karafuu Mhe. Rais ambapo njia mbovu anajua na mwenyewe anafuatilia suala hili. Kwa hivyo sharti mujue kwamba hii dhana ya taifa na mwenyewe Mhe. Rais anashughulikia ipasavyo. (*Makofi*).

Brand za karafuu. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wamependekeza kuzingatia suala la ubora kwenye suala zima la maendeleo ya karafuu. Wizara inakubaliana moja kwa moja na suala hili. Mhe. Suleiman Hemed Khamis, amesema kwamba sheria hii hasa imekuja kwa sababu ya *brand* ya karafuu na mimi ninakubaliana moja kwa moja kwamba Mhe. Suleiman amefahamu barabara sheria hii.

Sisi tunataka ku-*brand* karafuu. Tusihadaike, sasa hivi bei ya karafuu ni nzuri, kwa nini? Kwa sababu karafuu duniani ilikuwa katika mwaka 2003 zikizalishwa karafuu tani laki moja na hamsini na tano elfu. Wakati huo sisi Zanzibar hapa tunagaragara, karafuu hatuna wa kumuuzia kwa sababu karafuu zipo tani ishirini zaidi kuliko mahitaji ya soko.

Soko la karafuu duniani zinakuwa tani 130 lakini uzalishaji ni tani 155. Kwa hivyo kuna tani ishirini na tano za ziada. Karafuu sisi tutamuuzia nani, hakuna. Ndio ukaona karafuu hakuna wa kumuuzia zinagaragara hapa dola mia tano, sita hakuna anayezitaka.

Katika mwaka 2006 karafuu ilishuka kutoka tani laki hamsini na sita elfu ikawa tani elfu tisini na moja tu duniani. Kwa hivyo kukawa na *deficit* ya tani karibu elfu hamsini na tano hakuna. Ndio karafuu ikapanda bei. Sasa karafuu imepanda bei kwa sababu soko limekubali kwamba karafuu inayozalishwa bado haitoshelezi mahitaji ya matumizi au mahitaji.

Lakini mwishoni mwishoni hivi Madagascar wanafanya kazi ya kufanya karafuu ziwe nyingi na *quality* yao iwe kubwa. Comoro wanafanya kazi hiyo hiyo karafuu wazalishe nyingi na watoe high *quality* na India, Brazil na wengine popote duniani. Kwa hivyo katika kipindi cha miaka mitano sita

hapa karafuu itarudi vile vile itakuwa katika kima hicho hicho tani laki moja hamsini na sita. Kwa hivyo tunakuwa na matatizo hayo hayo.

Ili kuepukana na matatizo hayo lazima karafuu yetu iwe ya *first quality*. Ndio tunafanya *branding* na *branding* huwezi kuifanya wakati wa kuchambua karafuu kama anavyosema Mhe. Rufai Said Rufai pale, *branding* inaanza na:-

1. Kwenye mkarafuu wenyewe,
2. Uchumaji wenyewe,
3 Unyambuaji wenyewe,
4. Uanikaji wenyewe,
5. Uuzaji wenyewe,
6. Ufungaji wenyewe
7. Ku-*store* kwenyewe

Mambo saba hayo ndio uweze kufikia bei kubwa ili wakulima wetu wasije wakayumba. Tunataka ku-*brand* karafuu, tuki-*brand* karafuu tunai-*brand* Zanzibar, tuki-*brand* karafuu tunawa-*brand* Wazanzibari. Kwa hivyo suala la kupata karafuu ni mtambuka; wananchi wote, mwenye mkarafuu na asiyekuwa na mkarafuu tuulinde mkarafuu. Tuhakikishe kwamba karafuu zinatoka *first grade* inaitwa *premium grade*. Hatuwezi kufikia kiwango cha *premium grade* ikiwa leo Mwakilishi anakuja hapa anasema tukichambua tu, haiwezekani. Ni lazima tuanze tangu kupandisha mpaka kuchuma mpaka kufikia mwisho. Kwa hivyo naomba ndugu zangu Wawakilishi suala la *branding* karafuu linahitaji msaada wetu sisi Wawakilishi na tutakupeni semina nzuri ya *branding* ili mutusaidie ili karafuu ya Zanzibar iwe-*branded* na magendo yaondoke na karafuu iwe na hadhi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kurahisha maendeleo ya mfuko wa karafuu na sheria ya *ZSTC*. Wajumbe wamependekeza haja ya kuziunganisha sheria ya maendeleo ya karafuu na sheria ya *ZSTC* kutokana na umuhimu wa karafuu kuwa ni uchumi wa Zanzibar. Kuna haja ya kuwa na sheria ya maendeleo ya karafuu peke yake. Lilitoka swali hapa mbona hizi sheria zimekuwa mbili, kwa nini sheria hii isiunganishwe na sheria ya *ZSTC*. (*Makofi*).

Sheria hii tungeitia kwenye sheria ya *ZSTC* ingemezwa na wala karafuu isingepata maendeleo yake, lakini ili kuipa hadhi karafuu na mkarafuu na *branding*, tumeweka sheria yake peke yake isije ikazongwazongwa na sheria nyengine, isimamiwe vizuri, ifanye kazi vizuri.
Ninawaahidi Wawakilishi wote kwamba sheria hii pindipo mukiipitisha nyinyi hapa hivi leo na Rais akaitia saini haiendi kuwekwa katika madroo

hii, inakwenda kufanyiwa kazi, wala haiendei kunyiwa na mende, inakwenda kufanyiwa kazi. (*Makofi*).

Wananchi wote, Wawakilishi, Wazanzibari wote naomba mutuunge mkono juu ya suala la kuweka *branding* ya karafuu. Bado karafuu ni raslimali yetu, bado karafuu ni historia yetu, bado karafuu ni *heritage* yetu, tuithamini, tuipende, tuitukuze na Mwenyezi Mungu atatusaidia. (*Makofi*).

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya 1985 na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Yanayohusiana na Hayo

SEHEMU YA KWANZA

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Matumizi ya Sheria
Kifungu 3 Tafsiri Pamoja na Marekebisho Yake

SEHEMU YA PILI

Uanzishwaji Kazi na Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu Zanzibar

Kifungu 4 Kuanzishwa kwa Mfuko
Kifungu 5 Kazi za Mfuko Pamoja na Marekebisho Yake

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia nilimuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa kifungu cha 5 (j) kilichozungumzia kusaidia huduma za matibabu na huduma nyenginezo za bima kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu ilikuwa ni bima unajiunga mwanzo, wakati ukipata tatizo ndio ile bima itakusaidia ukapata malipo. Sasa hoja yangu hapa huyu aliyekwenda kuchuma karafuu leo na akapata ajali leo, hii bima kutakuwa na utaratibu gani. Nilimuomba Mhe. Waziri anifahamishe ili nijue bima hii itakuwaje.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salma na Mhe. Panya Ali Abdalla walichangia katika kifungu hiki.

Lakini ninataka nimfahamishe Mhe. Salma kwamba kwa mfano mimi ni mkandarasi kazi yangu ni kujenga unajua wewe. Mimi ninapochukua kazi, mimi ndio ninayechukua bima, kwa hivyo wafanyakazi wangu wakipata ajali bima ninayochukua mimi kwa ajili ya wafanyakazi wangu.

Kwa hivyo mfanyakazi akipata ajali bima inamkata yule mfanyakazi. Mimi dereva, wewe una gari yako, wewe ndio uchukue bima. Abiria yumo ndani ya gari yako kama umechukua bima kamili *full insurance*, gari ikipata ajali wale wote wanalipwa lakini uliyechukua bima ni wewe mwenye gari. Kwa hivyo mfuko huu ndio utakaochukua bima ya wadau watakaofanya kazi ya karafuu.

Kwa hivyo mfuko huu una dhima ya bima na hii tumeona India. India mpaka wakulima wa mpunga wote wamo katika bima; mpunga wao ukivia bima inawalipa. Kwa hivyo na sisi tunataka kuchukua mpango wa bima tumeshazungumza na bima zetu ili ikitokezea *any accident* bima itachukua mkondo wake na kila mwaka mfuko utalipia bima. Kwa hivyo usiwe na wasiwasi utakayejiunga si wewe, shirika au mfuko ndio utakaochukua bima kwa ajili ya wachumaji wa karafuuu wote wa Zanzibar.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa kweli nimemfahamu sana sasa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo tuendelee. Tunaendelea.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninamtaka Mhe. Waziri anipe ufafanuzi kuhusu suala hilo hilo la bima. Nilimuuliza kama kwa sababu anaweza akawa mtu ameshaanguka mkarafuu, pengine amevunjika miguu au wengine wamekufa. Nilitaka ufafanuzi kama tumefahamu vizuri ufafanuzi wake kama atakayeweka bima ni yule tajiri kwa ajili ya vibarua wake watakaokuja kuchuma karafuu.

Sasa nilitaka kujua hii bima itakuwa ni aina moja tu kwa wale wanaovunjika miguu na aliyekuwa amekufa. Sasa je, bima itakuwa ni ya aina moja ama kutakuwa na bima ya aina mbili.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, suala hili ambalo Mhe. Subeit ameliuliza naomba nilifahamishe zaidi.

Ukichukua bima kuna bima za aina mbali mbali lakini katika bima hizi, kuna *categories*, yaani kutakuwa sijui hata kwa Kiswahili itakuwa vipi. Kwa mfano ukivunjika mkono kuna kima cha mkono, umekatika kidole, kuna bima ya kidole, umevunjika mguu kuna bima ya mguu, umekatika kiuno hivyo hivyo lakini ukifa ni bima mbali.

Kwa hivyo bima zinatofautiana kutokana na athari yenyewe na bima ina-*cover* kwenye matibabu na kwenye fidia wakati huo huo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee nilikuwa ninataka ufafanuzi tu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia asububi nilizungumzia katika kuanzishwa kwa mfuko huu utawakomboa sana wananchi, lakini kabla ya kuanzishwa kwa mfuko huu huko nyuma kulikuwa na utaratibu gani kwa watu walioanguka mikarafuu na nikatoa mfano wa mtu aliyeanguka tarehe 14 Disemba, 2013. Nikamwambia Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe ufafanuzi wa kutosha ili tujue, kulikuwa na utaratibu gani huko nyuma.

Kama kulikuwa na utaratibu wanawezeshwa, kwa nini wasipate haki zao.
Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza ilikuwa wanaoanguka mkarafuu wote wanashughulikiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwenye miaka ya

nyuma. Baadae serikali ilijiondosha katika suala hili, kwa nini? kwa sababu za msingi.

Sababu ya kwanza karafuu wanaziuza Kenya, akianguka serikali imlipe. Hii haiwezekani. La pili kutokana na ubadhirifu mwengine sasa mtu anakuja *POP* wala hakuvunjika mguu, daktari anamtia *POP* na cheti chake anataka akalipwe, udanganyifu huo pia ulifanyika.

Jengine mtu kaanguka na *scooter* anaambiwa kaanguka na mkarafuu, aliyeanguka mnazi kaanguka mkarafuu. Kwa hivyo serikali ikashindwa kulipa. Kwa hivyo mwisho mimi nikakuta katika rekodi miaka ya nyuma huko kuna waathirika wanadai kiasi milioni 75 ambazo serikali imeshindwa kuzilipa kutokana na ubadhirifu na udanganyifu huo niliouhadithia.

Sasa bado ndio maana sisi tukatunga sheria hii ili mfuko huu uje uwasaidie watakaoathirika kikweli kweli hasa, na Kanuni zake tutazitunga hasa mtu akianguka tangu siku ya kwanza *process* gani itahitajika. Sasa mtu aliyeanguka mkarafuu mwaka jana au mwaka huu, sisi wizarani tunawasaidia kama binadamu tu, *ZSTC* inasaidia, wizara inasaidia na Waziri anasaidia; wengi tu nimeshawasaidia lakini hakuna sheria, hakuna masharti. Sheria hii kuanzia sasa hivi leo mukiipitisha na Rais akaitia saini atakayeanguka mkarafuu atayeathirika itachukua mkondo wake.

Kwa hivyo naomba haya nyuma tuyaweke upande kwanza tushughulikie haya. "*Yaliyopita si ndwele tugange yajayo*". Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba bado aniweke sawa kwa sababu anasema siku za nyuma kulikuwa na udanganyifu wa kutosha; mtu akianguka mnazi anasema kaanguka mkarafuu, wengine wakifunga *POP* wakisema wameanguka mkarafuu.

Je, sasa ni utaratibu gani unaotaka kuweka mpaka ukathibitisha kwamba mtu huyu kaanguka mkarafuu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ndio pale niliposema kwamba lazima tuweke buku la *registration*, tuwajue kwanza wadau wote wa mikarafuu tumewa-*register* na kila mtu ana namba yake. Akisema mimi nimeanguka mkarafuu kwa *registration* gani, wewe umekuwa *registered* au vipi, kama umekuwa *registered* wewe moja kwa moja una-*fly* kwenye ndege moja kwa moja mpaka Dar es Salaam au mpaka India kwa sababu umekuwa katika *register*.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee kama kutakuwa na *register* buku hilo na kama matajiri ndio watakaothibitisha kama kaanguka kwenye mkarafuu wangu. Tuendelee.

Kifungu 6	Uongozi wa Mfuko Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 7	Kuanzishwa kwa Kikosi Kazi
Kifungu 8	Uwezo wa Majukumu ya Bodi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 9	Usimamizi wa Mfuko

SEHEMU YA TATU

Usajili, Ulimaji, Ukaguzi na Uchumaji wa Karafuu

Kifungu 10	Usajili wa Wakulima wa Karafuu
Kifungu 11	Uimarishwaji wa Kilimo cha Karafuu Pamoja na Marekebisho Yake

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, jana wakati nilipokuwa ninachangia hapa nilijenga wasi wasi wangu kwamba huu mkarafuu umekuja karibu miaka mingi tu iliyopita, umekuja tangu karne ya 17. Na kwa kiasi kikubwa sasa hivi unaanza kupotea kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Na nikataka nipate maelezo ya kina ni kwa sababu gani ambazo zinazopelekea hadi sasa hivi serikali inakuwa ngumu katika kutuletea *variety* ambayo italingana na mabadiliko ya tabia ya nchi sambamba na kuimarisha huu mkongwe lakini iwe *variety* ambayo inalingana na mabadiliko ya tabia nchi.

Je, ni lini Mhe. Waziri kwa sababu mswada wa watafiti tumeshapitisha na wagunduzi wa mbegu mpya hapa za mimea. Sasa nataka unieleze ni lini tutatumia utafiti ule ambao tayari tumeshautungia sheria katika kuleta *variety* ya karafuu ambayo itakwenda sambamba na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na mazingira ambayo sasa hivi yamekuwa hasi sana kutokana na ongezeko la hewa ukaa jambo ambalo limeathiri sana mikarafuu hata majani hayawi mazuri, imekuwa imefanya mvi kama hivi mimi.

Kwa hivyo sasa ni lini mutaleta *varieties* mpya ili tuweze kuuendeleza mti wetu huu wa mkarafuu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Saleh Nassor Juma suala hili sio leo tu ya kwanza kila siku analisisitiza.

Katika sheria hii tumesema kwamba kuidhinisha aina tofauti za karafuu zitakazopandwa Zanzibar. Ndio maana tukasema kwani kuna aina ngapi. Sasa hivi kuna aina moja tu lakini sheria hii inaruhusu aina nyengine ikija itabidi tuifanyie *research,* tukiiona inafaa tuiruhusu, ndio sheria hii hapa.

Kwa hivyo sisi hatuna *complain*, pesa zipo katika mfuko wa kuweza kufanyia *research*, na watakaofanya *research* wote watasaidiwa alimuradi ikiwa karafuu hizo zitakuja kusaidia. Yupo mwenzako kasema hapa Mhe. Bi. Raya kuna karafuu zimefanywa *high breed* wiki mbili hazikauki na zikishakauka chapwa hazina ukali wowote.

Kwa hivyo ninasema suala hili sisi tupo tayari na fedha zitakuwepo katika mfuko za *research,* na sisi hatukatai kuja mbegu nyengine za mkarafuu, *provided* tutai- *prove* kwamba itakuwa haina uharibifu wa mazingira.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana kwamba sasa serikali imekubali kutuletea *variety* nyengine ya mkarafuu kama vile walivyokubali Wizara ya Kilimo kutupunguzia hii *East Africa Tall* na kutuletea minazi chotara ambayo hivi sasa tunakunywa madafu maji matamu sana.

Kwa hivyo sina budi kuungana naye mkono. Ninashukuru na tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa hata sina haja ya kusimama lakini ninaomba Mhe. Waziri anisaidie karafuu zetu kwa upande wa Zanzibar ni karafuu pekee ambayo katika ulimwengu mzima ndio karafuu halisi, *quality*.

Leo kama tutafanya utafiti kama tulete mikarafuu chotara, mimi hapo kwa kweli ninashindwa. Maana itabidi utafiti huo ili ufanyike na nini, ni karafuu chotara, tutakuwa ile *quality* tunaiondoa, hatutoweza kupata *quality* ambayo wenzetu huko hawana.

Kwa sababu kwanza tujue kwamba kwa Zanzibar *environment* yake ni tofauti, maana yake hapo Morogoro karafuu zipo, lakini ukiichukua karafuu ya Morogoro ukaileta hapa ni tofauti chapwa, Brazil, Indonesia.

Mhe. Mwenyekiti, ninasema haya tusije tukafanya mambo ya utashi halafu baadae tukajikuta kwamba karafuu yetu haina maana ili iweze kupotea. Mimi nilikuwa nilizungumze hilo Mhe. Waziri naomba unifahamishe. Maana mimi nitakuwa mgumu hivi sasa, kama kweli tutachukua hiyo hakimiliki ya mimea tutakwenda kuitia mambo karafuu yetu tuiharibu tulete chotara na hakuna karafuu chotara. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Asha Bakari Makame.

Ndio maana sheria hii ikasema mfuko utasaidia mamlaka inayohusika kwa kuidhinisha aina tofauti za karafuu zitakazopandwa Zanzibar. Kwa hivyo huu mfuko hautoidhinisha tu, hapana, unasaidia hiyo Wizara ya Kilimo, lakini haitoidhinisha hiyo karafuu ambayo kwetu sisi haitufai.

Bado karafuu ya Zanzibar ni muhimu sana kwa Zanzibar. Comoro wanaililia, Madagasca wanaililia, India wanaililia, sioni kama ipo haja hiyo, lakini haja ikija tutakuwa tunaiangalia, ikiwa haina maslahi ya Zanzibar, sheria hii haitoruhusu mbegu hiyo kutumika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru nimepata jawabu la kuniridhisha.

Kifungu 11	Uimarishaji wa Kilimo cha Karafuu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 12	Mpango wa Maendeleo ya Karafuu Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 13	Vitendo Vinavyokatazwa katika Kilimo cha Mikarafuu Pamoja na Marekebisho Yake

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kunipatia nafasi hii na kupiga buti hili kubwa kidogo.

Ninampongeza Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa kina na wa fasaha zaidi lakini nilipokuwa nikichangia katika kifungu hiki nilitoa maelezo kuhusiana na mkarafuu mkavu. Mhe. Waziri amesema kwamba mkarafuu mkavu lazima ipatikane ruhusa na kibali kutoka kwa Waziri. Hili Mhe. Mwenyekiti, ni tatizo kubwa kwa wakulima wetu wa mikarafuu.

Mhe. Waziri yupo Unguja, mkarafuu umekauka Ngomeni, Chambani, Pujini au kwengineko, utaratibu gani ambao utakaomfanya mkulima yule wa karafuu, mkarafuu ambao umekauka mpaka ampate Waziri ambaye yupo wizarani kwake hapa Unguja.

Namuomba Mhe. Waziri awape utaratibu mwepesi utakaowaondolea matatizo ya kusafiri na kwengineko ili wakulima hawa mkarafuu utakapokauka waukate katika utaratibu utakaokuwa rahisi kwao. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nimtoe wasiwasi Mhe. Mwakilishi.

Sisi sote tunajua kwamba mikarafuu inakufa ni lazima ife, kila kilichoumbwa kitakufa. Lakini binadamu tunamthamini sana, binadamu akifa katika mazingira yoyote yale ya kutatanisha anafanyiwa *post mortem* kwanza kuangaliwa sababu ya kifo chake. Sasa kwa hadhi ya mkarafuu tuliyoipa sasa hivi haiwezekani tu uende na shoka yako tu ukate mkarafuu.

Kanuni itatungwa namna gani ya kuja kuu-*state* mkarafuu wako na utakatwa na utakatwa kwa mpango gani na kwa matumizi gani. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi ukitaka kuanza kupunguza kasi ya sheria hii tayari unaukandamiza mkarafuu na hamsaidii mkulima.

Kwa kweli kama tunataka kuupa hadhi mkarafuu, tunataka kumnyanyua mkulima wa karafuu, mimi nimezungumza na wakulima wenyewe Chake Chake na Mkoani mpaka Wete, Konde huko, Micheweni hawana mikarafuu. Hawana tatizo na hili, taratibu zitapangwa wazi kabisa. Sio kwamba kila kitu atafanya wazi mwenyewe, hapana. Rais kanipa nafasi mimi waziri, mimi waziri nina katibu wangu, huko Pemba kuna Afisa Mdhamini wangu, nina wafanyakazi wangu maalum ambao watafanyakazi hiyo. Mimi nakuahidi ukipiga simu leo, kama mkarafuu wako umekauka basi asubuhi tumeshafika na tutaangalia, usiwe na wasi wasi kwa hilo, tuko hapa kwa kufanyakazi sio kuja kucheza, sasa unapotaka tupunguze makali ya sheria hii mikarafuu jamani itakwisha. Mikarafuu inakatwa sio mikavu tu mpaka mikarafuu mibichi itakatwa.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri, hofu yangu na wasi wasi wangu ilikuwa ni ule urasimu wa kwamba lazima apatikane waziri ndio kipatikane kibali hiki cha kukata mikarafuu. Naamini wakulima wa karafuu kwa mujibu wa karafuu ilivyo sasa basi wanauthamini mkarafuu kama ambavyo anauthamini Mhe. Waziri. Kwa hivyo, kwa kuwa kutakuwa kuna utaratibu mzuri zaidi utakaoekezwa katika kanuni basi naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 13 Vitendo vinavyokatazwa katika kilimo cha mikarafuu pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 14	Uwezo wa waziri kuitangaza sehemu ya ardhi kuwa ni ya kilimo cha mikarafuu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 15	Ubora wa usalama pamoja na marekebisho.
Kifungu 16	Sifa za mkaguzi.
Kifungu 17	Uwezo na majukumu ya wakaguzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 18	Msimu wa uchumaji wa karafuu pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaeleza niliyokusudia, naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake aliotoa, ambapo pamoja na kutingwa na shughuli fulani katika jimbo, lakini nilipokuwa nakuja nilifungua redio kwa makusudi ili kuhakikisha kwamba nayapata maelezo yake kadiri inavyowezekana.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu juu ya kifungu cha 19 nilieleza kwa kina kidogo, wasi wasi wangu juu ya kifungu cha 19(4) ambacho kinasomeka;

Kifungu cha 19(4)

"inakatazwa kwa mtu yeyote isipokuwa shirika kuhifadhi karafuu kavu ndani ya nyumba, ghala au sehemu nyengine yoyote".

Kwa hivyo, nilipendekeza kuwa kuna haja ya kukiangalia tena kifungu hiki kwa kutizama pia utamaduni wa watu wetu. Sasa Mhe. Waziri katika majibu yake alisema kwamba anaruhusu mtu akahifadhi karafuu zake *ZSTC,* ambapo kwa mara nyengine ni kama vile *ZSTC* itageuka kama ni benki ya karafuu za wakulima. Lakini kama nilivyosema jana Mhe. Mwenyekiti, kwamba pamoja na kuwa tunapitisha sheria hii, kuna haja vile vile ya kuzingatia mila na desturi za watu wetu, kwa sababu sheria nzuri ni ile ambayo pia inajikita kutizama watu wake.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka nimsikie Mhe. Waziri kuwa pamoja na kumkubalia kwa sehemu fulani ya pendekezo lake, kwa nini na yeye asiwakubalie wajumbe wa Baraza kuwa kukawekwa angalau kima fulani cha karafuu. Hii sheria ikataja *specific* kwamba kwa mfano pendekezo langu mimi ikatajwa kuwa karafuu zozote zinazozidi kilo 100 basi hizo zikahifadhiwe na *ZSTC*. Lakini kuanzia kilo 100 kuja chini angalau mkulima akaruhusika, na hoja yangu hii ni kwamba ukichukua kwa bei unayolipa sasa hivi, ingawa tunajua bei inaweza ikapanda au ikashuka. Ukichukua bei ya kilo moja Shs. 14,000, kwa kilo 100 ni kama Shs. 1,400,000. Kwa hivyo, kwa mkulima kuhifadhi karafuu ya thamani hiyo akaweka kama ni akiba

kwake, nadhani itakuwa kama ni hifadhi fulani ya maisha yake, kwa maana ya *security*.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hapa najua ni fundi kweli kweli, kawapiga na chini kila mjumbe aliyesimama hapa, lakini angalau katika hili nilikuwa naomba na yeye alikubalie Baraza hili, kwa sababu utaratibu wa kutunga sheria ni wa serikali kutoa mapendelezo na Baraza hili kutoa mchango wake. Katika hili nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri akubali kwamba angalau kwa kiwango hicho cha kilo 100 kuweza kuruhusiwa kuweka mwenyewe. Lakini zikizidi hapo kama anataka kuhifadhi basi atakwenda kuhifadhi katika maghala ya Mhe. Waziri kwenye *ZSTC*, namuomba sana Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki wamechangia wawakilishi wengi na wana wasi wasi. Mimi nataka niwatowe wasi wasi. Kifungu hiki ukiangalia chini hapa, tutafanya kanuni sisi ya masharti haya na hiyo kanuni itabadilika muda baada ya muda. Hatuwezi kutia kwamba mtu abakiwe na kilo mbili za matumizi ya nyumbani, hapana. Kanuni itaeleza na nyinyi mnaangalia padogo tu, lakini sisi tunaangalia pakubwa zaidi.

Sasa hivi tunashajihisha usarifu na wewe mwenyewe Mhe. Ismail Jussa umesema kwamba usarifu uingizwe katika sheria hii. Sasa usarifu huo itakuwaje, kutakuwa na viwanda hapa ambapo vitahitaji karafuu, viwanda hivyo sio lazima viwe na *store*, karafuu ziwekwe katika *store* zao. Kwa hivyo, kanuni itaweka wazi, kiwanda kitaruhusiwa kuweka karafuu tani ngapi na kwa mpango gani. Kila kiwanda kitapewa cheti kwamba kiwanda hiki matumizi yake kwa mwaka karafuu tani tatu, kwa hivyo, kitakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani tatu za karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, na mtu binafsi tunasema kwamba akiba yake ya nyumbani ni kilo 50, kwa matumizi ya nyumbani kilo mbili, lakini yote hayo unayatia katika kanuni hatutii katika sheria. Kwa hivyo, mimi nataka muniamini au mutuamini kwamba sisi hatukusudii sheria hii kuja kumkomoa mkulima wa karafuu, tunataka kumkomboa mkulima wa karafuu. Kwa hivyo, atapata fursa, itakuja kanuni itaweka wazi kila kitu na mtu hatokwenda kukamatwa na kilo 20 za karafuu akenda kufungwa miaka 3 au akatoa milioni 3. Vile vile mtu kuwa na kilo mbili ya kutumia kwa kupikia uji, kutengenezea dawa au kutengenezea singo ya kuwasinga mabiharusi, hapana. *(Makofi).*

Kwa matumizi yako binafsi, kwa mapenzi yako na mahaba yako unataka karafuu ndani ibakie mpaka iharibike basi utapewa kilo zako na mwenye kiwanda atapewa kilo zake, lakini kwa mujibu wa mahitaji ya kiwanda

chake. Kwa hivyo, naomba mtuamini kuwa kanuni itaweka wazi masuala haya. Hatuwezi kutia kilo 2, baada ya miaka 10 kuna kiwanda kinataka tani 20 lakini sheria hairuhusu mwisho kilo 50 na hiki ni kiwanda kinataka tani 20. Kwa hivyo, tuaminini ili tufanye kazi, ahsanteni. *(Makofi).*

Mhe. Ismaili Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sisi tunamuamini sana Mhe. Waziri na ninadhani hakuna waziri anayefurahia *confidence* ya wajumbe wa Baraza hili ambae anamshinda Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, mimi nafikiri hata na yeye analitambua hili. Kwa hivyo, sisi kimsingi tunamkubalia, lakini anayoyasema namuomba sana kaka yangu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui asiwe *regid.* Kuna maeneo lazima atukubalie chombo hiki. Mimi nimeipata *point* yake, lakini ninachomuomba ni kidogo tu na tukikubaliana hapo nafikiri tutaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, hayo aliyoyaeleza hivi sasa hayamo ndani ya sheria, kwa sababu kanuni ni kweli na kuna kifungu cha jumla kinachoelezea kuhusu kanuni, lakini kanuni haziwezi kuja kutungwa halafu zikenda kinyume na masharti ya sheria. Sasa mimi ningesoma hivyo alivyopendekeza yeye, basi kwa ufupi na atukubalie hapa na tuendelee Mhe. Mwenyekiti, kwamba hiki kijifungu cha 19(4) kisomeke kwamba;

Kijifungu cha 19(4)

"Isipokuwa kwa namna ambavyo itaelezwa ndani ya kanuni, halafu ndio iendelee, inakatazwa kwa mtu yeyote, isipokuwa shirika kuhifadhi karafuu....."

Sasa hapo itakuwa kweli imempa mamlaka ya yeye na kwa sababu *Hansard* itakuwa imeandika hii kwamba waziri kaji-*commit* ndani ya kanuni zake kwamba atalizingatia hilo. Kwa hivyo, hapo tutamuamini akafanye hiyo kazi. Kwa hivyo, mimi niko tayari kumkubalia, lakini akubali tuongeze maneno hayo, kwamba isipokuwa kwa utaratibu ambao utaelezwa ndani ya kanuni, halafu ndio iendelee hapo kuwa, inakatazwa kwa mtu yeyote, isipokuwa shirika kuhifadhi karafuu kavu ndani ya nyumba, ghala au sehemu nyengine yoyote. Akinikubalia hilo tutaendelea sasa hivi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, muafaka.

Mhe. Ismaili Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante tuendelee.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia katika kifungu cha 19(1) nilisema hapa uchumaji wa karafuu wa aina mbili. Kuna uchumaji wa karafuu wanaokwenda kuweka

kambi na kuna uchumaji wa karafuu wanaokwenda na kurudi. Sasa ndio nikasema hapa utaratibu uliowekwa ni mzuri wa kuhamisha karafuu kupeleka sehemu nyengine kwa utaratibu wa kutoa kibali. Lakini unapofika wakati wa msimu sisi kama wawakilishi wa wananchi tutapata tabu sana.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia mfano kama, zamani nakumbuka kama Kojani hakuna mkarafuu, lakini karafuu zilikuwa zinaanikwa Kojani, kutokana na matajiri waliokodi mikarafuu na vibarua wakitoka Kojani wakenda kuchuma na wakaichambua kwa tajiri.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, sheha amepewa mamlaka ya kutoa kibali, lakini wakati mwengine wanawasumbua wananchi kupata hicho kibali. Je, ni utaratibu gani mzuri kwa hao masheha ambao utawawekea mikakati kuweza kuwapatia wananchi kwenda kuhamisha karafuu mbichi na kwenda sehemu nyengine bila ya matatizo. Nilisema karafuu kavu unakata kibali kwa ajili ya kwenda kuuza na karafuu mbichi unakata kibali kwa ajili ya kwenda kuchambua sehemu ya kwenda na kurudi. Sasa Mhe. Waziri hapa atuweke sawa ili wananchi wanaochuma zao hilo kwa kuliokoa zao la kitaifa wasipate matatizo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mhe. Mjumbe kwamba karafuu mbichi mchumaji akichuma kutoka shamba, akenda kwa mwenye mali hakutaki kibali, sheria imeweka wazi kuwa mtu karafuu zake akishachuma anakwenda kwa tajiri kwenda kunyambua, halafu akapimiwa pale hapataki kibali.

Lakini anapotoka huyo mtu kutoka shehia moja na kwenda shehia nyengine. Kwa mfano katoka Mtukujuu kajakuanika karafuu kule kwako wapi, Kojani, anasema 'hapo chacha'. Kule Kojani mna mtindo nyinyi ndugu zangu wa Kojani, karafuu mnazitia ndani ya madebe yale ya manjano ya maji, kisha mkazitia kwenye vihori mnakwenda Mombasa na mkiwa na madumu manne au matano ndani mnatia karafuu, hayo ndio matatizo yenu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema karafuu ikitoka hapa ije kule, kibali kitaonesha kwamba wewe karafuu umeichukua sehemu fulani na umekwenda nayo sehemu fulani, sisi tutakutizama kama hukuja kuuza tutakuja kukudai karafuu zetu. Wakati huo umeshazitia ndani ya madebe, umeshazipeleka Mombasa. Tukija kukuuliza karafuu Sheikh ziko wapi, wewe ulipoondoka katika shehia hii uliondoka na karafuu gunia nne mbichi ukenda kuanika Kojani, lakini mpaka leo Kojani hajaja mtu kuuza karafuu hapa, je karafuu mmezipeleka wapi. Ndio maana yake.

Mhe. Mwenyekiti, tunachozuia hapa ni magendo ya karafuu yaliyokithiri na hasara ya magendo ya karafuu sio moja. Hasara ya kwanza taifa linakosa pesa za kigeni, hasara ya pili karafuu inakwenda kuchakachuliwa, kwa sababu karafuu ya Zanzibar ile *brand* inaondoka kabisa sasa hivi na inakuwa sasa hivi karafuu ya Zanzibar mbaya, chafu na haifai, ndio maana hatutaki karafuu ikauzwe Mombasa. Mombasa hawana karafuu, sana wakiuza karafuu ni ya Zanzibar, lakini wameshachakachua ndio maana hatutaki karafuu iende kule.

Kwa hivyo, mwakilishi utusaidie kuzuwia magendo ya karafuu, usitusaidie kusalihisha magendo ya karafuu. Kwa hivyo, kibali kinachotoka kwa sheha kutoka shehia moja kwenda shehia nyengine, ni ithibati itakayotusaidia sisi kuweza ku-*monitor* nani ana huo uchumi wa nchi hii. Sasa Mhe. Mwakilishi tusaidie tujenge uchumi wetu, usitusaidie kubomoa uchumi wetu, kibali hiki ni muhimu sana kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine au kutoka shehia hii kwenda shehia nyengine ni lazima kibali, tuzaidie ili tujenge uchumi wa nchi yetu, ukitusaidia kubomoa tutaharibikiwa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anifahamu mawazo yangu niliyozungumza. Sisemi kuwa utaratibu wa kutoa kibali kama ni mbaya, utaratibu huu mimi nimeupongeza. Lakini nasema hivi, kama nilivyoeleza mwanzo kuwa zao la karafuu lina pande mbili katika kuchuma. Kuna anaekwenda kuchuma akaweka kambi na...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hebu subiri kidogo. Waheshimiwa msitoke tunataka kumaliza hapa, waheshimiwa mnaokwenda kusali msitoke *quorom* inapungua hii. Endelea.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Na kuna anayekwenda kuchuma akarudi. Nikatoa mfano kama Kojani ina sehemu za Chwale, sio lazima Kojani tu Mhe. Mwenyekiti, na mimi sipalili kuwa magendo iendelee, hata siku moja sifanyi jambo hilo. Lakini nasema utaratibu mzuri uwekwe ili masheha wanapotoa vibali basi karafuu ihamishike mbichi kwenda kuaminikwa, mimi nasema wasiwasumbuwe wananchi, hili ndio tatizo liliopo.

Kwa hivyo, utaratibu mzuri kwa masheha uwepo, kama mtu anapotaka kibali cha kuchuma karafuu na kuhamisha shehia nyengine halafu siku nyengine aende kuchambua basi apewe. Nikazungumzia kama karafuu kavu mtu anakata kibali cha kwenda kuuza sio vyenginevyo, hili nieleweke, lakini ndani ya sehemu zote wakati wa msimu wa karafuu kunakuwa na *road block* kila sehemu na njia hizo ndizo zinazopitwa na wananchi. Sasa kama hukumpa kibali atafanya nini. Hilo ndio ninalomsisitiza sheha kutoa vibali kwa wananchi wanaokwenda kuchuma karafuu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, hili tatizo litakuwa ni la sheha. Sisi tukiripotiwa kuwa sheha hatoi vibali basi atachukuliwa hatua, hatoachiwa tu, huyo ndio usheha hautaki tena keshauchoka. Kwa hivyo, naomba kwamba kama kuna masheha ambao wanawasumbua wananchi kwenye vibali basi tuwaripoti hadharani na wachukuliwe hatua. Lakini ni wajibu wa sheha kwa sheria hii na sheria iliyopita, sheria zote zilizokuja zinasisitiza kwamba sheha ndiye atakayepewa kibali cha kusafirisha mzigo wa karafuu.

Sheria hii inakwenda mpaka kwa Mkuu wa Wilaya, ili kuwapunguzia dhiki basi tumemuondoa Mkuu wa Wilaya kwa sababu yuko mbali, lakini sheha yumo ndani ya kijiji. Mamlaka tumempa sheha basi Mkuu wa Wilaya sasa hivi hatoi tena kibali. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwakilishi kama kuna sheha yeyote atasumbua au anasumbua wananchi basi tusimfiche, itakuwa ni matatizo ya sheha ya kibinadamu hayo, lakini sio matatizo ya sheria.

Sheria haina tatizo, sheha huyo tukiripotiwa tumchukulie hatua, naamini kwamba hatoachwa afanye mambo yake anavyotaka. Sheria iko wazi kwamba sheha lazima atowe kibali kwa mujibu wa sheria hii. Naomba utukubalie ili sheha bado aendelee kuwa anafanya kazi hiyo, na kibali ni muhimu ili kitoke na sheha aliyekuwa anafanya sivyo tumchukulie hatua.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, kwa kauli ya waziri aliyoitoa kwamba sheha akienda kinyume na jambo hilo la kumzuwia mwanamke anayekwenda kuchuma karafuu kibali bila ya sababu za msingi atachukuliwa hatua basi naomba tuendelee.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niko kwenye kifungu hicho hicho na nina mambo mawili ambayo Mhe. Waziri atatusaidia. Mhe. Mwenyekiti, kila sheria tunayotunga hapa huwa na kifungu kwamba waziri atatunga kanuni, lakini inafika wakati waziri kwa miaka minne hajatunga kanuni na sheria nyingi sasa hivi hazina kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amesema hapa kwamba sheria hii ikishasainiwa na Rais, basi haiendi kukaa chini ya *file*, utekelezaji wake ni *fast track*. Kwa hivyo, mimi namuomba waziri kwamba wakati anasubiri sheria hii kutiwa saini na Rais basi yeye afanye hiyo kazi ya kutunga hizo kanuni, kwa sababu suala la karafuu ni suala endelevu na kama mnavyoona kila mwaka kuna misimu miwili. Hilo moja.

Lakini jengine alipotajwa sheha mimi hapa kichwa kimenizunguka. Mhe. Waziri anajua tabia ya sheha, anaposema kwamba sheha asipofanya hivi atachukuliwa hatua. Mimi kwanza siamini kwamba kuna chombo kinaweza

kumchukulia sheha hatua. Sasa ni vizuri atuwekee sawa, ni sheha yupi huyo ambaye amekusudia, ni huyu sheha wa shehia au kuna sheha mwengine. Maana sheha wa shehia waheshimiwa wameshapelekwa kila mahali hawaulizwi na ingekuwa yeye Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ndiye atakayewachukulia hatua basi mimi nakubali. Lakini kama kuna mtu mwengine wa kumchukulia hatua sheha, suala la sheha kutotoa vibali hatotoa na wala hatofanywa lolote.

Kwa hivyo, atuthibitishie hapa waziri kwamba sheha endapo hatotowa vibali kwa sheria hii basi ni hatua gani atachukuliwa na kama hatua hiyo haikuchukuliwa tufanye nini sasa sisi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu sheria hii ya karafuu Mhe. Mjumbe anataka ithibati. Mhe. Mwenyekiti, kwa sheria hii amuulize AG, kwa sababu AG alikuwa hanywi maji kwa sheria hii. Kila siku nilikuwa namfuata nataka sheria itoke. Kwa hivyo, sasa hivi sheria imeshatoka nashukuru sana, naitaka haraka na nakukuahidi kuwa kanuni itatoka mara tu sheria ikishatiwa saini na kanuni zitakuwa ziko tayari. Ikifika wakati wa bajeti basi nihoji iko wapi kanuni, kama kanuni sina basi bajeti yangu usipitishe hapa, hilo la kwanza.

La pili nataka nikuambie kwamba mimi ndiye Mwenyekiti wa *Taskforce*, *Taskforce* hii wajumbe wake ni Wakuu wa Mikoa wote watano wa Unguja na Pemba na Wakuu wote wa Vikosi vya Ulinzi ninao katika *taskforce* yangu na mimi namwambia Mkuu wa Mkoa, kikao kikiamua sheha huyu hafanyi kazi yake basi Mkuu wa Mkoa achukuwe hatua na ndio kazi ya *Taskforce*. Pia kuangalia magendo ya karafuu na moja katika magendo ya karafuu ni uhamishaji na vile vile kuangalia kila kinachotanza shughuli muhimu za karafuu.

Kwa hivyo, nasema kwamba masheha tunawashughulikia vizuri sana katika *Taskforce*. Wako masheha ambao wameshapewa onyo tayari na wako masheha ambao sasa hivi wamekuwa ni sehemu ya *Taskforce*. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Mhe. Tindwa anakwenda kwa masheha anawaambia hivi hivi kwamba kama sheha hataki kazi basi asituchafulie mipango yetu ya *Taskforce* katika suala la karafuu, anawaambia wazi kabisa.

Kwa hivyo, naomba uondowe wasi wasi kabisa, kwamba Wakuu wa Mikoa ambao wamo katika *Taskforce* ni *commited* na wale masheha wako kwa Wakuu wa Mikoa. Sheha ambae atakwenda kinyume na sheria na taratibu hizi hatoachwa mimi nakuahidi hili. Mambo mengine sielewi, lakini kuhusu karafuu masheha tunawashughulikia ipasavyo. Wako masheha wana

mashamba ya karafuu tutawanyang'anya, wako masheha ambao walikodisha karafuu kinyume na sheria wamengolewa.

Kwa hivyo, ninayo mifano minne mpaka mitano ya masheha wenye tabia hizo tukawachukulia hatua katika *Taskforce.* Naomba kukutoa wasi wasi huo kwamba masheha katika suala la karafuu hakuna mchezo tunawafanyia kazi.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia vizuri sana Mhe. Waziri alivyosema. Lakini katika maelezo yake sehemu kubwa anazungumza yeye. Kuna tofauti ya yeye kama waziri, sasa hivi Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ni yeye, lakini uwaziri haufi, wala hauondoki yeye kama Nassor Ahmed Mazrui anaondoka na anakufa.

Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu, mimi ninachozungumzia tutunge sheria ambayo akiwepo yeye na asiwepo yeye, iwe na nguvu moja ndio maana yangu tu. Sisi tunajua kwamba kwa yeye hata kama sheha hakuchukuliwa hatua basi yeye analo la kufanya, lakini ni yeye. Tutunge sheria kwamba Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko yeyote atakaye kuwepo, hizo hatua za sheha za kuchukuliwa basi zichukuliwe kweli na zionekane, masheha wana matatizo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa majibu yake ambayo ameyatoa yanayohusu masheha na namna hatua za serikali zilivyochukuliwa kwa wale masheha ambao wameonekana wanakwenda kinyume na sheria.

Sheria hii ni sheria ya karafuu ambayo inasimamiwa na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, lakini sheha ni mtendaji wa serikali katika ngazi ya chini kabisa ya serikali. Sheha ana sheria yake, mamlaka aliyonayo sheha katika sheria yake vile vile anatakiwa aheshimu sheria za mamlaka nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, serikali sio kwa vile mimi ni Waziri wa Tawala za Mikoa na Idara Maalum niwe ninatumia sheria zangu peke yake bila ya kujali sheria za wizara nyengine. Kwa hivyo, mimi nataka nimtowe wasi wasi Mhe. Mwakilishi, Mhe. Hamad Masoud Hamad (mtu mzima), kwamba kama alivyosema Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, tatizo la uhalifu katika karafuu, utoroshaji wa karafuu, uhaulishaji wakarafuu wa kijanja umewezekana kudhibitiwa kutokana na mashirikiano yaliopo kati ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makamanda wa Vikosi pamoja na masheha. Nafasi hiyo haimpi mwanya sheha ambae anakwenda kinyume na taratibu na maelekezo ya serikali au kutokufuata sheria za serikali.

Kwa hivyo, mimi nataka niendelee kumsihi Mhe. Hamad Masoud Hamad kwamba kwa hili atuamini kama serikali, kuwa sisi tunapania kulitunza na kulipa ubora zao la karafuu ya Zanzibar na katika hili hatutomuonea haya mtu yeyote, awe sheha, DC au mwengine yeyote. Kila anayefanya makosa tunamchukulia hatua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niwahakikishie kwamba kazi ya kudhibiti kazi ya karafuu, haifanyi Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko peke yake, tunaifanya kwa pamoja kama serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimekuwa nikifanya ziara za mara kwa mara kwenda Pemba, ninaposikia kuna mtu anafanya uharibifu katika zao la karafuu basi ninakwenda na ninachukua hatua, ninamuambia mwenzangu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwamba nimekwenda pahala fulani na nimekuta mtu ana kiwanda cha kutuharibia karafuu yetu ya Zanzibar. Anachukua makonyo anayatengeneza kama karafuu, anazichanganya na karafuu anauza Kenya.

Huyo mtu niliamua jana kumuweka ndani. Sio jana kwa maana ya jana, hapana. Wakati nilipokuwa nampa taarifa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ndio nilimuambia hivyo. Kwa sababu anatuharibia, kwa hivyo sio sheha, sio Mkuu wa Wilaya, sio Mkuu wa Mkoa, sio Kamanda wala sio waziri, tukibaini kama unakwenda kinyume na taratibu na sheria ambazo tumezipitisha na kanuni ziliopo, basi tutakuchukulia hatua.

Kwa hivyo, Mhe. Hamad Masoud Hamad atuamini, kwamba hiyo kazi tunaiweze kuifanya. Katika kipindi kifupi hiki wapo masheha ambao wameshachukuliwa hatu, baada ya kuonekana kwamba wanafanya mambo kinyume na utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa nitowe melezo hayo tu. *(Makofi).*

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaheshimu sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum ambaye ni mtu mzima mwenzangu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitosimama tena kwa hili kwa sharti lifuatalo, kuwe na kanuni maalum itakayomfanya sheha akithibitika na ukorofi katika hili, kwa maana kwamba hatoi vibali kwa ukorofi tu, basi sheha huyo *automatically* awe sio sheha tena. Sio sheha tu, lakini kwanza namzungumzia sheha, kwa sababu sheha ndio *basic*. Huyo mtu wa Kojani anayekwenda kuchukua karafuu zake Kirimdomo anaanza na sheha na hawa ndio wakorofi au kujua hatuna matatizo kiasi hicho. Kwa hivyo, kama kuna kanuni ambayo

waziri atatuthibitishia kwamba na hiyo kanuni itakuwemo. Mimi nitaachia ngoma iendelee. Vyenginevyo itabidi tukeshe.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mheshimiwa katika kipingele hicho, waziri ataweka taratibu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kifungu hiki. Mimi naahidi kwamba nitaweka taratibu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kifungu hiki wala asiwe na wasi wasi. Utaratibu utakuwa wazi kabisa, kama sheha hawajibiki tutamchukulia hatua.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mheshimiwa hicho kifungu nimekiona. Nataka waziri anithibitishie katika hizo taratibu atakazoweka kifungu hicho kimo. Anaweza akaweka taratibu lakini kifunguo hicho kisiwemo. Nataka anithibitishie, kwamba mie nimekiona, kwamba utarabu nitakaouweka ni huo endapo sheha atathibitika si maneno tu. Nikisema kuthibitika ni ushahidi. Sheha huyo iwe *automatically* si sheha tena, hapa ndipo sheha atakapoweka akili yake vizuri. Kwa sababu usheha una maslahi makubwa na akijua kwamba nikifanya hili mimi si sheha tena na elimu ikitolewa. Mimi nakuhakikishia ukorofi wa karafuu kama tunaweka hadhi kweli, hadhi yote hii endapo sheha hakudhibitiwa, anaweza akaikoroga wala hakuna lolote la kufanya.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mimi nadhani mnakosana padogo tu. Mhe. Waziri wa Biashara kasema ataweka kwenye kanuni na keshakubali hapa. Kwama mwanzo kwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Inakuwa tunawekana mda mwingi suala hilo kwa hilo tunazunguka. Kakubali kwenye kanuni kwamba atatoa maelezo, kwamba sheha yeyote ambaye hakufuata utaratibu ataondoshwa.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mheshimiwa sikumsikia aseme tena nimsikie.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa kiti hukiamini huku na kinasema kwa niaba ya Waziri.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mimi nasema kwamba sikumsikia sio kwamba nasema kiti sikiamini.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi niliyesikia ndio nakwambia kwamba waziri kakubali katika Kanuni ataweka utaratibu. Sheha yeyote aliyekuwa hakufuata utaratibu unaotakiwa kisheria basi ataondoshwa.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Basi tuendelee.

Sehemu ya Nne

Usimamizi wa Mfuko

Kifungu cha 20

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia niliuliza hapa na nilikitaja kifungu kwa ufafanuzi, kwamba katika suala la uteuzi wa Benki hapa. Pamoja na kutambua malengo ni kulinda maslahi ya mfuko, lakini niliuliza kwa nini Waziri wetu ambae ni mzalendo sana na anaipenda sana Zanzibar kama anavyoipenda karafuu basi aipende PBZ. Ili PBZ hapa ikatajwa kwamba ndio Benki itakayotumika kwa shughuli hizi kwa madhumuni ya kuendeleza, kuwekewa mitaji ambayo ikishapatikana faida, faida yenyewe nayo itakuja kutumika kwa wanachi wa Zanzibar. Naomba maelezo kuhusiana na hilo, kwa nini asiione haja hiyo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mheshimiwa nililijibu suala hili lakini nitajibu tena. Kwa sababu mimi ni mmoja ninaeipenda sana PBZ na ZSTC ina *account* zake zote PBZ. Lakini mimi ni Waziri wa Biashara na Viwanda na nina sheria ya kuweka *Bank competition* lazima niweke *fair trade competition* kama Waziri wa Biashara. Nitakapoiweka PBZ katika sheria mabenki yote yatalalamika kwamba nyinyi mnaipenda PBZ kama serikali. Hivi sasa malalamiko yapo tayari.

Zanzibar kuna Benki 13 ikiwemo PBZ, tukiitia katika sheria hapa tayari tunaipa *fever* PBZ kwa hivyo kutakuwa hakuna *fair trading competition.* Kwa hivyo, Bodi itakuwa ni hiari yake kuweka PBZ au benki nyengine yoyote ile, itakayokuwa na maslahi, na *experience* kwa mfuko huu. Kama wafanyabiashara nikitia PBZ itakuwa nnakwenda kinyume na zile silka za Biashara. Biashara huru Zanzibar hatuna *restriction*, tumeikaribisha mabenki na vyombo vyengine vya fedha. Nimesema kwamba siwezi kuitaja PBZ kwa sababu nitakuwa nakwenda kinyume na zile *marits* za biashara hapa. Kibiashara Benki ukiitaja hapa tayari wale wengine umeshawatia katika kapu na hawatokubali, wata-*claime*.

Kwa hivyo naomba tukubali kwamba PBZ tunaipenda, PBZ benki yetu lakini kwa kulinda silka za biashara tuache biashara huru, Zanzibar tunataka iwe ni Zanzibar ya biashara huru. Isiwe ni biashara ya ukiritimba, ukang'ang'ania chako tu. Ni vyema tuwape nafasi na mabenki mengine yoyote ikiwa ni biashara huru katika kisiwa hichi cha Zanzibar. Ili na wao wajisikie kwamba ni *part nad parcel* ya kujenga uchumi wa nchi hii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo hayo mazuri ya Mhe. Waziri nimemkubalia naomba tuendelee.

Kifungu cha 20 Uteuzi wa Benki Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 21 Ulipaji wa Fedha za Mfuko Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Tano

Masharti ya Fedha

Kifungu cha 22

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki nipo katika kifungu cha 22 (2) nadhani Mhe. Waziri wa Biasharara, Viwanda na Masoko, atakumbuka katika mchango wangu nilizungumzia kifungu hiki naomba nikisome ili hoja yangu iweze kueleweka vizuri.

> Kifungu cha 22(2) "Fedha za Mfuko zitatumika kwa kazi na madhumuni ya mfuko tu kama itakavyoainishwa na Bodi na uongozi wa Shirika hautakuwa na uwezo wa kutumia fedha za mfuko kinyume na masharti ya kifungu hiki."

Sasa katika mchango wangu nilimuomba Mhe. Waziri kwa nini isifanywe rejea hapa kwa kifungu cha 5 ambacho tayari kimeshataja nini malengo ya fedha za mfuko. Nilimwambia wasi wasi wangu kwamba tukiweka hivi, sawa imesema madhumuni ya mfuko lakini haikufanya rejea katika kifungu kile na imerejesha mamlaka kwa bodi ya uongozi wake kuweza kuamua. Nikawa na wasi wasi kwamba mara nyengine tukiachia namna kama hii inaweza kabisa bodi ikaja ikafanya maamuzi ambayo kinyume na yale pale. Kwa sababu itakuwa tayari wamo ndani ya sheria wanafuata madaraka ambayo wamepewa na sheria.

Kwa hivyo nimesema kwamba hapa tufanye rejea ya kile kifungu cha 5, kama ameshakikubali katika maelezo naomba anizindue mimi sikuwa nimekisikia, lakini kama hajakikubali basi naomba akubali awe na mimi kwamba hiki kifungu kifanyiwe marekebisho madogo tu, ya kusema kwamba "kwa kazi na madhumuni ya mfuko tu, kama ilivyoainishwa ndani ya kifungu cha 5 cha sheria hii" halafu tena itaendelea kama ilivyokuwa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Hilo tulilikubali tangu katika ratiba yangu ya mwanzo, *no problem*.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 22 Vyanzo Vya Fedha ya Mfuko
Kifungu cha 23 Matumizi ya Bajet
Kifungu cha 24 Hesabu za Ukaguzi Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Sita

Masharti ya Jumla

Kifungu cha 25 Miongozo ya Waziri
Kifungu cha 26 Makosa na Adhabu Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 27 Makosa ya Shirika Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 28 Makosa ya Uwakala Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 29 Kumaliza Kosa Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 30 Uwezo wa Kutunga Kanuni
Kifungu cha 31 Kufuta na Kubakiza

(*Baraza lilirudia)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi, wanaokubaliana na hoja aliyotoa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko mikono juu, waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Maendeleo ya Karafuu ya Mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria wa Maendeleo ya Karafuu ya Mwaka 2013, usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja aliyotoa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, mikono juu, waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolwa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa sheria ya serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa kazi tuliyoifanya, tangu katika michangio na baadae tumeupitisha Mswada. Tunampongeza Mhe. Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko na tunamtakia kazi njema pamoja na Naibu wake na watendaji wake kwa ujumla.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ): Mhe. Naibu Spika, naomba kwa idhini yako kusoma taarifa ya utekelezaji wa maagizo kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kutujaalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana katika kikao hiki muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Vile vile naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, na Wenyeviti wa Baraza wa Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa uongozi wenu wenye hekma busara na uwadilifu katika kuliongoza Baraza na kuliwezesha kusimamia vyema majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, pia natoa shukuruni zangu za dhati kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano makubwa wanayoipatia ofisi yetu na kwa ushauri na maelekezo yao kwetu yanayotusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa Fedha wa 2012/2013 Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ilipokea jumla ya maagizo 40 kutoka kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ambayo yaligusa idara na taasisi mbali mbali za Ofisi hii. Ofisi ilifuatilia maagizo hayo na kuchukua hatua za utekelezaji.

Maelezo ya utekelezaji wa Maagizo

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwa Baraza lako Tukufu juu ya utekelezaji wa maagizo hayo kama ifuatavyo:-

Agizo Namba Moja

Kwa kuwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inasubiri mchakato wa uwajiri wa wataalamu kutoka serikalini ni vyema mchakato huo ukaharakishwa ili Idara za ofisi hii zikapatiwa wataalamu hao na kuleta ufanisi wa utendaji.

Mhe. Naibu Spika, agizo hili limetekelezwa kikamilifu kwa Ofisi kuwaajiri vijana 21 wa fani mbali mbali katika ngazi ya elimu ya Shahada ya Kwanza. Vijana hao wamepangiwa kufanya kazi katika idara mbali mbali za ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Agizo Namba Mbili

Kuna umuhimu kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupatiwa usafiri wa kutosha katika ofisi zake, hususan zile zilizokuwepo Pemba na Dar-es-Salaam. Magari yaliyochakaa kupita kiasi ni busara yakapigwa mnada lakini baada ya kupatikana gari mpya.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kupitia bajet ya mwaka 2013/2014 imepanga kununua gari tano katika Idara ya Mipango moja, Idara ya Maafa, moja Uratibu na Ofisi ya Faragha gari mbili. Gari na vyombo vyengine vya usafiri vilivyochakaa vitauzwa kwa mujibu wa sheria ya manunuzi na uondoaji wa mali chakavu za serikalini.

Agizo Namba Tatu

Ununuzi wa mitambo mipya kwa ajili ya kiwanda cha uchapishaji ni vizuri ikaharakishwa. Lakini pia kunaumuhimu kwa taasisi za serikali kulipa madeni inayodaiwa na kiwanda ili kukiwezesha kiwanda hicho kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuiongezea mapato serikali. Aidha, kuna umuhimu kwa kiwanda hiki kufikiriwa kuwa Shirika la Umma.

Mhe. Naibu Spika, nina furaha kulieleza Baraza lako tukufu, kwamba ununuzi wa Mashine za kisasa za uchapishaji kwa awamu ya kwanza umekamilika. Tayari mashine hizo zimeshafungwa na kiwanda kinafanya kazi. Serikali inampango wa kukifanya kiwanda kijiendeshe kibiashara na kurudisha huduma za Bohari Kuu. Aidha, serikali inaangalia uwezekano wa kukifanya kiwanda kuwa taasisi inayojitegemea.

Agizo Namba Nne

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Zanzibar itasherehekea miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ifikapo mwaka 2014 kuna umuhimu mkubwa sherehe hizo zikaadhimishwa kwa hali ya kipekee kutokana na umri wa sherehe hizo.

Aidha kuna haja ya msingi katika mji wa Zanzibar kuwekwa kielelezo au alama inayoonyesha kumbukumbu ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964. Pia suala la kuanzishwa nembo ya kumbukumbu ya Mhe. Abeid Amani Karume, linahitaji kupewa kipaumbele ili kumuenzi kiongozi huyo shupavu.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu ni mashahidi wa namna serikali ilivyoadhimisha Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sherehe zilikuwa za aina yake na zilifana sana na kusifiwa ndani na nje ya nchi yetu. Aidha, Serikali imeweka jiwe la Msingi la Ujenzi wa Mnara wa Kumbukumbu ya Mapinduzi katika eneo la Michenzani na kuandaa nembo maalum ya kuadhimisha sherehe hizo kama ilivyoagizwa na Kamati.

Mhe. Naibu, Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza na Wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa jinsi tulivyoshirikiana katika kuadhimisha sherehe zetu hizo adhimu za Mapinduzi yetu kutimia nusu karne.

Agizo Namba Tano

Suala la malipo kwa wale waliofiwa na jamaa zao katika ajali ya MV. Spice linahitaji jitihada ya kukamilishwa kwani limekwisha kuchukua muda mrefu tangu ajali hiyo imetokea.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la malipo kutokana ajali ya meli ya MV. Spice Ilander One, naomba kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba wale wote wanaostahiki kulipwa malipo hayo kwa kuonesha vielelezo sahihi

wamelipwa. Hivi sasa hakuna madai yeyote ya watu wenye vielelezo vya kuhusika na ajali hiyo ambao hawajalipwa fedha zao.

Agizo Namba Sita

Mhe. Naibu Spika, kutokana na utekelezaji usioridhisha wa taarifa za Kamati za Kudumu na Kamati Teule za Baraza, kamati inaitaka serikali zifanyiwe kazi ripoti hizo ili kupunguza kero katika jamii na kupelekea wananchi kuwa na imani serikali yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba serikali tayari imezishughulikia taarifa zote za Kamati Teule na inaendelea kuyafanyia kazi mapendekezo yote yalitotolewa kupitia Kamati hizo.

Agizo Namba Saba

Kwa kuwa kuna malalamiko na migogoro mingi ya ardhi, kuna umuhimu wa msingi kwa waratibu wa Ofisi ya Makamo wa Pili Rais kuwashauri ipasavyo Makamo wa Pili na Waziri wa Nchi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa lengo la kulitafutia ufumbuzi suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la migogoro ya Ardhi. Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais hupokea malalamiko na kuyafatilia kujua kiini chake na hatimaye kuwasilishwa kwa taasisi husika na kuzitaka taasisi hizo kuyafanyia kazi malalamiko hayo na baadaye kuiarifu Ofisi ya Mako wa Pili wa Rais juu ya hatua zilizochukuliwa.

Aidha, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imekuwa ikiendelea kuwanasihi viongozi wa Wizara inayohusika na ardhi, Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Shehia na Wananchi kwa jumla kujiepusha na kujihusisha na migogoro ya ardhi. Vile vile zoezi la utambuzi na umiliki wa ardhi na mali zisizohamishika linaloendelea hivi sasa lina lengo la kupunguza tatizo hilo.

Agizo Namba Nane

Ili kutekeleza vyema suala la utawala Bora na kuzifanya taasisi tatu za nchi kwa maana ya Mahakama, Chombo cha kutunga Sheria na serikali kutekeleza kazi zao bila ya kuingiliana, ni vyema Mahakama ya Ardhi ikawekwa chini ya Mahakama Kuu badala ya utaratibu wa sasa ambapo Mahakama hiyo ipo chini ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, imepokea pendekezo la Kamati la kutaka Mahakama ya Ardhi kuwekwa chini ya Mahakama Kuu.

Kwa vile suala hili ni la kisheria na linahusu muundo wa kitaasisi. Ofisi yangu inaendelea kuwasiliana na taasisi husika ili kuona jinsi ya kulishughulikia.

Agizo Namba Tisa

Kwa kuwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ndio Kiongozi wa shughuli za serikali, ipo haja ya kukiboresha kitengo cha habari ili kuweza kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za serikali, pia kupitia *website* ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imechukua juhudi kubwa za kukiimarisha Kitengo cha Habari na Mawasiliano kwa kuwaajiri wataalamu wawili wapya wenye taaluma ya masuala hayo, kutoa mafunzo kwa watendaji wa kitengo hicho na kununua vifaa vya mawasiliano kupitia msaada wa UNDP. Hivi sasa tovuti ya serikali inafanya kazi na inaendelea kuimarishwa.

Agizo Namba 10

Kwa kuwa eneo kwa ajili ya makaazi ya Makamo wa Pili wa Rais limeshapatikana kuna umuhimu mkubwa wa kuchukuliwa hatua za kuanza ujenzi wa nyumba yenye hadhi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Wizara ya Fedha imeandaa mpango maalum wa ujenzi wa makaazi ya viongozi wakuu wa kitaifa kwa Unguja na Pemba. Mpango huu unatekelezwa kwa awamu kulingana na uwezo wa kifedha. Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, tayari imeandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa makaazi ya Viongozi hao na mara fedha zitakapopatikana hatua za ujenzi zitaanza mara moja.

Agizo Namba 11

Kuna umuhimu mkubwa kwa serikali kuipatia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais usafiri wenye hadhi na wa uhakika kwa ajili ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba hali ya usafiri kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa upande wa Pemba, Dar-es-Salaam na Dodoma si ya kuridhisha. Serikali inalishughulikia suala hili na imepanga kununua gari kwa ajili ya matumizi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kadri ya hali ya fedha itakavyoruhusu.

Agizo Namba 12

Ufinyu wa bajeti na uchangiaji wa fedha za bajeti katika ununuzi wa meli kumechangia kupunguza huduma za uendeshaji katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Pemba na taasisi nyengine zinazosimamiwa na Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa. Hivyo kuna haja kwa serikali kutenga bajeti itakayoiwezesha Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kufanya shughuli zake kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, serikali imekuwa ikiweka kiwango cha bajeti kwa wizara na taasisi za serikali kila mwaka kulingana uwezo wa serikali ulivyo.

Suala la ununuzi wa meli lilikuwa na umuhimu mkubwa ili kuimarisha hali ya usafiri baina ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba pamoja na Dar-es-Salaam. Hata hivyo Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kiasi kikubwa iliweza kutekeleza majukumu iliyojipangiwa katika mwaka wa fedha 2012/13, licha ya upungufu wa bajeti.

Agizo Namba 13

Idara ya Maafa Pemba inahitaji kupatiwa ghala yake kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake. Vile vile idara hii inahitaji kupatiwa vifaa kabla ya maafa kutokea.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Pili ya Rais imo katika hatua ya kupata maghala yake ya kudumu ya kuhifadhia vifaa vya maafa kwa Unguja na Pemba. Kwa upande wa Pemba jitihada zimefanyika za kupata ghala la muda katika kiwanja cha michezo Gombani. Aidha Ofisi yangu imo katika hatua za kutafuta vifaa vya maafa kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wakiwemo Mashirika ya Ummoja wa Mataifa.

Agizo Namba 14

Taasisi zinazohusika na utoaji wa elimu ya uraia, Tume ya Uchaguzi, Polisi pamoja na Polisi Jamii, zinahitaji kuwezeshwa na serikali ili ziweze kutoa elimu ya uraia kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984, Tume ya Uchaguzi inajukumu la kuwaelimisha wananchi wa Zanzibar na kuwahamasisha raia kwa kutoa elimu ya wapiga kura ili wajue wajibu wao, haki na fursa ya kujiandikisha ili waweze kushiriki kupiga kura na kuwachagua viongozi wao kila inapotokea uchaguzi. Kazi hiyo inaendelea na elimu hiyo hutolewa kwa njia ya mikutano, makongamano, vipindi vya

redio, televishen, magazeti na michezo ya kuigiza kupitia vyombo mbali mbali vya habari.

Agizo Namba 15

Miradi ya TASAF inayohusu ufugaji ni vyema ikawashirikisha wanavikundi wachache watakaowezeshwa vizuri ili waweze kutekeleza miradi hiyo kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, pendekezo lililotolewa na Kamati ni la Busara sana na Ofisi yangu italizingatia kikamilifu katika miradi itakayoendelezwa kupitia TASAF III na miradi mengine ili kuifanya miradi inayotekelezwa na wananchi kuwa ya tija, endelevu na yenye manufaa kwa wananchi.

Agizo Namba 16

Kamati inapongeza kuwa katika utekelezaji wa TASAF III familia masikini zitapatiwa fedha kwa ajili ya ununuzi wa sare kwa watoto wa familia hizo. Hata hivyo Kamati inaiomba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na serikali kwa ujumla kufikiria tena suala la wananchi katika TASAF III kuchangia asilimia 75 katika utekelezaji wa miradi kwani wengi wao hawana uwazo wa kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwaarifu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba katika mradi wa TASAF III wananchi hawatakiwi kuchangia bali fedha zote zitatolewa na mradi. Kilichokuwa kikielezwa ni kwamba asilimia 75 ya gharama za miradi itakayotozwa, itatolewa kwa njia ya fedha taslim zitakazolipwa kwa wananchi kama malipo ya nguvu kazi yaani *labour charge* na asilimia 25 iliyobaki itatolewa kwa ununuzi wa vifaa vya kuendeleza miradi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii, kuwaomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, viongozi wa maeneo na wananchi kutoa ushirikiano mkubwa kwa watendaji wa *TASAF* ili kutekeleza mradi huu kwa ufanisi na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika awamu zilizopita.

Agizo namba 17

Kuna umuhimu mkubwa kwa viongozi wa Jimbo kushirikiana na wananchi katika kuleta maendeleo ya vijiji vya majimbo yao. Aidha viongozi katika majimbo wa maeneo mengine ni muhimu wakaelewa kwamba ni jukumu lao kuwatumikia wananchi waliowachagua bila ya kujali itikadi ya vyama vyao.

Mhe. Naibu Spika, ninakubalina na wazo lilitolewa na Kamati la kutaka viongozi wa majimbo kushirikiana na wananchi katika kuleta meendeleo ya maeneo yao. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, inaendelea kutoa taaluma kwa wananchi juu ya kubuni, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Agizo namba 18

Taasisi za serikali zinazoshirikiana na washirika wa maendeleo katika kutekeleza miradi ya maendeleo katika majimbo mbali mbali zinapaswa kuzingatia umuhimu wa kuwashirikisha kwa kuwapatia ajira wananchi waliokatika maeneo yanayotekelezwa miradi hiyo kwa lengo la kustawisha maisha ya wananchi hao, lakini pia kupunguza malalamiko kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, serikali inachukua juhudi ya kutumia njia mbali mbali za kuona kuwa wananchi wa mijini na vijijini hali zao zinastawi na kuwapunguzia umaskini. Njia hizo ni pamoja na kuwawezesha kiuchumi kwa kuwapatia mikopo kupitia mifuko mbali mbali, ajira na kuwapelekea miradi ya kuongezea kipato. Kwa hivyo, serikali kwa kushirikiana na wafadhili na wewekezaji itahakikisha kuwa wananchi waliopo katika maeneo ambako miradi inatekelezwa wanafaidika sio tu na ajira katika miradi hiyo, lakini pia na faida za kiuchumi na kijamii zinazotokana na miradi hiyo.

Agizo namba 19

Suala la mikopo kwa wananchi lina umuhimu wake katika ustawi wa wananchi hao na taifa kwa ujumla. Hivyo, ni vyema mikopo itolewe bila ya kubagua maeneo. Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuchukua hatua mbali mbali zenye lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Miongoni mwa hatua hizo ni kuwapatia wananchi mikopo kwa gharama nafuu kupitia mifuko mbali mbali. Mikopo hiyo hutolewa bila ya upendeleo wa aina yoyote ilimradi anayeomba mkopo huo atimize masharti yaliyowekwa na afuate utaratibu.

Wananchi wengi Unguja na Pemba kutoka katika makundi mbali mbali kama vile watu wenye ulemavu, wanawake na vijana wamefaidika na mikopo hiyo inayotolewa na serikali.

Agizo namba 20

Suala la migogoro ya ardhi limechangiwa na baadhi ya viongozi wakiwemo masheha, hivyo kuna haja kwa viongozi hao kwa kushirikiana na wananchi

kuyatatua matatizo hayo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein, katika ziara zake za kutembelea Mikoa ya Unguja na Pemba amewaagiza viongozi wa Mikoa hiyo wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Masheha kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi katika maeneo yao kwani kwa kiasi kikubwa viongozi hao ndio walioisababisha migogoro hiyo.

Agizo namba 21

Kwa kuwa wananchi wa Mtambwe Kusini wanataka maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama walivyoieleza Kamati, kuna haja kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Taasisi nyenginezo na serikali kuhakikisha kuwa wanakikumbuka kijiji hicho na vyenginevyo katika utekelezaji wa miradi ya *TASAF* 111. Mhe. Naibu Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalenga kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Kutokana na azma hiyo ya utekelezaji wa *TASAF* 111 utashirikisha shehia zote za Unguja na Pemba kikiwemo kijiji cha Mtambwe Kusini.

Agizo namba 22

Kwa kuwa Tume ya Uchaguzi Pemba imeshapatiwa Kiwanja kuna haja kwa serikali kuiwezesha Tume kuanza ujenzi wa Ofisi yake. Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi, serikali ya Mapindzi ya Zanzibar inakusudia kuipatia Tume hiyo Ofisi katika ngazi za Mikoa na Wilaya Unguja na Pemba, utekelezaji wa azma hiyo, utakwenda hatua kwa hatua kutegemea na hali ya upatikanaji wa fedha.

Agizo namba 23, 27 na 37

Kuna haja kwa Idara ya Upelelezi Zanzibar kupatiwa usafiri ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Mhe. Naibu Spika, katika kulitafutia ufumbuzi tatizo la usumbufu wa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi Zanzibar, ikiwemo Idara ya Upelelezi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshafanya mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nia ya kulipatia jenshi hilo hapa Zanzibar vifaa na nyenzo mbali mbali ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Agizo namba 24, 25 na 40

Kwa kuwa nyumba za askari za Ziwani na Mwera ni Kongwe, zinahitaji kufanyiwa matengenezo na zaidi kwanza iangaliwe huduma ya dharura yaani

ziezekwe ili kuzihami. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba nyumba za askari wetu zinahitaji kufanyiwa ukarabati ili ziwe na hadhi inayostahiki. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, imelifatilia suala hili kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuarifiwa kwamba umeandaliwa mpango kwa Tanzania nzima wa ukarabati wa nyumba za Polisi na ujenzi wa nyumba mpya kwa ajili ya Jeshi hilo. Nyumba za askari za Ziwani, Mwera na Tunguu nazo zimeingizwa katika mpango huo.

Agizo namba 26

Kuna haja ya kuimarisha Kituo cha Chwaka kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo hayo ya kitalii. Mhe. Naibu Spika, ninakubaliana na hoja ya Kamati juu ya umuhimu wa kukiimarisha kituo cha Polisi Chwaka ili kuimarisha shughuli za ulinzi na usalama katika eneo hilo la utalii na maeneo ya jirani. Suala hili tayari limeanza kuzingatiwa na Serkali na mipango inaandaliwa yakuimarisha ulinzi katika maeneo yote ya utalii Unguja na Pemba ikiwemo eneo la ukanda wa Chwaka.

Agizo namba 28

Makaazi ya mbwa nayo yanahitaji kuboreshwa ili kusaidia ulinzi na usalama. Mhe. Naibu Spika, kamati pia imeona haja ya kuimarishwa makaazi ya wanaotumika kwa kazi za ulinzi na usalama. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tayari imefanya mazungumzo na Jeshi la Polisi Zanzibar na kuwataka kulitekeleza Agizo la Kamati la kuimarisha huduma na makaazi ya mbwa wa ulinzi wa Jeshi la Polisi. Taarifa tulizonazo suala hili tayari limeshaanza kufanyiwa kazi.

Agizo namba 29 na 38

Kitengo cha Kupambana na Dawa za Kulevya, kinahitaji kuimarishwa kwa kupatiwa usafiri, simu pamoja na radio za mawasiliano ili kupambana ipasavyo na suala la dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika: Kwa kuwa muda wetu umesalia mdogo na bado kuna karatasi tano, ninamuomba Mwanasheria Mkuu alete utaratibu ili tuweze kumalizia hotuba ya Waziri.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa vile muda uliobaki ni mdogo kumaliza shughuli iliyopo mbele yetu, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu litenge kando kanuni ya muda ili tuweze kuweka muda wa kumuwezesha Mhe. Waziri kumaliza kusoma hotuba yake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kaimu. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ): Mhe. Naibu Spika, agizo namba 29 na agizo namba 38 kama nilivyokwisha kulisoma utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshafanya mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya kulipatia vifaa na nyenzo mbali mbali Jeshi l Polisi upande wa Zanzibar. Kitengo cha kupambana na dawa za kulevya cha Jeshi hilo pia kitafaidika kwa kupatiwa usafiri, simu pamoja na radio za mawasiliano.

Agizo namba 30

Baadhi ya wakati askari hucheleweshwa kupatiwa mshahara, viinua mgongo na pencheni zao. Hivyo, kuna umuhimu kwa askari kupatiwa mishahara, viinua migongo na pencheni zao mapema ili kuondosha usumbufu malalamiko. Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tayari imefanya mazungumzo na uongozi wa Jeshi la Polisi juu ya kuwapatia kwa wakati askari wa Jeshi hilo waliopo Zanzibar mishahara yao. Aidha jeshi hilo pia limetakiwa kulipa kwa wakati malipo ya viinua mgongo na pencheni kwa askari waliostaafu ili kuondosha ufumbufu na kuwapunguzia ukali wa maisha.

Agizo namba 31

Mbali ya kuanzishwa kwa dawati la masuala ya unyanyasaji, askari wanahitaji kupatiwa elimu kuhusu masuala ya kinamama, watoto na unyanyasaji wa kijinsia ili kupunguza hali inayojichomoza katika vituo vya Polisi kwa baadhi ya wananchi kunyanyaswa kijinsia. Mhe. Naibu Spika, ninakubaliana na hoja ya Kamati kwamba kuna haja kubwa ya askari wetu wa jeshi la Polisi kupatiwa elimu kuhusu masuala ya watoto na unyanyasaji wa kijinsia ili kuondosha kasoro zinzojitokeza katika vituo vya Polisi. Ofisi yangu imelitaka Jeshi la Polisi kuandaa na kutekeleza *program* maalum ya kuwaelimisha askari Polisi ili kuwawezesha kutekeleza wajibu wao kwa jamii bila ya kujihusisha na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

Agizo namba 32

Muekezaji wa hoteli ya *Cristal Resort Limited* ambaye amefadhili ujenzi wa Kituo cha Polisi Paje, anawanyanyasa wananchi wa eneo hio. Hivyo, kuna haja kwa Jeshi la Polisi kuchukua hatua ya kuikomesha hali hiyo na kuliondoa bango linaloonesha ufadhili wa nyumba hizo. Katika kikao hicho Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa na Uongozi wa Jeshi la Polisi Tanzania wamekubaliana kama yafuatayo:-

Moja kuwa na utaratibu wa kufanyika vikao kati ya Kamati na Jeshi la Polisi ambapo ilikubalika vifanyike vikao vitatu kwa mwaka. Kati ya hivyo viwili Unguja na kimoja Pemba na Kimoja Tanzania Bara.

Pili, kuandaliwe semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili Wajumbe hao wafahamu majukumu ya Jeshi la Polisi Tanzania na pia wafahamu mashirikiano kati ya jeshi hilo na Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, imeliagiza Jeshi la Polisi kufatilia malalamiko ya wananchi wa Paje kuhusiana na muekezaji wa hoteli ya *Crystal* kuwadhalikisha wananchi wa eneo hilo na kulichukulia hatua ipasavyo. Aidha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais itasimamia utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa baina ya Jeshi la Polisi na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya kuwa na vikao vya pamoja na kuandaa semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ya kujenga uelewa wa majukumu ya jeshi hilo.

Agizo namba 33

Kuna haja kwa masheha kuwa makini na kuwafatilia wakaazi na wageni wanaoingia na kutoka katika maeneo yao, Mhe. Naibu Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba suala hii la masheha tayari linafanyiwa kazi na Ofisi ya Rais na Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na masheha wote wametakiwa kuwa makini na wageni wanaoingia na kutoka katika maeneo yao.

Agizo namba 34

Baada ya kutolewa vitambulisho kwa wananchi Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kwa kushirikiana na Polisi na masheha inahitajika kufatilia katika shehia ili kubaini wenye vitambulisho na wasiokuwa navyo, aidha zoezi hilo litasaidia kuwatambua wanaoishi nchini kinyume na sheria za nchi. Mhe.

Naibu Spika, ushauri uliotolewa na kamati ni mzuri nia ya serikali kuwatambua wenyeji na wageni waliopo nchini na wale ambao wanaishi kinyume na sheria.Wale wote watakaogundulika kuishi kinyume cha sheria watachukuliwa hatua zinazostahiki.

Agizo namba 35 na 36

Kuna haja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar kutayarisha eneo ndani ya Kiwanja hicho, kuwekaeneo la kufanyia uchunguzi watuhumiwa wa dawa kulevya wanaoingia na wanaotoka nchini, hatua hii itasaidia kuepusha suala la kupoteza ushahidi wa uchunguzi wa dawa hizo.

Mhe. Naibu Spika, kama walivyoliona Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati suala la kuwa na sehemu maalum ya kufanyia uchunguzi wa dawa za kulevya na kituo ch Polisi katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar ni suala muhimu na litazingatiwa katika ujenzi wa jengo jipya la abiria unaoendelea hivi sasa, tayari Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wameshajuilishwa kuhusu suala hili na wanaendelea kulifanyia kazi.

Agizo namba 39

Ni muhimu kwa serikali kuchukua hatua za kutoa miongozo na maagizo ya kulinda amani kwa kutumia sheria, kama sheria hazipo, basi kuna haja ya kutungwa. Hata hivyo jambo la msingi ni kuwapatia wananchi elimu ya uraia na masuala ya kulinda amani katika jamii. Mhe. Naibu Spika, suala la kuwashirikisha wananchi katika kulinda amani katika jamii ni suala linalotiliwa mkazo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Suala hili linakwenda sambamba na kutoa taaluma kwa jamii juu ya umuhimu wa kutii sheria bila shuruti na kufanyia mapitio na marekebisho ya sheria mbali mbali za nchi ili ziendane na wakati ulionao hivi sasa.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kukushukuru wewe binafsi na wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano mnayotupatia katika Ofisi yetu. Ninamshukuru Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa ushauri na maelekezo yao yanayotusaidia sana katika kufanikisha majukumu ya ofisi yetu. Ni imani yangu kwamba wajumbe wamefatilia kwa makini maelezo niliyoyatoa ambayo yamefafanua utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika ripoti ya mwaka 2012/13.

Mhe. Naibu Spika, na wajumbe naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Wazirim kwa hotuba yako ya kina na umeiwasilisha kwa ufasaha mkubwa. Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa mashirikiano yenu mlionipa hivi jioni na ripoti zilizobakia zitawasilishwa siku ya jumatatu. Kwa hivyo, ninakhirisha kikao chetu hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 27/01/2014 saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 1.50 usiku Baraza liliakhirishwa hadi siku ya Jumatatu
Tarehe 27/01/2014 saa 3.00 asubuhi)